

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 5 Novemba, 2019

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae sasa.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada minne ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

Kwanza, Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019 (*The e- Government Bill, 2019*).

Pili, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2019 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4, Bill, 2019*).

Tatu, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2019, (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 5, Bill, 2019*).

Nne, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2019, (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 6, Bill, 2019.*)

Kwa Taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge kwamba tayari Miswada hiyo minne imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi, sasa zimekuwa sheria za nchi zinazoitwa kama ifuatavyo;- (*Makofi*)

Sheria ya kwanza, ni Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 (*The e-Government Act No. 10 of 2019.*)

Ya pili, ni sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 4, Sheria Na. 11 ya Mwaka 2019 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4, Act No. 11 of 2019;* na

Tatu, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2019, (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 5, Act No. 11 of 2019,* na Sheria ya Marekebisho ya sheria mbalimbali Na. 6, Sheria Na.13 ya MWaka 2019 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 6, 2019.*)

Katibu tuendelee!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekozo Mapendekozo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa 2020/2021.

MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapendekozo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

SPIKA: Ahsante sana tunakushukuru Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuwasilsha hiyo. Waheshimiwa Wabunge niwaambie tu Watanzania kwamba Bunge letu limepiga hatua nyingine tena katika matumizi ya teknolojia wataona Waheshimiwa wote waliokuja hapa wana mitambo kama hii mezani na kwa kiwango kikubwa sana tunapunguza matumizi ya karatasi sasa ni mambo ni Mtandao tu moja kwa moja. (*Makofî*)

Kwa hiyo tunatoa wito kwa Taasisi nyingine za Umma nazo kwenda namna hiyo na wote ambao wanajianaa kushughulika na Bunge, iwe wanakuja kutoa semina shughuli yoyote wajiandae kuja kimtandao mtandao.

Baada ya hilo kabla hatujaanza maswali kwa vile leo ni siku ya kwanza Waheshimiwa Wabunge niwashukuruni sana tuliendo salama tumerudi salama, sina taarifa mbaya yoyote ile, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu karibuni Dodoma tuendelee na kazi ya uwakilishi wa wananchi. Jambo moja tu kabla hatujaanza maswali tulikuwa na semina Arusha wiki kama moja iliyopita ambayo ilikuwa ni semina inayohusu Mabunge ya Jumuiya ya Madola kuhusiana na mada inayosema ‘uongezaji wa Ushiriki wa Wanawake Katika

Michakato ya Uchaguzi' lilikuwa inahusisha Mabunge ya Afrika nzima.

Katika semina hiyo tulijifunza mambo mengi; moja wapo katika kukumbushana tu nataka kutumia dakika mbili katika jambo hili. Ni kwamba baada tu ya uhuru mwaka 1961 Bunge lile la kwanza lile kati ya 1961/1965 lilikuwa na Wabunge 81 jumla, kati ya Wabunge hao 81 Wabunge wanawake walikuwa sita tu. Kwa hiyo, walikuwa asilimia 7.4 mwaka 1961 Wabunge 81 wanawake sita; liliofuata la mwaka 1965 hadi 1970 miaka mitano ile waliongezeka Wabunge wote kuwa 183, Wabunge wanawake wakapungua wakawa watano wakati ule ili uingie Bungeni lazima uwe Mbunge wa Jimbo.

Kwa hiyo wameendelea namna hiyo kwa asilimia kiasi kwamba tangu uhuru jumla ya Wabunge wote ambao wamepata kuingia katika Bunge tangu uhuru ni 3041na katika hiyo 3041 Wabunge tangu uhuru ambao wameingia Bungeni wakiwa wamake ni 484 ambayo ni asilimia 15. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kuna ongezeko kubwa katika 3484 nadhani siyo haba asilimia 15 ya Wabunge wote na ni kwa sababu kule nyuma kulikuwa na tofauti kubwa ndiyo maana sasa hivi japo tumesogea sana lakini bado hatujafika mbali.

Sasa kwa upande wa vyama chama cha Mapinduzi na Upinzani idadi ya Wabunge wote tangu uhuru wa CCM ni 1294. Idadi ya Wabunge wanawake toka uhuru ni 256. Kwa hiyo CCM tangu uhuru kati ya Wabunge wote imeingiza wanawake asilimia 19.8 tu. (*Makofi*)

Tangu uhuru Wabunge wote wa upinzani wa vyama vyote vyta Upinzani ni 328; tangu uhuru idadi ya Wabunge wanawake wa Upinzani ni 124. Kwa hiyo, Upinzani umeingiza humu asilimia 40.3, Upinzani umeingiza wanawake asilimia 40.3, CCM imeingiza asilimia 19.8 ya Wabunge wote. Kwa hiyo, bado tuna kazi ya kufanya ili kuwezesha akinamama zaidi kuititia vyama vyetu vyote tuweze kufikia malengo yale ambayo tulikuwa tunayahitaji.

Katibu tusonge mbele!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

Ajira Kwa Vijana Waliohitimu Vythuo Vikuu Nchini

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. ANNA J. GIDARYA) aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Serikali imekaa kimya kuhusu ajira kwa vijana, kumekuwa na wimbi kubwa la vijana mitaani wasio na ajira waliomaliza vyuo mbalimbali takriban miaka mitatu illyopita.

(a) Je, ni lini Serikali itafungua milango ya ajira kwa vijana wa Kitanzania walioneseka kwa muda mrefu?

(b) Je, Serikali imefanya tathmini ya kiwango cha madhara yaliyotokana na vijana kukosa ajira?

(c) Je, ni vijana wangapi wameathirika na kujingiza katika makundi mabaya kwa kukata tamaa ya kupata ajira?

SPIKA: Kabla ya majibu hayo pia Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwenye Bunge illopita tulipitisha azimio la kumpungeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Baada ya kufanya jambo hilo jema la kumpungeza kiongozi wetu amekuandikieni barua ambayo ningependa niisome kufuatia azimio hilo. (*Makofii*)

Anasema Mheshimiwa Spika nimepokea kwa moyo wa furaha na shukrani Azimio la Bunge Na. 2, 2019 liliopitishwa tarehe 3, Septemba 2019. Mheshimiwa Rais anaendelea kusema kwa kweli nimefarijika sana kuona Bunge lako Tukufu

linatambua mchango wangu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia kama Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. (*Makofî*)

Ameendelea kusema ni wazi kwamba mafanikio yoyote katika uongozi hayawezu kuletwa na kiongozi mmoja peke yake bali ni matokeo ya jithada za pamoja. Hivyo basi, wakati nikizipokea pongezi zenu kwa moyo wa unyenyekevu kabisa, nalishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa linaota kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika naomba uzifikishe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja tunajenga Taifa Mheshimiwa John Pombe Magufuli. (*Makofî*)

Kwa niaba yenu narudisha tena salamu za shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa ushirikiano anaotupatia Katika kuendesha Bunge letu, ahsante sana.

Sasa naomba nimuite Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Antony Mavunde ujibu hili swali la Mheshimiwa Anna Gidarya. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya Mbunge wa (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008, Miongozo ya ILO na Kikanda, Ajira inajumuisha shughuli zinazokubalika kisheria ambazo ni za uzalishaji mali, zenyenye kufanikisha malengo ya kazi zenyenye staha na zinazozalisha kipato. Hivyo, ajira ni hali ya mtu kuajiriwa au kujiajiri kwa ajili ya kujilingizia kipato halali.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kama mmoja wa waajiri wakuu imeendelea kuajiri kupitia Taasisi zake mbalimbali kila mwaka kwa kuzingatia mahitaji na bajeti. Hata hivyo, kupitia Sera na Mipango mbalimbali ya Serikali katika kuchochaea Uwekezaji na Viwanda, shughuli nyingi za kiuchumi zimeongezeka hali ambayo pia imesaidia katika upatikanaji wa nafasi za ajira hasa katika kundi hili kubwa la vijana. Utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati imekuwa ni chachu kubwa katika kuongeza wigo mpana wa upatikanaji ajira. Kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2018/2019 jumla ya ajira Serikalini ikijumuisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma zilikuwa 184,141. Aidha, katika ajira za miradi ya maendeleo ya Serikali zilikuwa 787,405, na ajira zilizozalishwa na Sekta Binafsi zilikuwa ni 646,466.

(b) Mheshimiwa Spika, Ni dhahiri kwamba ukosefu wa ajira kwa vijana una madhara kiuchumi na kijamii. Ukosefu wa ajira unapunguza mchango wa nguvukazi isyo na ajira katika Pato la Taifa pamoja na jitihada za Serikali kupunguza umasikini. Aidha, kunapunguza uwezo wa nguvukazi hiyo kuweza kujitegemea na kuendelea kuwa tegemezi kwa jamii. Ili kupunguza tatizo hilo Serikali imeandaa mikakati mbalimbali za kuwawezesha vijana kuajiriwa au kujajiri. Mikakati hiyo ni pamoja na utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini ambayo katika kipindi cha Mwaka 2017-2019 jumla ya vijana 47,585 wamevezeshwa kiujuzi na kujajiri katika sekta mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la vijana kujingiza katika makundi mabaya ni suala la maadili na makuzi. Serikali kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana imekuwa ikiandaa miongozo ya maadili na makuzi kwa vijana na imekuwa ikiendesha mafunzo hayo kwa vijana nchini.

SPIKA: Ahsante kabla sijamuita Mheshimiwa Anna Gidarya au ambaye umemuuliza swali lake, naomba niwajulisheni Waheshimiwa Wabunge kwamba huu Mpango wa Taifa na Mwongozo wake ambao tutajadili muda siyo mrefu ujao tayari umeshatumwa katika vitendea kazi vyenu.

Kwa hiyo *click refresh* mambo yatakuwa mswano tunasonga mbele, Mheshimiwa Selasini nilikuona.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Serikali kwamba kuna mikakati fulani inafanywa kwa ajili ya kuwasaidia vijana. Vilevile sehemu kubwa ya kukosekana kwa ajira za vijana inatokana na mitaala mibovu. Tunakubaliana kwamba zamani tulikuwa na elimu ya kujitegemea ambayo ilikuwa inawasaidia vijana kuwa na *skills* baada ya kumaliza shule, lakini hilo sasa halipo:-

Je, Serikali iko tayari kuangalia upya mitaala ya vijana wetu ili wanapomaliza shule wawe tayari wana utaalamu wa namna fulani ambao utawasaidia kujajiri?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ni kwamba, wako vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu wana uwezo wa kufanya kazi lakini wanakosa mitaji; na nilishaomba hapa Bungeni, ni kwa nini Serikali isitengeneze utaratibu au sheria ambapo vyeti vya hawa vijana vitatumika kama dhamana ili vijana hawa wakopesheke waweze kuwa na mtaji wa kuanzisha mambo ambayo yanaweza kuwategemeza kama kilimo, biashara na kadhalika?

SPIKA: Ahsante sana. Swalii la kwanza nadhani Profesa, Waziri wa Elimu angeweza kulipitia halafu la pili Mheshimiwa Naibu Waziri atalijibu. Mheshimiwa Ndalichako tafadhali kuhusu mitaala.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Selasini. Kwanza napenda kutoa ufanuzi kwamba bado Elimu ya Kujitegemea inaendelea shulenii.

Kwa hiyo, kama kuna sehemu ambazo Elimu ya Kujitegemea haifanyiki, ni kwa sababu tu labda wahusika katika maeneo husika wanalegalega. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa walimu kuhakikisha kwamba elimu ya kujitegemea inaendelea shulenii.

Mheshimiwa Spika, katika mitaala yetu, tunalo somo la stadi za kazi ambapo lengo la somo hilo ni kujenga utamaduni wa watoto wadogo (wanafunzi) kupenda kazi na kuweza kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa wanafunzi kujifunza kujitegemea na tunayo katika mitaala yetu. Kwa hiyo, cha msingi ni kuhakikisha kwamba inatekelezwa kama ilivyopangwa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde tafadhali, majibu ya swali la pili la Mheshimiwa Selasini.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Selasini Mbunge wa Rombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mikakati ya Serikali kwenye kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira hasa kwa vijana wahitimu wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu, mkakati tulio nao hivi sasa, tumeanza kuwahamasisha vijana kupiditia fani zao kukaa katika vikundi na kuunda makampuni na Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikiwasaidia kufikia katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kwamba baada ya kuhitimisha hatua hizo za awali, waweweze kuwezesha kupiditia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kupiditia asilimia 10 ya mapato ndani ya Halmashauri na Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ipo kampuni moja ya vijana wahitimu wa Chuo Kikuu pale Sokoine, Morogoro ambao walihitimu katika kilimo wakakaa pamoja, Serikali tukawawezesha. Hivi sasa, juzi kampuni hiyo imeshinda tenda katika Ofisi ya Waziri Mkuu ya kiasi cha shilingi bilioni nne katika

masuala ya kilimo. Huo ni mfano ambao upo hai. Kwa hiyo, nitoe rai kwa vijana wengine wote nchi nzima kujikusanya kwa pamoja Serikali tutakuwa nao kuhakikisha kwamba wanafikia malengo yao.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo litaakea Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa litakaloulizwa na Mheshimiwa Hassan Selemani Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini. Mheshimiwa endelea kuuliza swali lako.

Na. 2

Mikopo na Posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH (K.n.y. MHE. HASSAN S. KAUNJE) aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itawadhamini Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ili waweze kupata mikopo kama ilivyo kwa Madiwani na Wabunge?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa posho/mishahara Wenyeviti wa Serikali za Mitaa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inalipa posho ya Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kuitia asilimia 10 ya mapato ya ndani yanayorejeshwa na Halmashauri kwenye Vijiji na yanayokusanya kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Madiwani, Wabunge hudhaminiwa kupata mikopo kwenye mabenki na taasisi za kifedha kuitia

posho za kila mwezi ambacho ni kipato chenye uhakika kuwezesha kurejesha mikopo hiyo waliyokopa.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuziwezesha Halmashauri kubuni vyanzo vipyta ya mapato ili kuimarisha makusanyo ya ndani katika vyanzo mbalimbali na kuimarisha uwezo wa Halmashauri kulipa posho hizo kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Ahsante.

SPIKA: Muuliza swali, swali la nyongeza

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni kiongozi wa kwanza wa ngazi ya Mtaa, lakini ukiangalia kazi kubwa anayoifanya katika kusimamia majukumu mbalimbali ya maendeleo pamoja na kuwanganisha wananchi kwenye Mtaa wake pamoja na kusimamia ulinzi na usalama kwenye Mtaa wake, kiwango cha posho wanazopewa na Halmashauri ni kidogo...

SPIKA: Sasa swali.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, napenda kujua, ni lini sasa Serikali itaongeza kiwango hiki cha posho wanayopata ya shilingi 10,000/= kulingana na kazi ambayo wanaifanya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza, napenda kujua kwamba Waheshimiwa Madiwani sasa wanadhaminiwa kukopeshwa mikopo kutoka kwenye vyombo vya fedha: Ni lini sasa Serikali itasimamia kuhakikisha kwamba Wenyeviti nao wanakopeshwa katika vyombo vya fedha? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anazungumzia kiwango cha posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Kama ambavyo nimejibu kwenye swali langu la msingi ni kwamba ni kweli kwamba Wenyeviti hawa wa Vijihi, Vitongoji na Mitaa wanafanya kazi kubwa na Serikali inawadhamini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, mapato ambayo wanapewa ya asilimia 20 ni makusanyo katika Halmashauri husika. Hivi viwango vyahili 10,000/=, shilingi 20,000/=, shilingi 50,000/= mpaka shilingi 100,000/= vinategemeana pia na uwezo wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote, kadri tunavyokuwa tunabuni vyanzo mbalimbali kwenye Halmashauri zetu, zkipata uwezo mkubwa Wenyeviti hawa watapata posho kulingana na mapato ya ndani kulingana na Sura ya 290 ya fedha za Serikali za Mitaa kama nilivyoleta.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anauliza ni lini Wenyeviti wataanza kupata mikopo? Yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge amesema hiki kiwango ni kidogo na wakati mwingine ni kweli kwamba Wenyeviti wa Mitaa wanaendelea kudai. Kwa hiyo, namna ya kurejesha ukikopeshwa fedha benki inakuwa na ugumu wake, inaonekana mapato pia hayana uhakika. Halmashauri wanaweza wakapata kiasi kidogo, wakapata kidogo. Wakati mwingine kulingana na msimu wakapata fedha nyingi, wakapata nyingi kidogo. Sasa mabenki yatakuwa ni ngumu sana kuweza kuwawezesha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuja na mpango wa kuwawezesha Halmashauri kuwa na miradi ya kimkakati, Halmashauri ikiwa na uwezo mkubwa wa kutosha kuanzisha kama masoko, stendi na vitu vingine vile vikubwa itawawawezesha Halmashauri kuwa na uwezo, kuwa na kipato cha uhakika na Wenyeviti wetu watakopeshwa na

watasimamiwa na Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yao ya kazi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa *Senator Lubeleje*. Shangazi tulia, *Senator amesimama kule*. (*Kicheko*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka 2000 mpaka 2010 Serikali iliunda Tume ya Kushughililia maslahi ya Madiwani na tume hii iliongozwa nami na ilitwa Tume ya Lubeleje kwa ajili ya maslahi ya Madiwani, kwamba Madiwani waongezwe posho kulingana na majukumu yao:-

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unasema nini kuhusu kuongeza posho ya Madiwani pamoja na kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu toka kwa *Senator Lubeleje*. Ni kweli Kamati hiyo ilikuwepo, mimi mwenyewe ni shuhuda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ni nia na lengo kubwa la Serikali ikiwa na uwezo mkubwa unaotosha tungependa kuongeza posho hii ya Waheshimiwa Madiwani ili waweze kujikimu kulingana na kazi wanazofanya katika Halmashauri zetu ambazo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, swali la msingi hapo mwenyewe umeshuhudia, Mheshimiwa Mbunge anauliza, ni lini Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji wataongezwa posho?

Mheshimiwa Spika, nchi hii tuna mitaa zaidi ya 4,200 na kitu hivi; tuna vijiji zaidi ya 12,000; tuna vitongoji zaidi ya 64,000; na kila mtaa una Wajumbe sita, Kijiji kina Wajumbe 25. Ukipiga hesabu kwa ujumla wake, ni watu wengi kweli

kweli; ongeza Madiwani wa Kata na Madiwani wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Madiwani waendelee kuchapa kazi, Serikali ya CCM inawaheshimu sana. Uwezo ukipatikana watapata posho, lakini tumeelekeza Halmashauri, wale Madiwani ambao wanadai posho zao na kukopwa, wasikopwe, walipwe kile ambacho kinawezekana kupatikana ili wachape kazi yao. Nakushukuru sana.

SPIKA: Nakuruhusu Mheshimiwa swali la mwisho la nyongeza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana katika maeneo yetu lakini wengi wao hawana ofisi na wengineo wanatumia nyumba zao kama ofisi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Wenyeviti wetu wanapata ofisi ili waweze kufanya kazi zao vizuri sana katika Halmashauri zetu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ni kweli kuna baadhi ya maeneo ambayo Wenyeviti wetu wa Vijiji na Mitaa hawana ofisi, lakini wengine wamepanga katika nyumba za watu binafsi na wakati mwingine wanalazimika kufanya kazi hizo za kuhudumia wananchi katika majengo yao binafsi. Maelekezo ya Serikali ni kwamba Wenyeviti wa Mitaa ofisi zao zinasimamiwa na Halmashauri na Wakurugenzi katika maeneo yao, kwa sababu Watendaji wa Mitaa na Vijiji ni Wawakilishi na wanafanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nielekeze Halmashauri zote, kwenye bajeti zao za kila mwaka lazima watenge bajeti

ya kujenga ofisi hata kama siyo zote, ndiyo maelekezo. Nasi tunaendelea kufuatilia na tuna taarifa za Halmashauri kuna baadhi wameanza kujenga ofisi hizo kwa kupitia michango mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge pia, nimeona kwenye taarifa kwamba kwenye Mfuko wa Jimbo baadhi ya Wabunge tena wengine wa Viti Maalum wamechangia ujenzi wa Ofisi za Mitaa na Vijiji, lakini kuweka zana kama *photocopy machine* na kusaidia utendaji uweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, tuwahimize Wakurugenzi kile kinachopatikana kila mwaka kwenye bajeti yao na Waheshimiwa Wabunge wafuatilie, tutenge kiasi kidogo ili kuweza kupunguza shida za Ofisi za Wenyeviti wetu wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Bahati nzuri Waziri wa TAMISEMI naye amekuja. Hili suala la posho za Madiwani napenda kuwashauri Waheshimiwa wa TAMISEMI; Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa na nini, lina matatizo makubwa sana ambayo ufumbuzi wake ni ninyi TAMISEMI. (*Makof!*)

Hii lugha ya kusema kwamba kila Halmashauri ilipe kufuatana na uwezo wake, hili ni tatiizo kubwa. Kwa mfano, nina Mamlaka za Miji Midogo mbili; Kibaigwa na Kongwa. Kibaigwa wanalipa kiasi fulani labda mara mbili, wa Kongwa analipwa nusu yake. Huyo anayelipwa nusu, anasema kwa nini wale wamelipwa vile sisi mnatalipa hivi? Yaani ni migogoro! Kwa nini pasiwe na mwongozo tu kwamba kipengele fulani malipo ni haya nchi nzima. Hakuna cha uwezo wala nini. Uwezo wa nini? Malipo yajulikane, Madiwani wanalipwa nini? Kipengele hiki unakuta Chemba wamelipwa hivi, Kongwa walipwa hivi. Kwa sababu ya simu za siku hizi, wanaulizana, ninyi mmelipwa ngapi? Sisi tumelipwa shilingi 200,000/=; kwa nini sisi shilingi 100,000/=? Mgomo, watu wanavunjika moyo. (*Makof!*)

Sasa kwa nini malipo yasijulikane tu? Kama Chembu shilingi 100,000/= na Kongwa shilingi 100,000/=, Kondoa 100,000/= basi. TAMISEMI inatakiwa itoe huo mwongozo. Hii ya kusema kwamba mwenye uwezo alipe anavyotaka, asiyekuwa na uwezo naye aendelee kujikaanga, kidogo naomba TAMISEMI uliangalie sana hili. Sisi siasa yetu ni ya Ujamaa na Kujitegemea, huwa zaidi tunaenda kwa usawa usawa hivi. Nyie toeni mwongozo kama Serikali malipo ni haya, migogoro yote hamtaisikia. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Said Bungara

Na. 3

**Kutatua Changamoto Zinazokabili Kituo cha Afya Kilwa
Masoko**

MHE. SELEMANI S. BUNGARA aliuliza:-

Kituo cha Afya Kilwa Masoko kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uhaba wa watumishi, upungufu wa dawa, upungufu wa vitanda, magodoro, mashuka, vifaa tiba, kipimo cha sukari, kipimo cha damu, uchakavu wa majengo na pia kituo hicho hakina gari la kubebea wagonjwa hali ambayo ni kero kubwa kwa wagonjwa wanaohamishiwa Hospitali ya Wilaya iliyo umbali wa zaidi ya kilometra 25:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto zinazokabili Kituo hicho cha Afya ili kuondoa adha kwa wananchi?

SPIKA: Bado tuko TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa

Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kilwa Masoko kilipatiwa kiasi cha shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi ambapo ujenzi na ukarabati wa majengo sita ya kituo umekamilika. Aidha, baada ya ujenzi na ukarabati kukamilika, kituo kimepokea vifaa tiba mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma hususan za upasuaji ambapo hadi Oktoba, 2019 kituo kimepokea vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 332,916,070/=. Hali ya upatikanaji wa dawa zote muhimu (*Tracer medicine*) katika Kituo cha Masoko ni asilimia 87.

Mheshimiwa Spika, kituo kina jumla ya watumishi 30 wa kada mbalimbali za Afya ikiwa ni upungufu wa watumishi 22. Kituo kina nafasi ya vitanda 55, vitanda vilivyopo ni 31 na mashuka 126. Idadi ya vitanda vilivyopo vinakidhi mahitaji kwani kwa sasa kituo kinapokea wagonjwa wa kulazwa angalau watano kwa siku. Kwa sasa Halmashauri ina gari maalum ambalo hutumika kubeba wagonjwa katika kipindi cha dharura.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta rasilimali fedha za kutatua changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kilwa Masoko.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Bungara nimekuona.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana na ninakupongeza kwa kutupatia *tablet* hizi. (*Makofi*)

Pili, hili swali niliuliza mwaka 2016, lakini naishukuru Serikali leo wamejibu kwa vitendo. Kweli Kituo cha Afya Masoko sasa hivi utasema upo Ulaya, nashukuru sana. Pamoja na shukrani hizo; je, ni lini Serikali itatimiza au itakamilisha

wafanyakazi 22 waliobakia ili kituo kiendane sawasawa na kilivyo? Swali la kwanza hilo.

Swali la pili; kwa kuwa hakuna gari maalum ya wagonjwa hiyo unayosema, lakini kwa kuwa umenipa matumaini kwamba mtatafuta gari nyingine: Je, lini hiyo gari ya Kituo cha Afya cha Kilwa Masoko itapatikana?

SPIKA: Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kendege, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, niruhusu nipokee pongezi za Mheshimiwa Bungara, maana huwa zinatolewa mara chache sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza anauliza ni lini upungufu wa watumishi 22 utatatuliwa ili hadhi ya Kituo cha Afya ambacho anasema ni sawa na kuwa Ulaya kitaweza kutoa huduma kukiwa na ikama ambayo inatakiwa?

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo ameendelea kuiamini Serikali ya CCM ikiahidi inatekeleza na utekelezaji ni pamoja na swali ambalo aliliuliza, nami nampongeza kwa kuuliza swali na Serikali tumemjibu kwa vitendo. Naomba nimhakikishie ni azma ya Serikali kuhakikisha maeneo yote ambayo Vituo vya Afya vimefunguliwa tunapeleka watumishi kwa kadri nafasi za ajira zinavyopatikana na Kilwa hatutasahu.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anaulizia suala la kuwepo gari. Gari liliopo aina ya Maruti linafanya kazi, lakini kama tulivyokiri katika majibu yetu kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunapata gari zuri zaidi kwa kushirikiana Halmashauri yake, ni vizuri nao katika bajeti; maana kama kuna Halmashauri ambayo inafanya vizuri katika makusanyo ni pamoja na Halmashauri yake maana zao la ufuta linaingiza fedha nyingi. Ni vizuri nao Halmashauri

wakatenga na sisi Serikali tukashirikiana ili gari ziweze kupatikana kwa ajili ya wananchi.

SPIKA: Kabla hatujaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Waheshimiwa Wabunge tuwiane radhi, matangazo yatakuwa mengi mengi kwa sababu tuko mwanzo wa mambo haya.

Kwa kawaida ukiwa umeuliza swali lako na limepangwa siku hiyo katika orodha ya shughuli, huwa asubuhi tunakupatia karatasi ya majibu ya Serikali. Nafikiri mnakumbuka jambo hilo. Sasa badala ya karatasi ya Serikali, majibu yale tutakutumia wewe mwuliza swali kwa njia ya mtandao, asubuhi ile utayapata.

Sasa kama hutakuwa Bungeni, ni vizuri ukaiharifu Ofisi ya Bunge mapema asubuhi ile ni nani ambaye atauliza swali kwa niaba yako ili huyo atakayeuliza swali kwa niaba yako naye atumiwe hayo majibu ili hata anapouliza swali la nyongeza awe kwa kweli swali lake la nyongeza linaendana na lile swali na wakati mwininge anakuwa ameshawasiliana na Mbunge mwenyewe kuweza kuona swali la nyongeza lifananaje. Natumaini itatusaidia katika kufanya maswali ya nyongeza yaendane na swali la mwuliza swali la msingi jambo ambalo ni jema zaidi.

Mheshimiwa Obama Ntabaliba, swali la Manyovu ambalo Mheshimiwa Mpango anatakiwa ajibu kuhusu kituo cha forodha. (*Kicheko*)

Na. 4

Serikali Kutumia Kituo cha Forodha cha Manyovu

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutumia Kituo cha Forodha Manyovu ili kuitisha mizigo kwenda Burundi kwa kiwango cha kutosha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali, Kituo cha Forodha Manyovu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Forodha Manyovu kinatoa huduma za forodha mpakani mwa Tanzania na Burundi katika Mkoa wa Kigoma. Kituo hicho kinatoa huduma kidogo ikilinganishwa na uwezo wake kwa sababu ya changamoto ya umbali wa *transit route* ya Dar-es-Salaam hadi Burundi kupitia Manyovu.

Mheshimiwa Spika, umbali wa *transit route* ya Dar-es-Salaam – Isaka – Nyakanazi hadi Manyovu ni kilometra 1457 wakati *transit route* ya Dar-es-Salaam – Isaka – Nyakanazi hadi Kabanga ni kilometra 1330. Tofauti ya umbali kati ya *transit route* ya Kabanga na Manyovu ni kilometra 127. Aidha, *transit route* ya Dar-es-Salaam – Manyoni – Tabora hadi Manyovu ni kilometra 1273, lakini *route* hii pia inakabiliwa na changamoto ya ubovu wa sehemu ya barabara ambayo haijajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ya umbali wa *transit route* ya Dar-es-Salaam - Isaka - Nyakanazi - Manyovu pamoja na ubovu wa sehemu ya barabara ya *transit route* ya Dar-es-Salaam – Manyoni – Tabora - Manyovu wafanyabiashara wengi hutumia Kituo cha Forodha Kabanga ili kuokoa sehemu ya gharama ya usafiri na usafirishaji.

Aidha, pamoja na changamoto hizi, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Kituo cha Forodha Manyovu kimeunganishwa na Mfumo wa Forodha wa Uthaminishaji Mizigo wa *TANCIS* na kina uwezo wa kutoa huduma za kiforodha kwa wakati na kwa ufanisi wa hali ya

juu. Vilevile, taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Uhamiaji, Polisi na Wizara ya Kilimo zimeanzisha Ofisi katika kituo hicho kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za kiforodha.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kwamba huduma za forodha katika Kituo cha Forodha Manyovu zitaimarika zaidi baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa vipande vyta barabara ya Manyoni – Tabora – Uvinza; ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa, pamoja na mradi wa ukarabati wa Bandari ya Kigoma.

SPIKA: Mheshimiwa Obama Ntabaliba, swali la nyongeza.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hili. Naishukuru Serikali kwa majibu yao mazuri kabisa, sina wasiwasi na majibu kwani mmejibu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa inavyoonekana *future transport logistic* kati ya Tanzania na Burundi itapitia Manyovu. Ameonesha kabisa kwamba Dar-es-Salaam – Kabanga ni kilometra 1330 na Dar-es-Salaam – Tabora – Manyovu ni 1273, kwa hiyo, katika mpango wetu wa *Blueprint* na *Easy of Doing Business* inaonesha kwamba siku za mbele wafanyabiashara watapitia Manyovu kupitia Tabora. Kwa kuwa iko hivyo, ni maandalizi gani sasa mmeyafanya kwa ajili ya kupokea biashara hiyo? Najua Serikali mtaendelea kujitahidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, amesema kuna changamoto ya barabara kwa ajili ya kurahisisha biashara kwenda Burundi. Je, Wizara ya Ujenzi ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hivi vipande vyta barabara vinaisha haraka?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, tafadhalii.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kitu cha kwanza Mheshimiwa Obama anawatetea kweli ndugu zetu kule, napenda tu nimjulisse kwamba katika utaratibu wa ujenzi wa barabara ambayo inatoka Burundi - Manyovu – Kasulu - Nyakanazi, moja ya vipengele vya barabara ile baadhi ya huduma ambazo zitajengwa kwa fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika ni pamoja na kujenga Kituo cha Pamoja cha Forodha pale Manyovu ambacho kwa hakika itakuwa ni mkombozi wa kuharakisha biashara kati ya Tanzania na Burundi.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa upande wa Wizara ya Ujenzi pamoja na sisi kama Wizara ya Fedha karibu tumekamilisha jithada za kupata fedha za kukamilisha vile vipande ambavyo vimebakia vya barabara ambayo inatoka Manyoni - Tabora - Kigoma. Fedha zimekwishapatikana, tunakamilisha taratibu za ujenzi kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Obama bahati mbaya Mbunge wa Ngara hayupo.

WABUNGE FULANI: Yupo.

SPIKA: Mheshimiwa Obama anasema lazima ile *route* ipite Manyovu na siyo Kabanga. Swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge wa Ngara. (*Kicheko*)

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mbali na Kituo cha Kabanga, kuna Kituo kidogo cha Forodha cha Murusagamba ambacho kinalelewa na Kituo cha Kabanga. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupandisha hadhi Kituo hiki cha Murusagamba ili kiweze kuwa kituo kamili hasa kwamba upo mkakati wa kuunganisha barabara ya lami kutoka Nyakahura - Murusagamba - Burundi *route* ambayo pia itaendelea kuwa karibu? (*Kicheko*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui kama maeneo hayo unayafahamu au tumuachie Waziri mwenyewe? Karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa hivi ina Vituo vya Forodha vipatavyo 97 na upandishwaji wa Vituo vya Forodha kutoka kuwa vituo vidogo kuwa vituo kamili vya forodha huwa vina *criteria* yake ambayo na Kituo cha Murusabanga nacho tutaendelea kukifanya kazi na tathmini. Kikidhi vigezo vya kupandishwa hadhi na kuwa kituo kamili cha forodha kutokana na shuguli nyingi za kiuchumi zinazofanyika maeneo yale, Serikali haina shaka kikipandisha kituo hicho na Mheshimiwa Mbunge wa Ngara tuko tayari kufika tuweze kufanya tathmini hiyo.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Madini na swali linaulizwa na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza, nikuombe kwa ruhusa yako nikupongeze wewe na ofisi yako kwa ubunifu uliouonesha wa kutusaidia na kutusababisha Wabunge wako kuepuka kuandikaandika kwenye makaratasil, sasa tunatumia *tablets*. Naamini kabisa kwa hili ulilolionesha inaonekana baadaye pia kuna mambo utatufanyia kabla hatujaenda majimboni ili wananchi watupokee vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba swali langu namba 5 lijibiwe.

Na. 5

Mgodi wa ACACIA Kuwalipa Fidia Wananchi

MHE. AGNESS M. MARWA aliuliza:-

Wananchi wengi walibomolewa nyumba zao na Mgodi wa ACACIA uliopo Nyamongo, Wilayani Tarime na wengine hawajalipwa fidia ya maeneo yao mpaka sasa. Aidha, mgodi pia umeanza kuchimba chini ya maeneo ya watu (*Underground mining*):-

Je, ni lini mgodi wa ACACIA uliopo Nyamongo utalipa fidia kwa wananchi hawa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, tafadhali.

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia sekta ya madini kwa kuhakikisha uwekezaji unafanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi ikiwemo kuhakikisha kuwa wananchi wanaishi katika maeneo ambayo miradi ya uendelezaji migodi inataka kufanyika na kulazimika kupisha maeneo yao wanalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na wanapewa makazi mbadala ambayo yana hali bora zaidi kuliko makazi waliyokuwa nayo awali.

Mheshimiwa Spika, uthaminishaji katika maeneo yanayozunguka mgodi wa North Mara na ulipaji wa fidia umegawanyika katika awamu nyingi kwa kuzingatia vijiji husika kuridhia. Kijiji cha Nyabirama chenye wakazi 1,974 waliothaminiwa katika awamu ya 20, 35 na 42 wote walilipwa fedha zao isipokuwa wakazi 64 ambaa fedha yao iliyoidhinishwa ya shilingi bilioni 1.9 waliikataa hundi zao zikabaki Ofisi ya Mkurugenzi Wilaya ya Tarime. Eneo la Nyabichune lilithaminiwa katika awamu ya 47 kwa kuidhinisha shilingi milioni 224 kwa ajili ya watu 69. Wizara iliagiza uthamini wa maeneo hayo ya Kijiji hicho cha Nyabichune urudiwe kwa sababu wananchi wale walionekana wamepunjwa. Mthamini Mkuu wa Serikali ameshakamilisha uthaminishaji wa

maeneo 1,838 ambayo tayari umeshawasilishwa kwenye menejimenti ya mgodi kwa hatua zake za ulipaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mgodi kubadilisha aina ya uchimbaji toka uchimbaji wa wazi (*open pit*) kwenda *underground mining*, uamuzi huo ulifikiwa baada ya mgodi huo kufanya utafiti ulioonesha kuwa gharama ya uchimbaji wa chini zilikuwa ndogo ukilinganisha na uchimbaji wa mgodi wa wazi. Naomba niwatoe shaka wana Tarime kuwa Wizara inafuatilia kwa karibu uchimbaji unaofanyika na mpaka sasa uchimbaji wa *underground* unafanyika katika eneo la Gokona kuelekea Nyabigena ndani ya maeneo waliyokuwa wakichimba toka awali. Hivyo, hakuna eneo ambalo mgodi wa *underground* unachimba kwenye makazi ya watu.

SPIKA: Mheshimiwa Agness Marwa, tafadhali.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba niulize swali moja la nyongeza lenye vipengele viwili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutokana na shilingi na vifaa vyta ujenzi kupanda thamani kila mwaka, deni la wananchi wa Nyamongo wanaodai fidia ni miaka sasa. Je, watakapolipa hizo fedha watawalipa pamoja na riba kwa sababu sasa vifaa vyta ujenzi vimepanda?

Mheshimiwa Spika, pili, kutokana na uthamini kila siku kufanyika kwa haohao wakazi wa Nyamongo lakini hawalipwi ukizingatia hali halisi kwamba na wao wana familia zao, wana watoto wanawasomesha na biashara zao na mahitaji yao ambayo yamesimama kusubiria kuondolewa katika maeneo yale. Je, Serikali ina mpango gani wa kulimaliza hili suala sasa ili wale walibaki walipwe fedha zao?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Agness Marwa kwa maswali ya huko Nyamongo, maana Mbunge wa Nyamongo ye ye wala haonekani Bungeni. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa maswali hayo yanayotetea wananchi wa Nyamongo.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agness Marwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nieleze kwamba tumekuwa karibu sana Mheshimiwa Agness Marwa kushughulikia masuala ya fidia kwa wananchi wa Nyamongo. Kwa kweli, amekuwa mstari wa mbele kuwapigania kila wakati na kutualika mara kwa mara kwenda Nyamongo kwa ajili ya kukutana na wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ziko fidia ambazo fedha zilishatolewa muda mrefu lakini bahati mbaya hazijalipwa kwa wananchi. Hii ni kwa sababu tu wako wananchi ambao walikataa zile fedha, kwa hiyo, zikawekwa Halmashauri. Kwa hiyo, nadhani si sahihi sana kuupa tena mzigo mgodi kwamba wao walipe na fidia ya *interest* kwa sababu fedha hazijachukuliwa. Wale wananchi waliokataa mwanzo walikuwa 138, wale wananchi wengine 70 wakachukua *cheque* zao wakabaki 64, niwaombe wakachukue *cheque* zao kwa sababu tayari uthamini ule ulikwishafanyika muda mrefu na fedha zao shilingi 1,900,000,000 ziko pale kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, swali lingine la pili ambalo ameuliza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba jambo hili la fidia sasa lifike mwisho. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Mgodi wa *Barrick* kuingia pamoja na Serikali kama mbia, tunachukua kila hatua kufuta yale makosa ambayo yalikuwa yanafanyika *ACACIA*. *ACACIA* walikuwa na utaratibu, mnaweza mkafanya uthamini leo kesho wakakataa kulipa tu kwa vigezo vingine. Nataka nimhakikishie kwamba tumeshazungumza na mbia mwenzetu *Barrick* anayekuja, jambo hili sasa litafika mwisho na Mthamini Mkuu ameshawasilisha vitabu vyatya uthamini ambavyo nimetaja wananchi zaidi ya 1,838 wamekwisha kufanyiwa uthamini. Kwa hiyo, tutalipa kwa wakati baada ya taratibu hizo kukamilika. Ahsante.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mheshimiwa Rhoda uliza swali lako.

Na. 8

Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Mkoa wa Katavi

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MHE. RHODA E. KUNCHELA) aliuliza:-

Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Mkoa wa Katavi ni jambo ambalo linaleta sintofahamu kwa maana ya umiliki wa eneo (Hati) na ujenzi wa Chuo ambao ni miaka sasa bado hakijajengwa na kusababisha jambo hili kuleta usumbufu kwa wanafunzi kwenda Mikoa mingine kutafuta vyuo vya killimo:-

Je, Serikali ipo tayari kuondoa sintofahamu hii ya ujenzi wa Chuo hicho cha Kilimo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, tafadhali, Elimu tuendelee.

WABUNGE FULANI: Umeruka.

SPIKA: Nitarudi kwa yale mengine, msiwe na wasiwasi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Katavi lilikuwa ni wazo la Halmashauri ya Mji wa Mpanda. Halmashauri iliingia makubaliano na Chuo cha *Royal Agricultural University* cha Uingereza kwa ajili ya utekelezaji wa azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2013 Halmashauri ya Mji Mpanda ililetu ombi la kukabidhi mradi huo kwa Wizara na walielekezwa kuwasilisha taarifa rasmi ya maendeleo ya mradi kwa ajili ya hatua stahiki. Hadi sasa Wizara hajapokea taarifa hiyo. Aidha, umiliki wa eneo hilo la chuo bado uko chini ya Halmashauri ya Mji Mpanda.

SPIKA: Muuliza swali.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na jibu la msingi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, tunaomba Serikali iweze kufuatilia majibu ya chuo hiki kwa sababu ni muhimu kwa wana-Mpanda kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama ilivyo kwa wana-Mpanda, Shirika la la Utafiti la Uyole lina kituo pale Kijiji cha Nkana katika Wilaya ya Chunya, wameanzisha utafiti kwa muda mrefu, lakini mpaka sasa Wizara ya Elimu hajjaweza kuwezesha utafiti ule kuendelea kwa ukosefu wa fedha. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika utafiti ule ili watu wa Nkana na Uyole, Mbeya, waweze kuendeleza shughuli za kilimo na kuweza kuwasaidia Watanzania? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mhesimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunchela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi lake la sisi tufuatilie kuhusu chuo hicho, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufuatilia, lakini majibu ambayo tumetoa sasa ni kwamba sisi tumeomba taarifa kutoka kwa Halmashauri ya Mji wa Mpanda lakini mpaka sasa hatujapata taarifa. Kwa sababu yeye anatokea kule, nafikiri itatusaidia sana kama angweza kusukuma kwa kushirikiana na Halmashauri yake ili tuweze kupata taaarifa hiyo ili tujue hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utafiti huo ambao anauzungumzia wa Uyole, naomba nifuatilie kwa sababu hajasema ni utafiti gani ili niweze kujua ni nini hasa ambacho kinampa changamoto Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Ahsante sana. Tunarudi Wizara ya Mifugo na Uvubi, swali Na. 6, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe.

Na. 6

Uvubi wa Kuzamia kwa Kutumia Chupa

MHE. ALI HASSAN OMAR KING aliuliza:-

Je, kwa nini uvubi wa kuzamia kwa kutumia chupa umezuilliwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo gumu sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shughuli za uvubi nchini zinasimamiwa kwa mujibu wa Sheria Na.22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 na Miongozo mbalimbali ambayo hutolewa kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha kuna matumizi endelevu ya rasilimali za uvubi. Kwa mujibu wa Kanuni ya Uvubi ya Mwaka 2009, kifungu cha 66(I – Q), vifaa vya kupumulia chini ya maji au scuba au mitungi ya gesi haviruhusiwi kutumika kwa ajili ya kuvua samaki au viumbwe wengine wa baharini. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 66(2), vifaa vya kupumulia chini ya maji au mitungi ya gesi vinaweza kutumika tu kwa ajili ya uvubi wa burudani (*sport fishing*), uvubi wa samaki wa mapambo, mafunzo na utafiti na ni kwa kibali maalum.

Mheshimiwa Spika, wavuvi haramu wanaotumia milipuko hutumia mitungi ya gesi kuzamia kwa ajili ya kukusanya samaki walowaua kutokana na milipuko hiyo. Athari za milipuko ni pamoja na kuharibu matumbawe, (*coral reefs*) na mazingira ya baharini kwenye maji ambayo ni mazalia na makulia ya samaki pamoja na viumbe wengine na hivyo kuharibu mfumo wa ikolojia ambao unatishia kutoweka kwa kizazi cha samaki. Kuua samaki bila ya kuchagua wakiwemo samaki wachanga na mayai yake na hivyo kuhatarisha uendelevu wa rasilimali za uvuvi nchini.

Pia milipuko husababisha wavuvi kupata ulemavu na hata kifo, hivyo kutokana na sababu hizi Serikali iliamua kupiga marufuku uvuvi wa kutumia chupa au mitungi ya gesi.

SPIKA: Tunataka wavuvi tu ndiyo waulize maswali hapa, Mheshimiwa Mbunge wa Jang'ombe.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesikia jawabu la Serikali, lakini ye ye amejibu mabomu hakujibu gesi. Gesi katika kuzamia haina madhara yoyote kwa sababu kwenye kina kirefu cha maji wenyewe tunaita *bahari lujii* inawezekana ikawa watu wanatumia nyavyu kwa hiyo nyavyu imekwama kule chini, kwa sababu ni kina kirefu anaweza akatumia gesi kuzamia kwenda kule. Halafu kingine, hayo mazingira ambayo anayasema Mheshimiwa Waziri kwamba yanaweza yakaharibiwa kwa mabomu kwa baharini wakati mwingine maji yanakupwa yanaweza yakafikika hata kwa miguu lakini haja ya gesi inakuwepo pale maji yanapojaa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri azidi kuniambia chupa inaharibu kitu gani alichotaja hapa ni mabomu, chupa inaharibu kitu gani, mabomu yanaweza yakategwa hata bila ya chupa. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega majibu ya swali hilo muhimu chupa ina shida gani?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Ally Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba ugomvi wetu siyo chupa, ugomvi ni matumizi yanayotokana na ile mitungi ya gesi. Kwa maana tunafahamu kuna mahali katika bahari umbali kwa maana ya kina kilomita 40, mvuvi ni lazima awe na namna ya kuweza kumfikisha kule na kufanya shughuli yake, lakini kwa utafiti wetu hapo nyuma ilionekana wazi kwamba waliokuwa wakienda kufanya uzamiaji, ukiacha wale waliofanya uzamiaji kwa ajili ya *sport fishing* na utafiti, wengine wote walikuwa ni wale wanaoambatana na shughuli za uvuvi haramu na ndiyo maana Serikali ikasema kwa sababu hiyo basi tutazuia zoezi hili isipokuwa kwa kibali maalum cha wale wanaofanya utafiti na wale wanaofanya *sport fishing*.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa sasa Serikali tupo katika kuboresha sheria zetu na kuboresha kanuni zetu, tumekisikia kilio hiki cha wavuvi wazamiaji na sisi tunakifanya kazi, endapo sheria hizi zitapitishwa na kanuni hizi mpya tuna imani kwamba inawezekana katika jambo ambalo litakuwa limekwenda kuboreshwa mojawapo ni jambo hili. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nimekuona.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kuuliza swal moja la nyongeza. Kumekuwa na mkanganyiko mkubwa sana baina ya zana zipi zinaweza kutumika katika uvuvi na zipi hazifai. Mlongoni mwa maeneo ambayo mkanganyiko huo upo ni pamoja na katika Jimbo langu la Mtwara na mara nyingi tumekuwa tukimwomba Waziri au Naibu Waziri mwenyewe waje ili wakae na wavuvi wakubaliane kipi ni sahihi na kipi si sahihi lakini suala hilo limekuwa gumu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuniambia ni lini atakuja Mtwara ili kuongea na wavuvi wa Mtwara kwa sababu kwa zaidi ya miaka mitatu hawajawahi kumwona Waziri wala Naibu Waziri?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Abdallah Ulega miaka mitatu hamjafika Mtwara.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Ghasia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa kufuatilia kwa karibu sana hali za wavuvi wa Mtwara na naomba tu nimhakikishie kwamba Serikali iko makini sana katika kuwafuatilia wavuvi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimefika Mtwara, nimefanya m Kutano na wavuvi wa Mtwara katika Mji wa Mikindani katika Chuo tulichokijenga cha Wavuvi cha *FETA* ambako ni mji wa asili wa kwake ye ye mwenyewe Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nataka nimwambie kwamba nilikutana na wavuvi na nikazungumza nao mwaka jana na katika kesi walizonipatia moja ya kesi ni matumizi ya zana aina ya nyavu za *ring net*, mgogoro wao ni muda gani utumike mtando huu kwa maana ya mtego huu wa *ring net* na ugomvi wao ni kina cha kutumika kwa zana hii ya *ring net*.

Naomba nimhakikishie kuwa katika jambo lingine lilitotokea pale Mikindani ni choo ambacho wavuvi walikilalamikia cha pale sokoni ambacho tulitoa maelekezo kwa Halmashauri waweze kukirekebisha na taarifa tuliyonayo ni kwamba tayari wameshafanya marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hii dhana ya kutumia kutokana na kina wavuvi walio wengi wangependza sana kuona wanatumia zana hizi nje maji mepesi, maji mafupi ambapo kwa kufanya hivyo wanakwenda katika uharibifu wa mazingira ya bahari kwa sababu huku katika maji mafupi, ndiko samaki wanakozaliana na wanapokuja kuweka nyavu zile maana yake ni kwamba wanaharibu maeneo ya mazalia. Naomba nimhakikishie kwamba nitarudi tena Mtwara kwenda kuzungumza na wavuvi na kuweza kupata hatima ya shughuli zao.

SPIKA: Mheshimiwa Khatibu ulisimama mara kwa mara. swali la mwisho la nyongeza, tafadhali.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Wavuvi wengi walikuwa wanategemea uvuvi wa jongoo bahari kuendesha maisha yao na jongoo bahari ni dhahabu ya baharini. Jongoo bahari sasa hivi anafikia dola 30 kwa kilo moja, lakini Serikali imepiga marufuku uvuvi wa jongoo bahari, tunataka kujua kuna faida gani Serikali inapata kwa kupiga marufuku ya uvuvi wa jongoo bahari hali wananchi wanaathirika kwa kukosa mapato?

SPIKA: Hili swali jipya kabisa, lakini kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri ni mtaalam jaribu kuitia bwana kuna nini katika jongoo bahari?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatibu, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ni kweli miaka ya hapa karibuni, ilipiga marufuku uvuvi wa majongoo bahari. Majongoo bahari ni mionganoni mwa viumbwe viliviyokuwa vinatishiwa kutoweka, kwa hivyo kwa kulinda rasilimali hii Serikali ikapiga marufuku katika eneo lote la pwani ya Tanzania

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hapa karibuni kama anavyothibitisha Mheshimiwa Khatib na ni kweli, jongoo bahari ni mali na ni mali sana tumeliona jambo hilo na tumeionna fursa hiyo. Mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba wananchi walio wengi siyo tu kusubiri majongoo bahari yale ya asili kwa maana *wild animals*, sasa tunakwenda katika utaratibu wa kuwafuga pia kwa maana ya *mariculture*. Tunataka fursa hii ienee katika ukanda wote wa pwani tutafuga majongoo bahari, tutainua mwani, tutainua pia vile vile na mazao mengine ikiwemo kaa ambao wenzetu katika Mataifa mengine kama Uchina wanapenda na wanataka sana. Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge wale wa pwani wakae mkao wa utayari wa kupokea fursa hizi na

tuwahamasishé Watanzania wavuvi wa pwani wakae katika vikundi ambavyo vitatusaidia kuwapelekea fursa hii kwa urahisi zaidi

SPIKA: Ahsante sana. Tuendelee Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Kilimo, swali liliolizwa na Mheshimiwa Zainab Mussa Bakari, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 7

Maradhi Yanayoikumba Mimea ya Mipapai Nchini

MHE. ZAINABU MUSSA BAKARI aliuliza:-

Yamejitokeza maradhi katika mimea ya mipapai nchini ambayo yanahatarisha kupotea kwa mimea hiyo:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ya kuweza kudhibiti maradhi hayo?

(b) Je, kuna utafiti wowote uliofanywa juu ya maradhi hayo ili kugundua yanasantabishwa na nini?

(c) Kama bado; je, Serikali haioni kuna hatari ya kupoteza mimea amba ni muhimu sana?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imefanya utafiti na kugundua kuwa ugonjwa wa Ubwili unga ndio unaoathiri mipapai kwa kiwango kikubwa. Baada ya kugundulika ugonjwa huo, Wizara ya kilimo imechukua hatua za kuudhibiti kwa kutumia viuutilifu vyenye viambata vya *crorpynfos* (udhibiti wa kwenye udongo), *Profenophos* na

Dichlorovosch (udhibiti kwenye majani). Aidha, njia nyingine ya uthibiti ni kwa kutumia mbinu bora za kilimo (*Cultural Control*) kwa kupanda miche wakati wa kiangazi ili mimea isishambuliwe ikiwa michanga, kupalilia shamba kwa wakati na kung'olea miche iliyoathirika na utumiaji wa wadudu marafiki (*Biological Control*).

Vilevile Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kufuata kanuni bora za kilimo ili kuepuka magonjwa mbalimbali yanayoweza kuathiri mimea ikiwemo mipapai.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Utafiti cha *TARI-HortiTengeru* imeendelea kufanya utafiti magonjwa na wadudu wanaoathiri mazao ya bustani ikiwemo mipapai. Utafiti huo umegundua kuwa ugonjwa wa Ubwili unga unaoathiri mipapai unaosababishwa na vimelea vya kuvu (*fungus*) vijulikanavyo kitaalam kama *Oidium caricae papaya*.

(c) Mheshimiwa Spika, mipapai haiwezi kupotea nchini kwa kuwa tayari njia za kudhibiti magonjwa na wadudu wanaoshambulia mimea hiyo zipo. Aidha, Wizara itaendelea kuwaelimisha wakulima na wadau mbalimbali juu ya udhibiti wa ugonjwa na wadudu wanaoshambulia mimea na mazao ikiwemo mipapai ili kuongeza uzalishaji na tija ya mazao hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab.

MHE. ZAINABU MUSSA BAKARI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya majibu ya Serikali napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, baada ya kufanya utafiti na kugundua ugonjwa huo ni kwa kiasi gani Serikali imewafikia wakulima kuwapa elimu pamoja na kuwafahamisha dawa muhimu za mipapai hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kiasi kikubwa Watananzania wamejikita katika kilimo cha mapapai na vilevile inaonekana kwamba wakulima wakinunua mbegu za mipapai, mipapai mingi inakuwa haizai. Je Serikali ina

mkakati gani wa kuwapatia wakulima pembejeo na kuhakikisha mbegu wanazonunua zinaza ilii kukiimarisha kilimo hicho?

SPIKA: Swali hili muhimu sana Mheshimiwa Naibu Waziri, zao la mipapai karibu kwa majibu, limekuwa mtihani ama haikui, ama inadumaa, ukipanda 100, 80 madume, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zainabu Bakari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kujua Serikali tumewafikaje wakulima baada ya kugundua matatizo hayo ya magonjwa ya mapapai. La kwanza tumewafikia kwa ajili ya kwenda kuwapa elimu moja kupitia kituo chetu cha *TPR*/ambao ndiyo wadhibiti wa magonjwa haya mbalimbali kupitia viuutilifu. Kwa hiyo wao kwanza wanapita sehemu mbalimbali kukagua maduka yanayouza viuutilifu hivyo ili kubaini kama viuutilifu vile vinaubora na vinakidhi vigezo kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, pili, tunapitia, tunatoa elimu mbalimbali kupitia vyombo mbalimbali nya habari kama redio, *TV* na makongamano na warsha kuwafikia wakulima huko waliko ili kwamba kuwapa elimu kukabiliana na magonjwa hayo mbalimbali ikiwemo hii ya mipapai

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anataka kujua mikakati ya Serikali tuliyokuwa nayo kwa ajili ya kuwapatia mbegu bora za mipapai. Moja kama nilivyosema jibu la msingi kwamba kituo chetu cha utafiti cha *TARI* - Tengeru, ambacho kiko maalum kwa ajili ya kufanya utafiti wa mazao ya mbogamboga na mazao ya matunda hapa nchini, lengo ni kufanya utafiti wa kina kugundua mbegu bora ambazo zinaendana na hali yetu ya mazingira, lakini pia zenye ubora wa ukinzani wa magonjwa haya pamoja na hali ya mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hiyo, atupe nafasi tu kituo hiki

kinafanya utafiti huo na wako katika hatua za mwisho kuja na majibu ambayo sahihi kukabiliana na ugonjwa huo.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali langu la nyongeza. Kabla sijaauliza swali la nyongeza naomba nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwatakia heri wanafunzi wote wa Tanzania kwa kuanza mitihani yao ya kidato cha nne, tunawaombea Mwenyezi Mungu awasimamie, awabariki ili waweze kufanya vizuri mitihani yao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niulize swali langu la nyongeza, kutokana na swali la msingi namba saba, nami nataka niulize kwamba, kuna suala la sumu kuvu ambalo lipo ndani ya karanga na lipo vile vile ndani ya mahindi na ukizingatia mahindi ni chakula chetu kikubwa na ni chakula cha msingi kutokana na utafiti uliofanyika. Je, wamefikia hatua gani kuhakikisha kwamba mahindi haya hayana sumu kuvu au yamepungua kwa kiasi gani? Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, kwa swali zuri. Mheshimiwa Naibu, Waziri Omary Mgumba, majibu tafadhali, kuhusiana na ugonjwa huo wa mahindi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mama yetu Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kuna ugonjwa hatari unaosababishwa na huu wa sumu kuvu unaosababishwa na fangasi wakuvu ambao ugonjwa huu umeleta athari kubwa hasa katika mikoa hii ya Kanda ya Kati hususan kwenye kule Wilaya ya Kondo, Chemba na watu zaidi ya 19 walipoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali baada ya kugundua hiyo kwanza sasa hivi tumekuja na programu ambayo

imeanza tangu mwaka jana na tumetenga zaidi ya bilioni 35 kwa ajili moja kutoa elimu ya ugonjwa huu kwa umma, lakini pili kujenga miundombinu ya kuhifadhi mazao haya ambayo kama mahindi na karanga ili yasiweze kuathirika na sumu kuvu. Mikoa ambayo tumeilenga ni mikoa 10 na mikoa miwili ya Zanzibar na ikiwepo hii ya Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo moja kabisa ni kuwafikia wakulima kuwapa elimu sababu gani zinasababisha ugonjwa huu, madhara yake ni nini na kinga yake ni nini? Ili kuondokana na tatizo hili lililopo hapa nchini.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini. Mheshimiwa Mendrad, tafadhali.

Na. 9

Mradi wa Maji wa Mtwango

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Mradi wa maji katika Kata ya Mtwango bado haujakamilika:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huo ambao umechukua muda mrefu bila kukamilika?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo langu la Pangani pamoja na wananchi wa Mkoa wa Tanga kwa mafuriko ambayo yalikuwa yametokea, tumepoteza ndugu zetu lakini pia kuharibika kwa miundombinu. Tunamshukuru Mkuu wa Mkoa kwa hatua ya haraka ya kuweza kurejesha miundombinu ile.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mradi wa Maji wa Kata ya Mtwango umechukua muda mrefu kutokana na changamoto iliyokuwepo ya wakandarasi kutokamilisha kazi kwa wakati hali ambayo ililazimu kuwaondoa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga shilingi milioni 300 kwa lengo la kukamilisha mradi huo. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa matenki, ununuzi wa pampu na ununuzi wa mabomba ya kusambaza maji kwa wananchi. Kazi hizo zitafanywa na wataalam na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji yaani *RUWASA* katika ngazi ya wilaya na mkoa. Taratibu za kukamilisha kazi zilizobaki katika Kijiji cha Sawala zinaendelea. Mradi huo unategemewa kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

SPIKA: Mheshimiwa Kigola kama kuna swali la nyongeza!

MHE. MENDARD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huu mradi wa maji wa Sawala umechukua muda mrefu sana zaidi ya miaka 6 na Serikali mara ya kwanza ilitoa fedha zaidi ya milioni 200 lakini hakuna kitu ambacho kimefanyika. Mara ya pili imetoea milioni 230, hakuna kitu kilichofanyika na wananchi pale sasa wanakata tamaa. Swali langu, ni lini mradi huu utakamilika ili wananchi waanze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna wakandarasi wawili wameshatolewa, sasa hivi Serikali inatumia mbinu gani ili kuhakikisha kwamba ile kazi inafanyika kikamilifu? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili ya Mheshimiwa Kigola kutoka kule Mtwango, Mheshimiwa Naibu Waziri Aweso tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuweza kufuatilia miradi yake ya maji. Kikubwa utekelezaji wa miradi ya maji katika ubora unategemeana na upatikanaji mzuri wa wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, nilifika pale Mufindi Kusini eneo lile la Mtwango, moja ya changamoto kubwa mkandarasi ambaye amepewa kazi ile alikuwa wa kibabaishaji (kanjanja) kwa hiyo tulimuondoa mkandarasi yule lakini tumeiagiza TAKUKURU kuhakikisha fedha zile za wananchi walipakodi azitapike mkandarasi yule. Sisi kama wizara tumehukua jukumu sasa la kuwapatia ndugu zetu wa Wakala wa Maji Vijijini (*RUWASA*) kwa maana ya kufanya kazi ile kwa *force account* mradi ule ukamilike na wananchi wake waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji tunatumia *forced account* katika kuhakikisha mradi ule tunautekeleza kwa wakati na wananchi wako waweze kupata huduma hii muhimu. (*Makofi*)

Na. 10

Mradi wa Maji Kutoka Kilimanjaro Hadi Arusha Mjini

MHE. JAMES K. MILLYA aliuliza:-

Kuna mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Mkao wa Kilimanjaro kuelekea Arusha Mjini, mradi huu unapitia kwenye mipaka ya Wilaya ya Simanjiro Kata za Naisinyai na Mererani.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wananchi wa Kata hizo wanapatiwa huduma hiyo inayopita kwenye maeneo yao;

(b) Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua ujenzi wa barabara ya kilometra 14 toka K/A hadi Mererani aliwaahidi Wananchi wa Mererani na Naisinyai kwamba atawakumbuka kwenye kuondoa adha ya maji; Je, Serikali imejipangaje kutimiza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu ya swali hilo la Mheshimiwa James Millya.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Kinyasi Millya Mbunge wa Simanjiro lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru. Mradi huu pia utatoa huduma ya maji katika maeneo ambayo bomba kuu la maji kuelekea Arusha litapita. Kata za Mererani na Naisinyai ni miongoni mwa kata hizo na vijiji vitakavyopata huduma ya maji ni Naepo, Oloshonyoke na Kibaoni ambavyo viko katika Kata ya Naisinyai na vijiji vya Songambele, Getini na Kangaroo ambavyo viko katika Kata ya Mererani.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kuondoa adha ya maji katika maeneo hayo, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru utahusisha kuboresha huduma ya maji katika kata za Mererani na Naisinyai. Mradi huu mkubwa wa maji kutoka Kilimanjaro kwenda Jiji la Arusha unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2020. Mradi utakapokamilika, adha ya maji katika maeneo hayo itakuwa ni historia.

SPIKA: Mheshimiwa Millya umeridhika?

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Maeneo niliyosema ya Naisinyai na Mererani ni maeneo ambayo tunapata madini

ya tanzanite, ni aibu sana kama pamoja na rasilimali hiyo kubwa maeneo yale hayana maji. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anihakikishie kwamba bomba lile litakapopita Vijiji vya Lengasti, Mihiye, Oloshonyoke kama ambayo umesema yatapata maji.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna bomba la maji kutoka Ruvu kwenda Olekosmet la takribani bilioni 41, niishukuru Serikali ya Dkt. John Pombe Magufulsi kwa kuleta mradi huu. Je, yupo tayari kuongozana na mimi kukagua mradi huu ili ifikapo Mei mwakani kama ambavyo Serikali imeahidi mara zote mradi huu uweze kukamilika na wananchi wapate maji safi na salama kwa ajili ya mifugo na watu wa Simanjiro?. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya, kiukweli ni mionganini mwa Wabunge ambao wanafanya kazi kubwa sana na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge anatosha mpaka chenji inabaki.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho ninataka kukisema, tunatambua maji ni uhai na sisi kama Wizara ya Maji eneo lile la Mererani tulishachimba kisima kikubwa lakini changamoto ambayo tuliona ni kuwepo kwa *fluoride* kwa kiwango kikubwa sana. Sasa tunatekeleza mradi zaidi ya bilioni 520 katika Jiji la Arusha na baadhi ya vyanzo hivi vya maji viro katika Jimbo lake. Ninachotaka kumhakikishia bomba kuu lile litakapopita katika maeneo yale ya Mererani na Naisanyi yote yatapatiwa huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda katika Jimbo lake la Simanjiro katika ule mradi wa Olekosmet, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge nipo tayari kuongozana nae katika kuhakikisha tunafika katika mradi ule. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Flatei nilikuona swali fupi sana la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Hali ya ukosefu wa maji iliyopo Simanjiro inafanana kabisa na Mbulu Vijijini, Mheshimiwa Naibu Waziri umefika Mbulu Vijijini. Je, miradi hii ya maji na kisima cha Hyadom ulichotoa ahadi nini unatimiza, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi lini unatimiza.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninachotaka kumhakikisha Mbunge maji hayana mbadala na nilikwishafika katika Jimbo lake na kuna fedha ambayo tuliiikuta, nawaagiza sasa *DDCA* wafike haraka katika kuhakikisha wanakichimba kisima kile ili wananchi wake waweze kupata huduma ya maji ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, tunaelekea Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linauliza na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe.

Na. 11

**Hitaji la Vyuo vya Uhifadhi wa Wanyamapor
Kanda ya Ziwa**

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Mikoa ya Kanda ya Ziwa imeathirika na mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu mkubwa wa mazingira:-

Je, ni lini Serikali itajenga vyuo vya uhifadhi wa wanyamapor na uhifadhi wa mazingira na elimu ya utalii hasa baada ya kuanzishwa kwa hifadhi za Taifa Burigi- Chato, Kigosi, Ibanda – Rumanyika, Rubondo na Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Agustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina vyuo vinavyotoa mafunzo katika fani za uhifadhi wa wanyamapori, utalii na misitu ambapo uhifadhi wa mazingira ni sehemu ya mafunzo hayo. Mafunzo hutolewa katika ngazi za astashahada, stashahada, shahada na elimu nyingine za juu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Chuo cha Pasiansi kilichopo Kanda ya Ziwa katika Mkoa wa Mwanza kinatoa Astashahada ya awali ya uhifadhi wa wanyamapori na himasheria, na Stashahada ya uhifadhi wa wanyamapori na himasheria, Chuo cha Wanyamapori - MWEKA kilichopo Kilimanjaro, kinatoa Astashahada na Shahada ya uhifadhi wa wanyamapori na utalii. Chuo cha mafunzo ya Uhifadhi wa maliasili kwa jamii - Likuyu Sekamaganga kilichopo Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Namtumbo kinatoa mafunzo kuhusu mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa askari wanyamapori wa vijiji (*VGS*), viongozi na wajumbe wa Kamati za Maliasili za vijiji.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Misitu Olmotonyi kinatoa mafunzo yanayohusu misitu katika ngazi za astashahada na stashahada pamoja na mafunzo ya ufgaji nyuki katika chuo cha Ufgaji Nyuki – Tabora. Vilevile, Wizara kupitia Chuo cha Viwanda vya Misitu kilichopo Moshi hutoa mafunzo ya teknolojia ya viwanda vya misitu katika ngazi ya astashahada ya awali, astashahada na stashahada.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Utalii inatoa mafunzo ya utalii, ukarimu na uongozaji watalii katika ngazi za Astashahada na Stashahada.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kuimarisha vyuo vilivyopo na haina mpango wa kujenga chuo kipya ili kukidhi mahitaji ya nchi nzima.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe maswali ya nyongeza.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa ni mkubwa sana katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na Mkoa wa Geita kwa maana ya kwamba hifadhi za misitu zinatoweka kwa haraka sana kwa mfano Hifadhi ya Msitu ya Geita, Rwanagasa, Rwande na Miyenze inatoweka kwa haraka. Sasa je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuweza kudhibiti hali ya uharibifu wa mazingira na utowekaji wa misitu unaofanyika kwa sasa katika mkoa huo wa Geita.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe haina maafisa wanyamapori, je, Serikali ipo tayari sasa kutupatia maafisa wanyamapori ili huduma yao iweze kuonekana kwa wananchi wa Wilaya ya Mbogwe, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akiwasiliana na mimi kuhusu uharibifu wa misitu aliyoitaja; Misitu ya Rwanagasa na Rwande ambayo kwa ujumla imevamiwa sana na wachimbaji wadogowadogo na wakataji wa kuni na mkaa lakini tumeshirikiana nae kutoa maelekezo ili kuilinda. Kwa hiyo, naomba nimpongeze sana kwa juhudhi hizo ambazo ameendelea kuzionesha.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa misitu ambao unaendelea karibu nchi nzima ni tatizo ambalo ningependa kulitolea maelekezo. Imekuwepo tabia ya Halmashauri nyingi kufikiri jukumu la kulinda misitu ni la *TFS* au Wizara lakini misitu

hii mingi ipo kwenye maeneo ya Halmashauri na mingi ni misitu ya vijiji na Halmashauri na misitu michache inayosimamiwa na *TFS*inalinda vizuri. Kwa hiyo, nizielekeze tu Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinashirikiana vizuri na maafisa wetu wa *TFS* kulinda na kudhibiti wanaoharibu misitu hii kwa kasi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika swal lake la pili la nyongeza amesema Halmashauri ya Mbogwe haina afisa wa wanyamapor. Na naomba tu nitumie nafasi hii pia kuwaambia Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe kwamba katika maombi yao ya watumishi tunawaelekeza Halmashauri zote ambazo zinapakana na hifadhi ambazo zimekuwa na historia ya migogoro ya wanyama na binadamu kuhakikisha kwamba wanaomba kuwa na maafisa wa wanyamapor. Katika halmashauri hizo kwa sababu hawa ni watu wa kwanza ku-*respond*na matukio ya wanyama waharibifu wanaoenda kwenye maeneo ya makazi ya watu.

Kwa hiyo, naelekeza halmashauri hiyo katika maombi yao ya watumishi ya mwaka huu waweze kuomba afisa wa wanyamapor.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Constatine John Kanyasu. Swal i la Mheshimiwa Kiteto Koshuma sasa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 12

Kutangaza Mkoa wa Mwanza Kwa Utalii

MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. KITETO Z. KOSHUMA) aliuliza:-

Bodi ya Utalii pamoja na mambo mengine ina jukumu la kutunza utalii wa ndani ya nchi:-

Je, Serikali inasimamiaje Bodi hiyo ili kuhakikisha Mkoa wa Mwanza unatangazwa kama Mji wa Kitalii?

SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constatine John Kanyasu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimisha Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa vivutio vya utalii vilivyopo Mkoani Mwanza vinatangazwa ipasavyo, Wizara inayo ofisi ya kanda ya Idara ya Utalii Jijini Mwanza na mwaka 2011 ilielekeza Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*) kufungua Ofisi ya Kanda jijini Mwanza. Aidha, Wizara imeelekeza Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - *TANAPA* kufungua Ofisi ya kanda ya kaskazini magharibi Mkoani Mwanza. Lengo likiwa si tu kusogeza karibu huduma kwa wadau wa sekta ya utalii lakini pia kuhakikisha vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii Mkoani Mwanza na maeneo yote ya kanda ya Ziwa zinatangazwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Wizara yangu kwa kushirikiana na Sekta binafsi imekuwa ikishiriki na kuratibu matukio na matamasha yanayolenga kutangaza vivutio vya Mkoani Mwanza ikiwemo; Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani, Tamasha la Bulabo *na Afro Calabash*, Tamasha la Urithi (*Urithi Festival*), *Rocky City Marathon* na Mashindano ya Urembo. Lengo ni kuvutia wageni na watalii wa ndani na nje kutembelea mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwa Mkao wa Mwanza ni mionganii mwa maeneo machache yenye rasilimali nyingi za utalii ikiwemo fukwe nzuri za Ziwa Viktoria, visiwa vinavyovutia, Hifadhi ya Taifa ya Saanane, wanyamapori, utamaduni, miamba ya mawe yenye kuvutia na mandhari nzuri ya jiji. Vivutio hivi kwa miaka ya karibuni vimekuwa vivutio wageni wengi kutembelea mkao huo.

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa Wizara inaendesa zoezi la kubainisha vivutio vya utalii kwa dhumuni la kuviendeleza na kuvitangaza. Katika mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara imelenga kutekeleza zoezi hilo katika Mikoa sita ikiwemo Mkoa wa Mwanza. Kazi hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii Tanzania (*TTB*), uongozi wa mkoa, Wilaya, Vijiji na wadau wa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, aidha, tarehe 16 na 17 Machi, 2019 Wizara ilifanya kikao na wadau wa utalii kanda ya ziwa na magharibi ikiwa ni jitihada za kuimarissha utalii Mkoani Mwanza na Kanda ya ziwa kwa ujumla. Katika kikao hicho kilichofanyika Mkoani Mwanza kilihuisha viongozi kutoka Mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Kagera, Shinyanga na Kigoma. Vilevile Wizara inaendelea na jitihada zingine za kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za utalii na vijana kujifunza uongozaji watalii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya utalii ni mtambuka, hivyo kazi ya utangazaji na uendelezaji sekta hii inahitaji juhudzi za pamoja za wadau wa sekta ya umma na binafsi. Nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge na Uongozi wa Mkoa wa Mwanza kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Wizara yangu katika jitihada za kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii vya Mkoa wa Mwanza.

SPIKA: Nimekuona umesimama Mheshimiwa Mabula, swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa kuonesha wazi kwamba kama Wizara wanatambua namna ambavyo Mji wa Mwanza una vivutio vingi na unaweza kuwa sehemu ya utalii kwenye nchi hii. Sasa nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa spika, moja ni kwamba pamoja na mazingira na vivutio vingi vilivyopo ni nini sasa mkakati wa Wizara kuhakikisha kwamba ili watalii waje ni lazima

wapatikane watu wanaosababisha watalii kuja. Tunatambua ili watalii hawa waje wanatakiwa wawe na watu wenye weledi ambao vijana wamefundishwa kwa kuona maeneo ambayo tunaweza kuwa na *ma-tour guide* wazuri ni nini mkakati wa Wizara kuhakikisha vijana wengi walipo Mwanza wanapatiwa mafunzo haya na kufanya kazi hii vizuri.

Mheshimiwa spika, la pili; tunatambua kwamba *TTB* tayari kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza pamoja na *St. Augustine University* wameanzisha *Mwanza Tourism* na kupitia mkakati huo tayari Wizara kwa maana ya halmashauri pamoja na Ubalozi wa Ujerumani wameanza ukarabati wa ile *Gunzezi House* ambayo iko pale Makoroboi itakayokuwa ni moja ya majumba ya maonesho ya historia pamoja na ile *Gallostream* Nini mkakati wa Wizara kuhakikisha maeneo haya yanapewa kipaumbele na kuwa moja ya vivutio katika Mji wa Mwanza, nakushukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu majibu ya maswali hayo, nyumba za Wajerumani zinakuwa kivutio, za Wasukuma vipi zeneyewe sio kivutio? Majibu tafadhali Mheshimiwa Kanyasu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mabula kwa namna ambavyo tumekuwa tukishiriki kwa pamoja katika juhudii hizi za kuifanya Mwanza kuwa *hub* ya utalii wa Mikoa ya Kaskazini Magharibi. Tulikuwa nae kwenye kongamano hilo ambalo nimelisema na alishiriki kwenye kuchangia mambo mazuri sana ambayo Wizara inayafanya kazi, kwa hiyo nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ameuliza ni mkakati upi wa Wizara katika kuhakikisha kwamba tunapata washiriki wengi katika shughuli za utalii katika mikoa hiyo. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Wizara katika nyakati mbalimbali imefanya mikutano na wadau katika Mkoa wa Mwanza na tumeendelea kufanya semina mbalimbali kupitia ofisi yetu ya idara ya utalii lakini pia kupitia *TTB* na hivi karibuni tutafanya

mkutano mwingine kutathmini kikao tulichokifanya pale awali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wito wangu tu ni kwamba naomba kuwakaribisha wadau wote wa utalii wa Mkoa wa Mwanza na watu walio na interest ya kufanya biashara ya utalii kama alivyosema mwenyewe, watalii wanaletwa na watu na watalii wanatafutwa lazima wawepo wapo Mkoani Mwanza wanaotafuta watalii. Sisi tutakuwa tayari kufadhili mafunzo hayo ili kuhakikisha kwamba tunapata watu wengi wanaoshirikiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, swalilake la pili amezungumzia kuhusu ukarabati wa jengo liliopo Makoroboi na kwamba ni upi mkakati wa Wizara. Wizara yetu imeendelea kutoa utaalam katika maeneo haya na katika maeneo mengine kwa mfano pale Mkoani Iringa lilikuwepo pia jengo la mkoloni ambalo zamani ilikuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya lilikarabatiwa na kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *RUCO*sasa hivi jengo hilo ndilo ambalo linaonesha makumbusho na historia mbalimbali ya Mkoa ywa Iringa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino kwa kuandaa kila mwaka *Mwanza Tourism* ambapo wamekuwa wakipeleka watu mbalimbali katika Kisiwa cha Saa Nane na kuwazungusha katika Jiji la Mwanza. Juhudi hizi tunaziunga mkono tutaendelea kushirikiana na Mkoa wa Mwanza.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa majibu ya nyongeza tafadhalii.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa, lakini kwa kuwa *circuit* ya Kaskazini Magharibi ni *circuit* ya Kimkakati kwenye Serikali ya Awamu ya Tano hususan kwenye Sekta ya Kiutalii, napenda niongeze mambo yafuatayo ambayo tunayafanya na tunakusudia kuyafanya katika *circuit* hii ya Kaskazini Magharibi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, Serikali inawekeza kwa kiasi kikubwa sana kwenye miundombini (*hard infrastructure*) kama vile Reli ya SGR ambayo itafika mpaka Mwanza, viwanja vya ndege; Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kitakuwa cha Kimataifa na sasa hivi ujenzi unaendelea pale. Vile vile ukiunganisha na mtandao wa Viwanja vya Ndege vilivyopo katika *circuit* hii, Kiwanja cha Ndege cha Chato, Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, Kigoma, Tabora pamoja na cha Musoma vyote vinafanyiwa *first lifting* ili kuhakikisha kuna ndege zinatua *regularly* katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni sambamba na mtandao wa lami. Pia tunawekeza katika *softly infrastructures* ambapo sasa hivi tumewaelekeza Chuo cha Taifa cha Utalii wafungue Tawi kwa ajili ya kuongeza idadi ya vijana ambao wanaseomea mambo ya utalii, *tour guiding*, upishi na vitu vingine katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo yote, *circuit* hii ya Magharibi ina bahati ya kuwa na maziwa na mito na tumeona kwamba hii ni *unique feature* ambayo kama tukiitumia vizuri itaifungua kwa kasi sana *circuit* ya Kaskazini Magharibi ambapo kwa kuanzia, tumewaelekeza TANAPA na tayari wameshafanya manunuzi ya boti ambayo itakuwa ni *luxury* kwa ajili ya utalii, itakuwa inachukua watu 50 na itakuwa inazunguka kutoka *spix gulf* kwenye eneo la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, inakwenda, ina-dock Mwanza, itakuwa ina-dock pale Kisiwa cha Saa Nane, Kisiwa cha Rubondo lakini pia kwenye eneo la Katete ambapo Hifadhi ya Taifa ya Burigi Chato inaanzia. Hii boti itakuwa ni *luxury* na itakuwa inatumia masaa takribani matatu na nusu mpaka manne kutoka Serengeti kufanya huo mzunguko wote.

Mheshimiwa Spika, tunakusudia boti hiyo itakuwa ni ya *business class* lakini tumewaelekeza pia TANAPA wawekeze kwenye manunuzi ya boti nyingine ambayo itakuwa *economy class* ambayo itachukua watu 300 kwa ajili ya kuwazungusha kwenye Ziwa Victoria ili kuvinjari katika Ziwa, lakini pia Visiwa vilivyoko pale na maeneo ya Hifadhi

ambayo yanaungana moja kwa moja na Ziwa Victoria.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipenda kuongezea hayo.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Muda hauko upande wetu. Eh! Haya mambo haya, boti inaanzia Busega, *luxury boat, business class*, kweli Wasukuma watapanda hiyo boti kweli! (*Kicheko*)

Swali la mwisho kwa siku ya leo linatoka kwa Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, Mheshimiwa Neema kwa niaba yake tafadhali mwulizie swali.

Na. 13

**Hitaji la Nyumba za Askari na Gari za
Doria – Makambako**

MHE. NEEMA W. MGAYA (K.n.y. MHE. DEO K. SANGA)
aliuliza:-

Askari wa Kituo cha Polisi katika Mji wa Makambako hawana gari la doria wala nyumba za kuishi:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za kuishi Askari hao?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa gari la doria kwa Kituo cha Polisi Makambako?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Masauni, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo

Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Makambako ina askari wapatao 111 na kuna jumla ya nyumba 12 tu katika Mji wa Makambako. Nyumba hizo ni takribani asilimia 11 ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi na askari katika mji huo. Hata hivyo, katika jitihada za kutatua changamoto hiyo, mwezi Oktoba, 2018 Serikali imeanzisha ujenzi wa nyumba 20 katika Mji wa Makambako ambapo nyumba hizi kwa sasa zimeshakamilika na askari wameshahamia.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Makambako kwa sasa ina magari matatu; magari mawili ya zamani ambapo moja ni PT. 0766 *Landrover* inayohitaji matengezo makubwa ili liweze kufanya kazi; na nyingine ni aina ya PT.1912 *Toyota Land Cruiser* ambayo ndiyo inatumika ingawa inafanyiwa matengenezo ya hapa na pale. Gari hili ndiyo inalotumika kwenye doria na operesheni mbalimbali pamoja na kupeleka askari kwenye matukio makubwa yanayotokea sehemu za mbali. Doria katika Mji wa Makambako hufanyika kwa kutumia gari, miguu pamoja pikipiki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwezi Septemba mwaka 2018 Wilaya ya Makambako imepata mgao wa gari jipya moja aina ya *Ashok Leyland* kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Jeshi la Polisi katika wilaya hiyo. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Neema, swali la nyongeza tafadhalli.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza swali la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa walizozifanya katika Jimbo la Makambako, lakini vilevile eneo la Polisi la Makambako liliipimwa na kufanyiwa uthamini kwa ajili ya kulipa fidia wananchi ambao walikuwepo ndani ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, lini Serikali itawalipa wananchi hawa pesa zao kama fidia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wilaya ya Wanging'ombe tuna changamoto ya Kituo cha Polisi; nichukue nafasi hii kulipongeza Kanisa Katoliki kwa kuona umuhimu wa usalama wa raia na kujitolea baadhi ya majengo kutumika kama Kituo cha Polisi ndani ya Wilaya yetu ya Wanging'ombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe imeshatoa kiwanja, nilitaka kujua: Je, lini Serikali itajenga Kituo hiki cha Polisi ndani ya Wilaya yetu ya Wanging'ombe?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo *double double* kwa kifupi tafadhali Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Masauni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusiana na fidia ya wananchi, nataka nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeamua kuwaachia hilo eneo wananchi, kwa hiyo, suala la fidia halipo tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Kituo cha Polisi, niwapongeze Kanisa kwa kuanzisha hizo jitihada pamoja na wananchi wa eneo hilo; na niwahakikishie kwamba pale ambapo hali itaruhusu tutaongezea nguvu jitihada hizo ili Kituo hicho kiweze kukamilika. Tunatambua umuhimu wa Kituo hicho.

SPIKA: Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawaona lakini muda wetu mtaona hauko upande wetu lazima tuka-*catch up*, kwa hiyo, tuwiane radhi. Limebaki swali Na.14 la Mheshimiwa Malembeka, litapangwa kesho na limebaki kwa sababu tulikuwa na mambo mengi pale mwanzoni.

Matangazo kuhusu wageni walioko Bungeni asubuhi hii; tunaye mgeni ambaye ni Mshauri Mwelekezi kutoka Makao Makuu ya CPA London, Uingereza Ndugu Anthony Staddon. Ndugu Staddon amekuja kuendesha zoezi la tathmini ya Bunge Kidemokrasia. Mr. Stardon *please can you stand up where you are!* Ni huyo mgeni wetu kutoka Ofisi yetu ya Jumuiya ya Madola kule London Makao Makuu ya CPA, yuko kwa ajili ya kupitapita na kupata taarifa zitakazosaidia ku-*benchmark* Bunge letu na Mabunge mengine kuhusu Demokrasia ya Kibunge. Karibu sana Staddon. (*Makof!*)

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Mpango, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Dotto James, yuko nasi? Karibu kama upo; Naibu Katibu Mkuu Sera, Adolf Ndunguru, karibu sana; Naibu Katibu Mkuu Utawala, Ndugu Mary Maganga, karibu; Mtakwimu Mkuu wa Serikali Ndugu Albino Chuwa, karibu sana, nimekuona pale; Mhasibu Mkuu wa Serikali, Francis Mwakapalila, simwoni; Msajili wa Hazina, Ndugu Athuman Mbutuka, ahsante; Kaimu Kamishna wa Sera, William Mhoja, ahsante sana Mhoja; Kaimu Kamishna wa Bajeti Ndugu Constantine Mashoko, karibu sana Mashoko. (*Makof!*)

Wengine ni Kamishna Msaidizi wa Bajeti, Ndugu Emmanuel Tutuba, karibu Emmanuel; tunaye pia Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Fedha ya Ubia ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (CPPP) Ndugu Dkt. John Mboya, karibu Mboya; Mchumi Mkuu, Dkt. Lorah Madete, hongera sana Lorah, huyu Lorah ndio Mchumi Mkuu kule Wizara ya Fedha. Hongera sana. (*Makof!*)

Wameongozana na Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi, wengine kutoka katika Taasisi za Wizara ya Fedha na Mipango.

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, ni Wageni 30 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Walewavi, ambaao ni Umoja wa Madereva Pikipiki ya Magurudumu

mawili na matatu (UMAPIDO) wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Kenneth Chimoti. Wale Madereva, eeh, wale pale. Karibuni sana, karibuni sana. Hawa wanaendelesha Bajaji na Bodaboda na kadhalika na kadhalika. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ana Mgeni kutoka Jijini Dar es Salaam, mwanafunzi, Dkt. Salim Rashid Msuya, karibu sana, yule pale. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa John Kadutu ambaao ni familia yake kutoka Tabora Mkoani kule kule Tabora unyamwezini. Familia ya Kadutu, wale pale karibuni sana na tunawapongeza sana kwa kumuuguza Mheshimiwa mpaka sasa ana nafuu kubwa sana. Ahsanteni sana na mbarikiwe sana. (*Makofi*)

Wageni 58 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambaao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya. Wanamaombi, karibuni sana, basi mtuombee sana. Tunahitaji sana maombi yenu. (*Makofi*)

Wageni 50 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambaao ni Kwaya ya Tumaini Msalato hapa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Golden Lesilwa. Ooh, hongereni sana Tumaini Msalato. Waheshimiwa Wabunge, hii Kwaya ni moja ya *top* kabisa katika nchi hii. Kwa hiyo, eeh, kabisa kabisa! Kama mmeshasikia mambo yao, wako juu. Hongereni sana. Wanafanya mambo makubwa sana Kwaya hii. Siyo kama Yanga wanaenda huko wanafanya vitu vya ajabu ajabu eeh, wanafungwa magoli matano, inakuwaje hii? Sasa wamerudi kwenye ligi tuwasikie na Ndanda huko kama hawakugaragazwa tena. (*Kicheko/Makofi*)

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni wapiga kura wake kutoka Mbulu Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Bibi Maendeleo, Ndugu Sioni Msuya. Karibuni sana Wageni kutoka Mbulu, karibuni sana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni Wafanyakazi Bora wa *TAZAMA Pipeline* kutoka Mkoa wa Iringa na Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Iddi Nkanabo. Eeh, karibuni sana Wafanyakazi Bora wa *TAZAMA Pipeline*, karibuni sana. (*Makofii*)

Wapo wageni kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 113 na walimu sita kutoka Shule ya *St. Peter Clever High School Dodoma* hapa hapa. St. Peter Clever! Ooh, hongereni sana sana sana na karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge, mnapokuja kwenye Jiji la Dodoma, mkikaribia Mjini baada ya Mtumba upande wa kushoto kuna majengo makubwa makubwa hivi, ndiyo *St. Peter Cleverwanapotoka vijana wetu hawa na mnaona jinsi wanavyopendeza.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Ngeleja anawatangazieni Waheshimiwa Wabunge matokeo ya Mchezo wa mpira wa miguu uliochezwa siku ya Jumamosi kwenye Uwanja wa Kilimani, *Bunge Sports Club* walishinda kwa bao mbili, Dodoma Veteran bao moja. Upande wa Bunge ni Mheshimiwa Ally King na Mheshimiwa Alex Gashaza. (*Makofii*)

Tunaendelea kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wanamichezo, mwendelee kujitokeza kwa wingi, nami nachukua mahudhurio, wale watoro wasahau kwenda Uganda. Maana kuna wengine wanajitokeza dakika za mwisho mwisho ili kuchupia boti. Hiyo haiwezekani. (*Makofii*)

Zoezi la upimaji na ushauri wa afya linaendelea na linaratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Waheshimiwa Wabunge iko huduma pale kwenye Kituo chetu cha Afya cha Bunge ambapo kuna upimaji wa magonjwa ya njia ya mkojo, upimaji wa magonjwa ya ngozi, uchunguzi wa maumivu ya mgongo na chanjo ya mwisho ya Homa ya Ini, basi wale wote ambao mngependa kushiriki katika zoezi hili tunaomba mfile pale, wako Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* na Taasisi ya Mifupa *MOI*. Karibuni sana Kituo

cha Afya endapo unajihisi kupimwa au una changamoto fulani inayokupata.

Idara ya Utawala na Rasilimali watu inatuomba Waheshimiwa Wabunge kututaarifu kwamba wale Wabunge ambaao ni Mabalozi wa Usalama Barabarani wanataarifiwa kuwa TAWLA wameandaa Semina ya Kuwajengea Uwezo Juu ya Athari za Kiafya na Kiuchumi Zinazosababishwa na Ajali za Barabarani. Semina hiyo itafanyika Nashera Hotel Dodoma kuanzaia saa 7.30 mchana mpaka saa 10.30 jioni ya leo tarehe 5 Novemba. Orodha ya Waheshimiwa ipo kwenye Lango A kwa Wabunge wahusika na masuala ya Usalama Barabarani. Wanaomba usiyehusika usiende, maana yake siku hizi ikiitwa semina kila mtu anahudhuria. Kwa hiyo, majina yako lango A kule. (*Kicheko*)

Tangazo la mwisho ni kwa Waheshimiwa Wabunge waliopokea barua kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwamba wataalam kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma watakuwepo hapa Bungeni katika kipindi cha Mkutano huu wa Bunge kwa ajili ya mazungumzo kuhusiana na fomu za maadili walizozijaza.

Napenda kuwajulisha kuwa Maafisa hawa wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma wataanza kazi hii leo tarehe 5 mpaka mwisho wa zoezi hili. Wale wote ambaao mmepeata barua zile, basi wanaomba mkutane nao. Mazungumzo haya ni ya kawaida tu, wala msiwe na wasiwasi.

Pia niwataarifu kwamba kwa sababu tunakaribia mwisho wa mwaka, zile fomu ambazo huwa tunajaza ambazo ni za Tume ya Sekretarieti ya Maadili ya Umma kuhusiana na madeni na mambo mengine, zile fomu muhimu kabisa safari hii hazitatolewa *hard copy*, ziko katika mtandao wa *Secretariat*.

Kwa hiyo, kila Mbunge ata-*download* kwa wakati wake na kuzijaza, ukishazijaza waweza kuzipeleka Maadili moja kwa moja, lakini utaratibu mzuri zaidi ni kuleta Ofisi ya

Spika nakala mbili, halafu Ofisi ya Spika inazipeleka kule. Utakavyoona, *is just okay* lakini hakikisha na Spika anapata nakala.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuendelee.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, hoja ya kuahirisha mjadala wa Bunge. Huku *CUF*.

SPIKA: Mheshimiwa Sakaya umesimama pia au! Kwa hiyo, mko wawili eeh, haya hao wawili. Mheshimiwa nakuruhusu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naitwa Maftaha Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Spika, natoa hoja na nasimama kwa Kanuni ya 69(1) kuomba Bunge lako tukufu liahirishe mjadala unaondelea uahirishwe mpaka wakati mwingine kwa sababu ya jambo la dharura ambalo linaendelea hivi sasa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, leo hivi, tupo katika mchakato wa uteuzi wa wagombea wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na hivi ninavyozungumza kuna hali ambayo inatokea kwa makusudi kabisa nchi nzima Wagombea wa Upinzani takribani maeneo mengi ya nchi wameenguliwa bila kufuata utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, Wilaya ya Liwale Mkoa wa Lindi wagombea wote wa Chama cha Wananchi *CUF* hawajapewa fomu na Wasimamizi wa Uchaguzi na hivi ninavyozungumza Wilaya ya Ubungo, Maswa, maeneo yote ya Kanda ya Ziwa Wagombea wa Upinzani hawajapewa fomu lakini wale walipewa fomu

wamenyimwa kurejesha zile fomu kwa Maafisa wa Usimamizi wa Uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi sasa, maeneo yote ya Tanzania Wagombea wa Upinzani wote wanaenguliwa kwa makusudi kabisa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Nachuma, unapaswa kuongea...

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, kwa sababu...

SPIKA: Mheshimiwa Nachuma, ngoja, nikukumbushe, unajua tumerudi Bungeni sasa, tumetoka huko tulikotoka, hapa pana taratibu zake, unaposema maeneo yote nchi nzima na wewe hujawa huko, huwezi kujikuta unalidanganya Bunge? Wewe umekuwa kote huko unakokutaja?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (*CUF*), nazungumza haya kwa ushahidi kabisa kwamba tunaletewa taarifa usiku na mchana na wagombea wetu wa Chama cha Wananchi (*CUF*)...

SPIKA: Naomba ushahidi huo unipatie, tuwekee hapo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ushahidi tunao.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ushahidi tunao.

SPIKA: Ndiyo nasema tunauomba.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, sawa, tutauleta.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, tutauleta ushahidi huo kwamba wagombea wameenguliwa, nilikuwa naomba tuahirishe mjadala unaoendelea hivi sasa, tujadili suala la dharura kwa sababu ni hatari kwa taifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae, jambo lake ni jema tu.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Ni hoja nzuri tu kwa maana hiyo, lakini kama alivyosema mwenyewe kwa kweli ana ushahidi lakini ushahidi hakuna.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Hajanipa, anipatie tu ushahidi, sasa inapokuwa hakuna hata ushahidi na unasema unao, Bunge kama Bunge ni vigumu kuendelea na jambo hilo. Kwa hiyo, ni vigumu *ku rule* kukuunga mkono katika jambo hili kwa sababu bado hujanipatia kitu ambacho unasema unacho tayari. Kwa hiyo, utakapokuwa tayari utatupatia, nitaangalia na kupima kama kuna haja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa ushahidi huo utakaonipatia ili tuweze kufanya mjadala.

Mheshimiwa Sakaya, ulisema mwongozo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa Kanuni ya 69(1) kwa suala la alilozungumzia Mheshimiwa Maftaha, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni la Kitaifa na ni hatua ya kwanza kabisa ya maendeleo ya taifa hili. Kinachofanyika ni kuua kabisa kabisa demokrasia ndani ya nchii hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge kama taasisi tusichukulie *simple* kiasi hicho, kwa kweli, tunaomba tulipe uzito wa kutosha. Leo watu wamenyimwa fomu, waliorejesha fomu vituo vimefungwa kuanzia jana na juzi lakini wale wachache ambao wamerejesha, wameenguliwa wote na hakuna sababu yoyote ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge kama wawakilishi, tulipe suala hilo uzito wa kutosha. Vinginevyo, haya yaishie humu ndani ya Bunge yaktoka nje ni hatari kwa amani na hata usalama wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Sakaya, nilikuruhusu unajua wewe ni Kamishna, sasa niliona nikuruhusu tu lakini nilikwisha *rule out* tayari kwa Mheshimiwa Maftaha na ulikuwa unarudia yaleyale kwamba ule ushahidi ambao mnao hebu tupatieni, halafu tutaona nini cha kufanya. Kama Bunge tukiruhusu tu mtu akisema kitu basi tunaahirisha mambo, itakuwa pia hatutendi inavyopaswa kuwa. Muda bado tunao, tupatieni huo ushahidi halafu tutaona nini cha kuishauri Serikali.

Kwa hiyo, nashindwa hata kumnyanyua Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa sababu sasa atajibu nini maana ushahidi hakuna.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Mngekuwa na ushahidi ningempa aangalie ushahidi halafu ajibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Kwa hiyo, mjiandae mlete ushahidi. Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mtapata taabu sana.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

SPIKA: Miswada ya Sheria ya Serikali.

NDG. NENELWA MWIHAMBI - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Kumi na Moja (11) kwa lengo la kuboresha Sheria husika illi ziendane na mabadiliko ya wakati na kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (A Bill for An Act to Amend Certain Written Laws)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Katibu.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

SPIKA: Kamati ya Mipango.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Sasa Mheshimiwa Waziri ni wakati wako wa kuchukua nafasi na kutupitisha kwenye hotuba yako ya Mpango wa Taifa. Karibu sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, tafadhalii.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kutoa ushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena hapa Jijini Dodoma kwa ajili ya kutekeleza majukumu muhimu ya kikatiba ya Mhimili huu wa Bunge kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Vilevile, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu umoja na amani ambavyo vimekuwa nguzo muhimu ya kutuwezesha sisi Watanzania kuendelea kutekeleza majukumu yetu, kila mmoja katika nafasi yake na kuchangia katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufikisha umri wa miaka 60 tangu kuzaliwa kwake. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendeleee kumjalia afya njema na maisha marefu zaidi ili kutuwezesha Watanzania wote kufurahia mafanikio makubwa ambayo yanaendelea kupatikana chini ya uongozi wake mahiri. Hakika tunajivunia kumpata kiongozi mchapakazi, mzalendo, anayechukia rushwa, mtetezi wa wanyonge na mfano wa kuigwa Barani Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa

weledi mkubwa katika kuishauri na kuisimamia Serikali. Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kwa ushauri mzuri walotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa kuanda Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata (2020/2021).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa fedha 2020/2021 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali yanayowasilishwa katika Bunge lako Tukufu ni kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016. Mapendekezo haya ya Mpango na Mwongozo yameainisha vipaumbele na masuala muhimu ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wilaya, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti za Mafungu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 yamezingatia mambo yafuatayo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021); Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kisekta na ya kikanda na hususan Jumuia ya Afrika Mashariki, SADC na AU na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni mwenendo wa viashiria vya uchumi. Uchumi wa Taifa umeendelea kuwa

imara ambapo katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.4 kwa mwaka. Kwa mwaka 2018, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2017 kwa mwaka wa kizio wa 2015. Aidha, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019 (Januari – Juni), Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio wa 2015 lilikua kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huu ulichochewa zaidi na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika ujenzi wa barabara, reli na viwanja vyta ndege; kutengamaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Sekta zilizokua kwa kasi zaidi katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019 ni pamoja na ujenzi (asilimia 16.5), uchimbaji madini na mawe (asilimia 13.7), habari na mawasiliano (asilimia 10.7), maji (asilimia 9.1) na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 9.0). Aidha, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 3.6 mwezi Agosti 2019 na kuendelea kupungua hadi asilimia 3.4 mwezi Septemba 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2019, urari wa malipo ya kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,257.3 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,771.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 27.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, hususan, bidhaa za kukuza mitaji kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha na kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma nje ambapo hadi Agosti 2019, akiba ya fedha za kigeni (bila kujumuisha bidhaa na huduma ambazo zinalipiwa na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja) ilifikia dola za Marekani milioni 5,200.1, ikiwa sawa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 6.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi uliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 27,163.2 Agosti 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Mwenendo wa viashiria vya sekta ya kibenki ulikuwa wa kuridhisha ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa faida kutokana na uwekezaji wa rasilimali kutoka asilimia 6.88 Agosti 2018 hadi asilimia 8.16 Agosti 2019 na kuongezeka kwa faida kutokana na uwekezaji wa mtaji kutoka asilimia 1.68 Agosti 2018 hadi asilimia 1.89 Agosti 2019. Kwa ujumla gharama za mikopo zilipungua ambapo riba za mikopo ziliflikia wastani wa asilimia 16.77 Agosti 2019 kutoka asilimia 17.09 Agosti 2018. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua na kuchochea shughuli za kiuchumi ambapo hadi Agosti 2019 ukuaji ulifikia asilimia 8.2 ikilinganishwa na asilimia 5.2 Agosti 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa thamani ya Shilingi iliendelea kuwa tulivu katika kipindi cha mwaka unaoishia Agosti 2019, ambapo Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh.2,289.1 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,273.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Deni la Serikali lilitifikia shilingi bilioni 52,303.04 Agosti 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 49,283.44 Agosti 2018. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyoonyika Desemba 2018, inaonesha kuwa Deni la Serikali bado ni himilivu katika muda mfupi, wa kati na mrefu kwa vigezo vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika Sura ya Pili ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango na Sura ya Pili katika Sehemu ya Kwanza ya kitabu cha Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2018/2019. katika mwaka 2018/2019 mapato ya ndani yalifikia shilingi triliioni 18.52 sawa na asilimia 88.7 ya lengo la shilingi triliioni 20.89. Kati ya kiasi hicho, mapato yaliyokusanywa na TRA yalikuwa shilingi triliioni 15.51, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi triliioni 2.35 na mapato ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 661.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya mapato kulichangiwa na upotevu wa mapato kutokana na shughuli za magendo na hususan kupitia bandari bubu katika ukanda wa bahari ya Hindi na njia zisizo rasmi mipakani, pamoja na ukwepajji kodi. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yalivuka lengo kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki na kuimarika kwa usimamizi na ufuatilaji wa vyanzo vya mapato husika. Katika kipindi hicho, fedha za misaada na mikopo nafuu zilizopokelewa zilikuwa shilingi trilioni 2.08. mikopo ya nje yenye masharti ya kibashara iliyopatikana ni shilingi trilioni 1.14 na mikopo kutoka katika soko la ndani ni shilingi trilioni 3.95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 27.04, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi trilioni 19.09 na matumizi ya maendeleo yalkuwa shilingi trilioni 7.94. Vile vile, Serikali ililipa shilingi trilioni 6.65 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi billioni 599.94 kwa ajili ya madeni ya wakandarasi, wazabuni na watumishi wa Serikali. Kadhalika, katika kipindi hicho, Serikali ilitoa jumla ya shilingi trilioni 7.70 kwa ajili ya kulpia kwa wakati mitaji (*principal*) na riba kwa mikopo ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeleo ya kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2018/2019 yanapatikana katika Sehemu ya Kwanza ya kitabu cha Mwongozo (Sura ya Pili).

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 na robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2018/2019 na robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020 ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere. Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa daraja la muda namba 2; utafiti wa

miamba na udongo; uchimbaji wa mitaro ya chini kwa chini (*adit tunnel*) wenyewe urefu wa mita 147.6 kuelekea kwenye mtaro wa chini kwa chini wa kuchepua maji ya Mto Rufiji (*diversion tunnel*); na mtambo wa kuchakata kokoto (*Batching Plant and Crusher*) namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni Mradi wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge*. Ujenzi wa reli hii kwa sehemu ya Dar es Salaam mpaka Morogoro (km 300) umefikia asilimia 63 na sehemu ya Morogoro mpaka Makutupora kilomita 4,222 imefikia asilimia 16.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; ndege nne zimepokelewa ambapo mbili ni aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* na mbili ni aina ya *Airbus A220-300*, lakini pia tumelipa sehemu ya gharama ya ununuzi wa ndege moja aina ya *Bombardier Dash 8 Q400* inayotarajila kuwasili Disemba 2019. Pia tumesaini mikataba na kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege nyingine mpya tatu ambapo mbili ni aina ya *Airbus A220-300* na moja ni aina ya *Bombardier Q400*. Aidha, Shirika limeongeza idadi ya vituo vya safari za ndani kufikia 11 na nje ya nchi kufikia vituo sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nne kuhusu Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda mpaka Chongoleani Tanga. Tanzania iliendelea na majadiliano ili kufikia makubaliano na Serikali ya Uganda na *Mwekezaji yaani Host Government Agreement*, pia tafiti za *Mateocean*, Kijiolojia na Kijiofizikia katika eneo la Chongoleani - Tanga zimekamilishwa na kazi ya usanifu wa kina wa kiuhandisi yaani *detailed engineering design* wa eneo la ujenzi wa mradi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, tano ni mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kule Lindi. Serikali inaendelea na majadiliano na kampuni za mafuta yaani *Equinor* na *Shell* katika kitalu namba moja, mbili na nne katika Bahari Kuu. Aidha, Tathimini ya athari za mazingira na jamii pamoja na mpango wa uhamishaji wa wananchi watakaopisha eneo la mradi imekamilika.

Mheshimiwa Spika, sita ni makaa ya mawe Mchuchuma na Vanadium, *Titanium* na Chuma kule Liganga. Kazi zilizotekelze wa ni pamoja na kukamilika kwa utafiti wa kina kuhusu wingi, aina na thamani ya madini katika miamba ya Liganga na uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, saba ni shamba la miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi. Hatua iliyofikiwa kwa upande wa Shamba la Mkulazi namba moja ni kukamilika kwa michoro ya ujenzi wa bwawa la maji lenye ukubwa wa mita za ujazo milioni 15 na maandalizi ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha sukari. Kwa upande wa shamba la Mbigriri yaani Mkulazi namba mbili, hatua iliyofikiwa ni kuendelea kwa ujenzi wa majengo wa kiwanda cha sukari, kuboresha miundombinu ya barabara na majengo na kupatikana kwa mzabuni wa kutengeneza na kufunga mitambo ya kiwanda ambapo mikataba imesainiwa.

Mheshimiwa Spika, nane ni miradi ya umeme; mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kv 220 Makambako mpaka Songea umekamilika na utekelezaji wa miradi ya kufua umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati ikiwemo maji na gesi unaendelea. Aidha, Serikali imeendelea na juhudhi na kupeleka umeme vijiji hususani kupitia awamu ya tatu ya miradi ya nishati vijiji (*REA*) ambapo hadi Septemba, 2019 jumla ya vijiji 8,102 vilikuwa vimefikishiwa umeme kati ya vijiji 12,268 vya Tanzania Bara, sawa na asilimia 66.04. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tisa ni miradi ya mji mijini na vijiji. Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya kitaifa na kukamilisha ulazaji wa mabomba, upanuzi na ukarabati katika maeneo yanayohudumiwa na miradi na kuboresha huduma za maji vijiji ambapo miradi 1,659 ya maji vijiji imekamilika. Aidha, miradi 653 ya maji vijiji ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kumi ni miradi ya viwanda. Serikali inaendelea kuimarisha Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*),

ukarabati na upanuzi wa Kiwanda cha Ngozi na Bidhaa za Ngozi cha Karanga Moshi na kuimarisha Shirika la Nyumbu ili kuongeza uzalishaji ikiwemo kuzalisha magari ya zimamoto.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja ni kwa upande wa barabara na madaraja; Serikali imeendelea kugharamia ujenzi wa barabara za lami nchini ambapo Mtandao wa barabara kuu umefikia kilomita 8,306 na mtandao wa barabara za mikoa umefikia kilomita 1,756. Ujenzi wa madaraja yafuatayo umekamilika. Kwanza ni Sibiti kule Singida, Momba mpakani mwa Songwe na Rukwa, Mlalakuwa Dar es Salaam na Lukuledi kule Lindi. Aidha, ujenzi wa barabara na madaraja mengine upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili ni kwa upande wa meli katika Maziwa Makuu. Ujenzi wa Meli ya MV Mbeya katika Ziwa Nyasa umekamilika na vilevile mikataba ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria na Tanganyika imeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kumi na tatu ni viwanja vyatya ndege. Ujenzi wa jengo la tatu la abiria *Terminal III* katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umekamilika na jengo hilo limeanza kutumika. Ujenzi na ukarabati wa kiwanja cha Mwanza umefikia asilimia 95. Aidha, ujenzi na ukarabati wa viwanja vyatya ndege katika baadhi ya mikoa upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kumi na nne ni upande wa bandari; uboreshaji wa gati namba moja na namba mbili katika Bandari ya Dar es Salaam na ujenzi wa gati la RoRo vimekamilika. Aidha, uboreshaji wa gati namba tatu umefikia asilimia 60 na uboreshaji wa Bandari ya Tanga na Mtwara unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kumi na tano ni uwekezaji wa Sekta binafsi. Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana

ni pamoja na kufutwa na kupunguzwa kwa ada na tozo 54 ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na uwekezaji na kuzinduliwa na kuanza uzalishaji katika viwanda saba ambavyo ni Kiwanda cha *Pipe Industries Company Limited*, Kiwanda cha Chai cha Kabambe kule Njombe, Kiwanda cha *Yalin Cashewnut Company Limited*, Mikindani Mtwara; Kiwanda cha 21st *Century Food and Packaging*, Kiwanda cha Kusaga Mahindi cha Kampuni ya Mohamedi *Enterprises Tanzania Limited*; Kiwanda cha Bidhaa za Plastiki cha *Plasco Pipelines Company Limited*; Kiwanda cha Kufungasha na Kuhifadhi Parachichi, Rugwe *Avocado* na Kiwanda cha Kuchakata Parachichi kwa ajili ya kutengeneza mafuta ambacho kinamilikiwa na KUZA Afrika.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2018/2019 na robo ya kwanza ya 2019/2020, yameelezwa kwa kina katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango, Sura ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano kwa kipindi cha toka mwaka 2016/2017 mpaka robo ya kwanza ya 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, yapo mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia 2016/2017 mpaka Septemba mwaka huu. Mafanikio hayo ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa upande wa ukuaji wa uchumi, tulien��ea kuimarisha uchumi wa Taifa ambapo uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2018 kutoka ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2017 na mfumuko wa bei kuendelea kupungua na kufikia asilimia 3.4, Septemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, mapato ya ndani yaliongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 800 kwa mwezi katika mwaka 2016/2017 hadi

kufikia wastani wa shilingi triliuni 1.29 kwa mwezi katika mwaka 2018/2019 kutokana na juhudhi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, juhudhi hizo zimeendelea kuleta mafanikio ambapo mapato ya ndani kwa mwezi Septemba, 2019 yamefikia shilingi triliuni 1.74.

Mheshimiwa Spika, tatu ni ulipaji wa deni la Serikali; tangu mwaka 2016/2017 mpaka Septemba, 2019 Serikali imelipa jumla ya shilingi triliuni 24.49 kwa ajili ya deni liliiloiva la fedha zilizokopwa kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nne ni ulipaji wa mishahara, mishahara ya watumishi wa Serikali yenye jumla ya shilingi triliuni 22.16 ililipwa kwa wakati katika kipindi chote cha 2016/2017 mpaka Septemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, tano ni barabara na madaraja. Ujenzi wa barabara 23 za lami umekamilika hivyo kuongeza mtandao wa barabara kuu za lami kutoka kilomita 7,646 Juni, 2016 hadi kilomita 8,306 Juni, 2018 na mtandao wa barabara za mikoa umeongezeka kutoka kilomita 1,398 mpaka kilomita 756. Barabara ya juu ya Mfugale pale *TAZARA* Dar es Salaam ilikamilika na kuanza kutumika. Ujenzi wa barabara unganishi ya Ubungo yaani Ubungo *Interchange* Dar es Salaam unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 55.

Mheshimiwa Spika, Madaraja yaliyokamilika ni pamoa na Daraja la Magufuli katika Mto Kilombero Morogoro; Kavuu, Katavi; Sibiti, Singida; Momba, mpakani mwa Songwe na Rukwa; Mlalakuwa, Dar es Salaam; Lukuledi, Lindi; na Daraja la waenda kwa miguu la Furahisha kule Mwanza. Pia kazi ya ujenzi wa daraja la Kigongo, Busisi Mwanza imeanza. Aidha, ujenzi wa barabara na madaraja mengine upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, sita, kwa upande wa reli; ujenzi wa reli ya kati ya *standard gauge* unaendelea ambapo sehemu ya Dar es Salaam - Morogoro kilomita 300 umefikia

asilimia 63 na Morogoro - Makutupora umefikia asilimia 16. Aidha, ukarabati wa reli ya kati ya zamani madaraja yake na ujenzi wa makalavati upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Pia ukarabati wa kipande cha reli ya Tanga - Moshi kilomita 353 umekamilika na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, saba, kwa upande wa nishati uwezo wa kuzalisha umeme katika Gridi ya Taifa umeongezeka kufikia Megawati 1,613.52 idadi ya vijiji vilivyounganishwa na umeme umefikia 8,102 kati ya vijiji 12,268 vyta Tanzania Bara sawa na asilimia 66.04 na utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere utakaozalisha megawati 2,115 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nane, kwa upande wa Shirika la Ndege la Tanzania jumla ya ndege mpya 11 zimenunuliwa ambapo ndege saba zimepokelewa, utengenezaji wa ndege moja upo katika hatua za mwisho na inatarajiwaa kuwasili nchini kabla ya mwisho wa mwaka huu. Vilevile ndege tatu zimeanza kutengenezwa baada ya malipo ya awali kulipwa. Aidha, uboreshaji wa Shirika la Ndege la Tanzania umeongeza huduma za usafiri wa anga kutoka vituo 11 nchini na vituo sita nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tisa, Viwanja vya ndege; jengo la abiria la tatu katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere limekamilika na kuanza kutumika. Awamu ya kwanzaya ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro umekamilika; ujenzi na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mwanza umekamilika kwa asilimia 95 na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya mikoa unaendelea na umefikia hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kumi, kwa upande wa bandari, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam unaendelea kama ambavyo nimekwishakueleza na hususani gati la RoRo ambalo limekamilika na kuwesheha meli ya kwanzayenye uwezo wa kubeba magari 6,000 ilihudumiwa katika gati hilo tarehe 15 Septemba, 2019. Uboreshaji wa gati namba tatu

umefikia asilimia 60 na uboreshaji wa Bandari ya Tanga, Mtwara na Bandari za Maziwa Makuu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, upande wa usafiri katika Maziwa Makuu, ujenzi wa Matishari mawili na meli ya *MV Mbeya* katika Ziwa Nyasa umekamilika; ujenzi na ukarabati wa meli tano katika Ziwa Victoria ikiwemo *MV Victoria*, *MV Butiama*, *MV Umoja* na *MV Serengeti* unaendelea na mikataba ya ujenzi wa meli moja mpya na ukarabati wa *MV Liemba* katika Ziwa Tanganyika imeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili, kwa upande wa Kilimo uzalishaji wa mazao ya kilimo katika msimu wa 2018/2019 ulifikia tani 16,408,303 na hivyo kuwa na ziada ya tani 2,565,774 za mazao ya chakula na hivyo kiwango cha utoshelevu wa chakula kilikuwa asilimia 119.

Mheshimiwa Spika, kumi na tatu, kwa upande wa madini Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuboresha mazingira ya biashara kwenye Sekta ya Madini ikihusisha vituo vya umahiri yaani *Centers of Excellence* katika mikoa saba; vituo vitatu vya mfano; jengo la Taaluma ya Madini katika Chuo cha Madini; Kituo cha pamoja cha biashara ya madini yaani *One stop Center* Mererani; jengo la wafanyabiashara *Brokers House* Mererani; uanzishwaji wa masoko 28 ya madini na vituo 11 vya ununuzi wa madini katika mikoa 24 nchini; uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kidijitali Mererani; ununuzi wa mtambo na uchorongaji miamba kwa ajili ya kusaidia wachimbaji wadogo na kufutwa kwa kampuni ya madini ya *ACACIA* na kuundwa badala yake kampuni mpya ya *Twiga Mineral Corporation* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania hisa asilimia 16 na Kampuni ya Barrick hisa asilimia 84.

Mheshimiwa Spika, kumi na nne, kwa upande wa viwanda Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo jumla ya viwanda 3,530 vimejengwa katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kumi na tano, kwa upande wa huduma za afya mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Kitaifa. Ujenzi wa hospitali mpya za wilaya 67 na pia kuanza maandalizi ya ujenzi wa hospitali ya uhuru hapa Dodoma; Hospitali ya Wilaya ya Tunduma kule Songwe; na Hospitali ya Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam. Ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya 470 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98. Pia kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa nyumba 301 za watumishi wa afya na kuendelea na ununuzi wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi.

Mhesimiwa Spika, kumi na sita, kwa upande wa huduma za maji, mradi wa kuboresha huduma za maji Dar es Salaam utekelezaji umefikia asilimia 74. Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria yamelazwa mabomba ya kusambaza maji katika Miji ya Isaka, Tinde na Kagongwa na imekamilika kwa asilimia 99 na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Miji ya Tabora, Igunga, Uyui na Nzega pamoja na vijiji 89 vilivyo pembezoni mwa bomba kuu umefikia asilimia 78. Miradi 1,659 ya maji vijiji imekamilika na ujenzi na ukarabati wa miradi 653 ya maji ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kumi na saba, kwa upande wa elimu Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kugharamia elimu msingi bila ada, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote. Maktaba ya Kimataifa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,600 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilikamilika na kuzinduliwa. Utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu umeendelea pamoja na uimarishaji wa Vyuo vya Ufundis Stadi yaani *VETA*.

Mheshimiwa Spika, kumi na nane, kwa upande wa kuhamishia shughuli za Serikali Makao Makuu Dodoma, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikisha ndoto ya baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Jijini Dodoma kwa ajili ya kurahisisha

utoaji wa huduma kwa wananchi ambapo jumla ya watumishi 8,883 wa Wizara na Taasisi za Serikali wamehamishiwa Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma na ujenzi wa ofisi 23 za Wizara katika Mji wa Serikali pale Mtumba umekamilika ikijumuisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano yameoneshwa katika Sehemu ya Kwanza, Sura ya Pili ya Kitabu cha Mwongozo na Kitabu cha Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2016/2017 hadi robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji wa mpango na bajeti na hatua za kukabiliana nazo. Bajeti ya mwaka 2018/2019, illkabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mahitaji makubwa yasiyowiana na uwezo wa mapato; ukwepaji kodi kwa njia mbalimbali ikiwemo kutotoa stakabali za kieletroniki na kuendesha biashara za magendo hususani kupitia bandari bubu na katika maeneo ya mipakani; mabadiliko ya viwango vya riba katika masoko ya fedha ya nje; kutokupatikana kwa misaada na mikopo kutokana na baadhi ya washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kwa wakati na ukosefu wa takwimu za uwekezaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti, Serikali itaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwianisha mapato na matumizi;

(ii) Kuimarissha ulipaji wa kodi wa hiari kwa kutekeleza Mpango wa Kusimamia vihatarishi vya Mwitikio wa Ulipaji Kodi;

- (iii) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mashine za stakabadhi za kielektroniki kupitia matumizi ya Mfumo ulioboreshwaa;
- (iv) Kuongeza doria na ukaguzi unaolenga kudhibiti biashara za magendo;
- (v) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji;
- (vi) Kukuza soko la fedha la ndani;
- (vii) Kuendeleza majadiliano na Washirika wa Maendeleo na taasisi za fedha za nje;
- (viii) Kutekeleza mwongozo wa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo; na
- (ix) Kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi ili kupata taarifa za uwekezaji wa sekta hiyo katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, tano, mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 misingi iliyozingatiwa katika kuweka malengo ya uchumi jumla ni pamoja na: Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na umoja hapa nchini na katika nchi jirani; kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha ya ndani na ya kimataifa; na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa katika muda wa kati ni pamoja na yafuatayo:-

- (i) Ni kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.0 mwaka 2019 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 7.1 itakapo fika mwaka 2022;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia katika 3.0 - 5.0;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2020/2021 na kufikia wastani wa asilimia 14.9 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2022/2023;

(iv) Matumizi ya Serikali kuwa asilimia 21.7 ya Pato la Taifa mwaka 2020/2021 na asilimia 20.9 ya Pato la Taifa mwaka 2022/2023;

(v) NiKuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada inakuwa chini ya asilimia 3.0 kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Awali wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021, katika mwaka 2020/2021 mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya halmashauri yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi tirioni 23.45 mwaka 2020/2021 kutoka makadirio ya shilingi tirioni 23.045.3 mwaka 2019/2020 na kukadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 8.8 katika muda wa kat. Uwiano wa mapato ya ndani kwa mapato yote unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 68.3 ya bajeti ya mwaka 2020/2021 hadi asilimia 73.7 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.3 hadi shilingi tirioni 19.76 mwaka 2020/2021 kutoka shilingi tirion 18.95 mwaka 2019/2020 na kukua kwa wastani wa asilimia 8.9 katika muda wa kat. Mapato yasiyo ya kodi yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadariwa kuwa shilingi bilioni 3.60 mwaka 2020/2021 na kuongezeka kufikia shilingi tirioni 4.34 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 jumla ya misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi tirioni 1.268 ambapo Misaada ya Kibajeti inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 154.2, Misaada ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta shilingi bilioni 172.9 na Misaada ya Miradi (*Project Funds*) shilingi bilioni 941.5. Aidha, nakisi ya bajeti inayojumuisha misaada inakadiriwa kuwa shilingi tirioni 3.94 sawa na asilimia 2.5 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2020/21 ambapo jumla ya shilingi tirioni 2.35 zitaghamariwa na mikopo ya nje na shilingi tirion 1.58 zitaghamariwa na mikopo ya ndani sawa na asilimia 1 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi tirioni 34.36 sawa na asilimia 21.7 ya Pato la Taifa kutoka shilingi tirion 33.10 mwaka 2019/2020. Matumizi ya kawaida yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.7 hadi shillingi tirioni 21.66 sawa na asilimia 13.7 ya Pato la Taifa na matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi tirioni 12.699. sawa na asilimia 8.0 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu sera za mapato na matumizi katika muda wa kati yapo katika Sehemu ya Kwanza – Sura ya Tatu ya Kitabu cha Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, Maelekezo Mahsus ya Mwongozo Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 umeainisha maelekezo mbalimbali ambayo Maafisa Masuuli watatakiwa kuyazingatia wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuutiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa. Hivyo, Maafisa Masuuli watatakiwa kutekeleza kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo na kusimamia Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Kanuni zake.

Aidha, Kamati za Mipango na Bajeti za kila Fungu zitatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za mwaka 2015. Baadhi ya maelekezo yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli ni yafuatayo:-

- (i) Kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Mafungu;
- (ii) Ni Kubuni na kuboresha mifumo ya usimamizi wa mapato ikiwemo kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari;
- (iii) Kupitia, kurekebisha na kuandaa sheria ndogo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na utawala bora katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iv) Kuhakikisha gharma za miradi inayoendelea zinajumuishwa kwenye mpango wa muda wa kati na bajeti kabla ya kuanzisha miradi mipya;
- (v) Kufanya ukadiriaji sahihi wa stahili za kisheria kama vile posho, pango, umeme, simu na maji kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia mabadiliko baada ya shughuli za Serikali kuhamishiwa Dodoma;
- (vi) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa kwa kutumia ukomo wa bajeti uliotolewa;
- (vii) Kuhakikisha Kamati za Bajeti za Mafungu zinafanya kazi kwa kuzingatia Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake;
- (viii) Kuandaa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia Waraka wa Katibu Mkuu Utumishi;
- (ix) Kuandaa na kuwasilisha mikakati ya uwekezaji, mwongozo wa gawio na mipango ya biashara kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuidhinishwa;

(x) Kuandaa na kuwasilisha kwa Msajili wa Hazina mpango mkakati wa kuboresha utendaji wa mashirika ili kuepuka kuijidesha kwa hasara;

(xi) Kubuni mikakati ya kuongeza vyanzo vyta mapato ya ndani;

(xii) Kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 10(A) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 kwa kutenga na kuwasilisha kwa wakati katika Mfuko Mkuu wa Hazina michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi;

(xiii) Kuzingatia viwango vyta ukomo wa bajeti vilivytotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;

(xiv) Kuandaa mpango na bajeti kwa kuzingatia muundo wa Matumizi wa Muda wa Kati na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Mawasilisho hayo yanatakiwa kufanyika wiki ya tatu ya Januari, 2020 baada ya kuidhinishwa katika ngazi za maamuzi husika ikijumuisha Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura 105.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu maelekezo mahsus ya Mwongozo yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli yanapatikana katika Sehemu ya Pili ya Kitabu cha Mwongozo (Sura ya Kwanza na Sura ya Pili).

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo manne ya kipaumbele yanayojumuisha miradi ya kielelezo iliyobainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Maeneo ya kipaumbele pamoja na baadhi ya miradi itakayopewa kipaumbele kwa mwaka ujao wa fehda 2020/21 ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa upande wa ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda ni kuendelea kuimarisha

sekta ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa mbegu na pembejeo za kilimo pamoja na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji magala na masoko kujenga viwanda vinavyotumia mali ghafi zinazopatikana nchini hususani za kilimo, kuimarisha shirika la viwanda vidogo SIDO kuweza kuhudumia wananchi wengi zaidi ili kuchochea mageuzi ya viwanda nchini; kuanzisha na kuendeleza maeneo ya viwanda (*Industrial parks*) na Kanda Maalum za Kiuchumi; kuboresha utendaji kazi na kutumia taasisi za umma za utafiti na huduma za viwanda; kuanza shughuli za ujenzi katika mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga; na kuendeleza Shamba la Miwa na kuendelea na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi.

Mheshimiwa Spika, pili, Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu Serikali itaendelea: kuimarisha upatikanaji wa elimu na huduma za ustawi wa jamii; kuboresha huduma za afya ikiwemo kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba kwa ajili ya kutoa huduma za tiba kwa wananchi; kuboresha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama vijijini na mijini; kuimarisha usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; kuimarisha shughuli za utawala bora ikiwemo Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; kuendelea kutekeleza sera ya elimu msingi bila ada, kusomesha wataalam na mafundi wengi wenye fani na ujuzi maalum; na kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni Ujenzi wa Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji na hapa Serikali inadhamiria kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ikijumuisha miundombinu ya nishati, lakini pia ile usafirishaji (reli, madaraja, barabara na bandari), usafiri wa anga na usafiri wa majini kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji ikiwemo kutekeleza *Blue Print*; na kuimarisha mfumo wa ugawaji na usimamizi wa ardhi. Miradi itakayopewa msukumo ni: Mradi wa kufua umeme wa Maji wa Julius Nyerere; ujenzi wa reli ya kati ya *Standard Gauge*; kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; na ujenzi wa

bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Eneo la nne ni kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango Katika mwaka 2020/21, utekelezaji Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) unatarajiwa kukamilika ambapo Serikali itaandaa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) kwa kuzingatia matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ubria Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, katika mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi au kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika maeneo ya kipaumbele. Baadhi ya miradi itakayotekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni pamoja na Mradi wa uzalishaji wa Dawa Muhimu na Vifaa Tiba; Kusambaza Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo cha Kibiashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; Ujenzi wa Reli ya *standard gauge* ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (kampasi ya Dar es Salaam na Kampasi ya Dodoma) na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma; Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza; na Ujenzi wa Reli ya *standard gauge* ya Tanga - Arusha – Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu Maeneo ya kina kuhusu maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka 2020/2021 yapo katika Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango (Sura ya Nne).

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa niaba ya Serikali, napenda kuahidi kuwa maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mapendekezo ya Mpango yatazingatiwa kikamilifu katika uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Aidha, Mapendekezo haya

yatazingatiwa na Maafisa Masuuli wote wakati wa kuandaa Mipango na Bajeti za Mafungu yao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Mapendekezo ya Mpango huu, Serikali itaainisha na kuandaa mipango ya kisekta, kitaasisi na kimaeneo ambayo tunaamini kuwa utekelezaji wa mpango utakaoandalialiwa utachochaea ujenzi wa uchumi wa viwanda, mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango na lakini pia wazingatie ushauri makini wa Bunge wakati watakapoandaa Mipango na Bajeti za Mafungu yao kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika vile vile, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 na kusimamia Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kupongeza kwa dhati hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wako kupunguza matumizi kwa kuanza kutekeleza mfumo wa Bunge mtandao *e-parliament* na kuokoa fedha nyingi zilizokuwa zinatumika kuchapisha nyaraka mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Waheshimiwa Wabunge, na kama ulivyofanya wewe Serikali inatoa rai kwa Wizara na Taasisi zote za Umma kufuata mfano huu mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika naomba nikuhakikishie kwamba hii ni mara ya mwisho Waziri wa Fedha atakuja kusoma karatasi kama hizi. Baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako tukufu Tukufu lipokee, lijadili na kuishauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa kuwasilisha vizuri kabisa mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa na mwongozo wa maandalizi ya mpango huo ambao ni ndiyo mwongozo wa kuweka katika bajeti yetu ya Serikali ya mwaka 2020/2021 ahsante sana sana.

Na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kila kitu kipo katika kitendea kazi chenu hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma iko pale *crystal clear* pale ni safi kabisa mambo mazuri. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti, Mwenyekiti wa bajeti karibu sana Mheshimiwa Ndaki na yeche hotuba yake pia mnayo katika vitendea kazi vyenu Mheshimiwa mwenyekiti wa bajeti tuendelee.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru wakati najaribu kuangaliangalia hapo sikuwa nimeiona taarifa yangu kwa hiyo na mimi itakuwa mara yangu ya mwisho kusoma haya makaratasi mbele zako kwa sababu na mimi siyo BBC yani *born before computer* kwa hiyo, tunakupongeza kwa hatua ulizochukuwa.

Mheshimiwa Spika, hii ni taarifa ya Kamati ya Bunge la Bajeti kuhusu mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa pamoja na mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 94(5) ya kanuni za kudumu za Bunge toleo la mwaka 2016 naomba kuwasilisha taarifa ya kamati ya Bunge ya bajeti kuhusu mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa pamoja na mwongozo wa kutayarisha mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti

kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango huu.

Aidha, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilipitia na kujadili Mpango wa Miaka Tano, Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu (2016/2017 – 2018/2019) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Lengo la kupitia taarifa hizi ilikuwa ni kupata mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano kupitia Mipango ya Maendeleo ya Taifa inayotekelawa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imepitia na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambao unatoa mwelekeo wa namna ya Bajeti ya Serikali utakavyotekelawa pamoja na kubainisha maelekezo mahususi yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara, Taasisi na Wakala wa Serikali na Mashirika ya Umma katika kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji za Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, taarifa yangu ni ndefu kidogo, nitaomba iingie yote kwenye kumbukumbu za Bunge (*Hansard*), kwa hiyo, kuna maeneo ambayo ntayasoma lakini kuna baadhi ya maeneo sitayasoma.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo tu juu ya mapitio ya hali ya uchumi jumla kwa kipindi cha mwaka 2018. Nizungumzie Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo vyta kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umasikini. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka 2018 ukuaji wa pato la Taifa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa kwa wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.3 kwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, aidha, Pato la Taifa la Tanzania limekua kwa kiasi cha asilimia 7.0 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.8 kwa mwaka 2017. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi ni wa kuridhisha kuelekea kufikia malengo ya kiwango cha juu cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilifanya uchambuzi na kubaini kwamba kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Pato la Taifa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji hasa katika miundombinu, upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika, kuimarika kwa huduma za usafirishaji, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha hadi kufikia nusu ya kwanza ya mwaka 2019 sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na ujenzi (asilimia 16.5), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 13.7), habari na mawasiliano (asilimia 10.7), maji (asilimia 9.1) pamoja na usafirishaji mizigo (asilimia 9.0).

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo licha ya kuwa imeajiri zaidi ya asilimia 65 ya wananchi na kuchangia asilimia 28.2 ya Pato la Taifa, bado imekua kwa kiwango kidogo cha asilimia 5.3. Hivyo, Kamati inaona bado kuna haja ya Serikali katika Mpango huu kuendelea kusaidia kuwezesha Sekta ya Kilimo pamoja na Sekta za Ujenzi, Biashara, Uzalishaji Viwandani na Uchukuzi ambazo kwa pamoja zinachangia wastani wa theluthi mbili (asilimia 66) katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo juu ya huduma za kifedha lakini nizungumzie suala la riba za mabenki; moja ya viashiria vya ufanisi wa mfumo wa kibenki ni tofauti ya viwango vya riba kati ya riba za amana na mikopo. Kuwepo kwa tofauti kubwa ni kielelezo (pamoja na mambo mengine) cha kukosekana kwa ufanisi katika Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali na madhubuti kwa lengo la kuongeza ufanisi katika Sekta ya Fedha kwa kuongeza ukwasi kwa mabenki kwa kupunguza *discount rate* kutoka 12% hadi asilimia 6% na sasa imefikia 7%. Pamoja na hatua zote hizo, kiwango cha riba kwenye mikopo binafsi kimepungua kwa asilimia 1.87 tu kutoka asilimia 17.09 mwezi Agosti, 2018 hadi kufikia asilimia 16.77 mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, aidha, riba inayotozwa kwenye amana ni wastani wa 3% na riba inayotozwa kwenye mikopo ni wastani wa asilimia 16 (sawa na tofauti ya asilimia 13. Hii inaashiria kuwa bado kuna tatizo la ufanisi katika viwango vya riba vinavyotozwa kwenye riba za amana na mikopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: kwanza, kuangalia gharama zinazotozwa kwenye huduma zinazotolewa na mabenki; pili, kuangalia vyanzo vikuu vya mapato ya mabenki pamoja na viharishi vinavyoikabili sekta; na tatu, kuangalia kiasi kikubwa cha mikopo ya sekta binafsi kinaelekezwa kwenye maeneo gani? Shughuli binafsi au biashara, uzalishaji viwandani au kilimo?

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu ujielekeze kutatua changamoto hii ili kuongeza ufanisi wa mfumo wa kibenki kupunguza tofauti ya viwango vya riba kati ya riba za amana na mikopo na hivyo kuchochea ukuaji wa mikopo ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mwongozo. Kamati imepitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/2021 ulioandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia sheria, sera, kanuni na miongozo iliyopo wakati wa uandaaji, utekelezaji, uwasilishaji na utoaji taarifa wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mwongozo umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ikiwemo kuandaa mipango inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha, udhibiti wa matumizi yasiyo ya lazima, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao, uingizaji wa takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye mifumo ya *CBMS* na *PlanRep*, miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Halmashauri pamoja na ulipaji na udhibiti wa ulimbikizaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi triliioni 34.36 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 3.78 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2019/2020 ya shilingi triliioni 33.12. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi triliioni 23.46 ikiwa ni sawa na asilimia 68.3 ya bajeti. Kati ya fedha hizo, mapato ya kodi ni shilingi triliioni 19.76, mapato yasiyo ya kodi shilingi triliioni 2.89 na mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 803.76. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha shilingi triliioni 5.212 zikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja ya kuwa Serikali imeainisha kiasi cha fedha itakachotumia katika bajeti ijayo, bado mwongozo huu haujatoa ufumbuzi wa upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wa kibajeti ambapo kwa kiasi kikubwa huelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inashauri mwongozo ujielekeze katika kutatua changamoto hii inayojirudia kila mwaka. Sambamba na hili, Serikali ijielekeze katika kukopa vyanzo vya nje vya fedha vyenye masharti nafuu ili kusaidia sekta binafsi kuweza kukopa ndani na kupata mikopo kwa gharama iliyo nafuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, msisitizo uelekezwe kwenye kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji mapato pamoja na kuimarisha taarifa za walipa kodi kutoka katika kanzidata mbalimbali ili kuwa na mapato endelevu pamoja na kuimarisha makusanyo ya ndani. Kamati inaishauri Serikali

kuharakisha kukamilisha utekelezaji wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kieletroniki la Tanzania kwa lengo la kurahisisha upitishaji wa mizigo katika mipaka na kupunguza gharama ya kufanya biashara nchini. Aidha, Serikali ihakikishe kila Halmashauri zinakusanya mapato yake kwa njia ya Mfumo wa Serikali wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa mikopo chechefu imeendelea kupungua, mapendekezo ya mwongozo bado hayajaweza kuainisha maeneo ya msingi yatakayowezesha taasisi za fedha zitakavyoweza kutatua tatizo la uhaba mkubwa wa mitaji ya kusaidia uwekezaji na biashara ili kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania. Pamoja na wingi wa taasisi za fedha na mabenki nchini bado wananchi hawajapata fursa ya kutumia huduma za kifedha kwa ufanisi katika shughuli zao za kipato na kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, eneo moja ambalo ni changamoto kubwa, ni lile la maoteo ya mapato na matumizi. Mapendekezo yamegusia tu kwamba mapato yatakusanywa kwa asilimia 14.8 kama uwiano na pato la Taifa na matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia asilimia 21.7 ya Pato la Taifa. Hata hivyo, mapendekezo ya mwongozo hayajaeleza ni nini kifanyike hadi tufike kukusanya mapato ya asilimia 18 au 19 au hata 20 ya Pato la Taifa kwa lengo la kuziba nakisi ya bajeti na hivyo kuwa endelevu katika kukuza uchumi wetu kwa kasi nzuri. Makusanyo bado yanaendelea kuwa madogo kuliko matumizi.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kwa kifupi tu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa ule wa Mwaka 2018/2019. Zipo changamoto lakini changamoto iliyopo ni upatikanaji wa mapato ya kutosha kuweza kugharamia miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hivyo, ni mategemeo ya Kamati kuwa Mwongozo wa Mpango na Bajeti utahakikisha maeneo ya upatikanaji wa mapato yaliyoainishwa kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2020/2021 yanasmamiwa ipasavyo ili kuhakikisha fedha zinapatikana katika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyaweka wazi maeneo hayo, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yaainishe mambo kadhaa, kwa mfano vipaumbele tulivyojiwekea vimetekelvezwa kwa kiwango gani? Vipaumbele vipi vibaki kama vilivyo? Au vipi vinahitajika vibadilike kutokana na hali ya kiuchumi na upatikanaji wa fedha?

Mheshimiwa Spika, aidha, kama tunataka kufikia malengo tuliojiwekea, nini kifanyike; na pale ambapo hatujafanya vizuri tufanye nini ili kutimiza malengo tuliojiwekea katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa? Hali hii itatoa taswira ya mwelekeo tunaoelekea na hivyo hapo baadaye kufanya tathmini bora ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2020/2021, nianze na eneo moja la utekelezaji wa miradi mikubwa ya kielelezo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia na kutekeleza kwa mafanikio makubwa miradi ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama vile ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*, Mradi wa Kufua Umeme wa Mwalimu Julius Nyerere, Mradi wa kuboresha Shirika la Ndege na ujenzi wa miundombinu ya barabara. Aidha, pamoja na pongezi hizi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake. Serikali inaendelea na ujenzi wa Reli (*Standard Gauge*) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Morogoro hadi Makutupora. Hata hivyo, Mapendekezo ya Mpango hayaoneshi moja kwa moja mkakati wa ujenzi wa matawi vipande vilivyobaki katika ujenzi wa matawi mengine ya reli hiyo yenye urefu Kilometra 1,815 pamoja na matawi yake.

Mheshimiwa Spika, kiuchumi reli hii inatakiwa ifike katika Mikoa ya Mwanza na Kigoma ili iweze kuunganisha nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Watu wa Congo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na juhudzi za kutafuta mikopo kwa ajili ya kukamilisha matawi yaliyobaki

ya Makutupora – Tabora, Tabora – Kigoma na Tabora – Mwanza. Aidha, ukamilishaji wa Reli hii utapelekea kuimarisha huduma ya usafirishaji wa mizigo kuititia Bandari zetu za Dar es Salaam, Mwanza na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, pili, uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu wa viwanja vya ndege pamoja na Shirika la Ndege. Kamati ya Bajeti inapongeza hatua ya Serikali ya kuimarisha Shirika la Ndege ambalo hapo awali lilikuwa halifanyi kazi vizuri. Ili shirika hili lijiendeshe kwa faida, Kamati inaishauri yafuatayo:-

- (i) Kuongeza miruko mipyä ya ndani na nje ya nchi (*route*) pamoja na kurejesha safari ya Afrika ya Kusini;
- (ii) Kuboresha viwanja vya ndege vya ndani ikiwa pamoja na kuweka taa ili kuongeza idadi ya miruko ya usiku;
- (iii) Kuendelea kuimarisha menejimenti ya shirika pamoja na kuboresha Chuo cha Marubani kwa lengo la kuboresha mafunzo ya Urubani hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zitasaidia kuimarisha Shirika letu la Ndege na hivyo kujijendesha kwa faida na kusaidia upatikanaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, namba tatu, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere. Kamati inaipongeza Serikali pia kwa hatua iliyofikia ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji pamoja na miundombinu yake. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika na hivyo kusaidia maendeleo ya viwanda pamoja na kuendesha mitambo treni ya mwendokasi. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona fursa ya utalii katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itafungulia utalii katika mikoa ya kusini pamoja na kuboresha miundombinu ya maeneo husika. Hivyo, Mapendekezo ya Mpango yajielekeze katika kuainisha mpango bora wa matumizi ya ardhi kwa ajili

ya kupata maeneo ya uwekezaji wa kitalii, kilimo cha umwagiliaji pamoja na maeneo ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa vyanzo vyatapato vya kugharamia Mpango, mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021 unategemea kwa kiasi kikubwa cha upatikanaji wa rasilimali fedha. Takwimu zinaonesha kuwa ugharamiaji wa mipango iliyopita imegawanyika katika vyanzo vikuu vitatu. Moja, mapato kutoka Serikali Kuu yatotakanayo na mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; pili, mikopo ya ndani na nje; tatu, sekta binafsi kutoka ndani na ile inayotokana na uwekezaji kutoka nje (*Foreign Direct Investment*).

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoea taarifa kuwa itatumia kiasi cha shilingi billioni 12.6 kwa mwaka 2020/2021 kugharamia miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha shilingi billioni 10.16 ni fedha za ndani na shilingi billioni 2.53 ni fedha za nje. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa Serikali hukusanya na kutumia kati ya shilingi billioni 8,000 hadi shilingi billioni 9,000 hivyo ni wazi kwamba lengo la kutumia wastani wa shilingi billioni 12,699.4 kwa mwaka lillolokuwa limewekwa kwenye mpango halifikiwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuainisha namna ambavyo itapata na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi (*FDI*) kushiriki katika utekelezaji wa mpango pamoja na kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki na Sekta ya Umma katika kugharamia na kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi. Aidha, msisitizo uelekezwe katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia vyanzo vipyta vyatapato ya kodi, hati fungani, kuongeza mitaji kwa taasisi zake za fedha pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kijumuiya na kikanda. Hatua hizi zitasaidia katika kupata mapato yatakayogharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha pia bado Serikali itaendelea kukopa katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti kwa kupitia dhamana za Serikali na

hati fungani. Hatua hii itasababisha mabenki kupunguza kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi na hivyo kuathiri soko la fedha. Kamati inaishauri Serikali ijielekeze zaidi katika kuongeza udhamini wa wakopaji wadogo (*credit guarantee schemes*) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenewe kwa lengo la kusaidia sekta binafsi kushiriki katika maendeleo ya nchi. Vilevile, Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi Soko la Mitaji (*Liberization of Capital Market*) ili kupunguza athari za Serikali kukopa kwenye soko la ndani. Aidha, inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ikamilishe zoezi la kufanyiwa tathmini ya uwezo wa kukopa na kulipa ili kupanua wigo wa Sekta Binafsi na Serikali kukopa kutoka katika vyanzo vya fedha nya kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, vyanzo vingine vya mapato ambavyo Serikali inaweza kutumia kugharamia miradi ya maendeleo ni kupitia vyanzo mbadala kama vile mikopo maalum ya maendeleo, mifuko maalum ya Serikali, hati fungani za miundombinu na mapato yatokanayo na Sekta za Uvuvi, Madini Utalii na Huduma. Pia, Serikali iendelee kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework - DCF*) ili kukuza mahusiano ya kimaendeleo na hivyo kusaidia upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wa kibajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika kuchangia maendeleo ya jamii; katika mpango unaopendekezwa na Serikali moja ya jambo ambalo limebainishwa kama hatua ya kukabiliana na changamoto ya mapato ni kuendelea kuhamasisha Watanzania kuchangia katika maendeleo yao wenewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na hatua hii kwa sababu kuu mbili. Kwanza ni lazima Watanzania tuendeleze utamaduni wetu wa kuchangia katika maendeleo yetu wenewe. Pili, hatua ya Serikali kutoa elimu bila malipo haiondoi jukumu la mzazi kuchangia katika ujenzi wa madarasa, vyoo, nyumba za walimu na ofisi pale inapobidi. Jambo ambalo Kamati inaishauri Serikali ni kuweka

mwongozo ambao utatumika kwa Halmashauri zote nchini ili zoezi la uchangiaji lisiwe kandamizi au linalonyanyasa wananchi kutokana na hali zao za kipato zilivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee uwekezaji wa Serikali katika sekta ya kilimo. Mchango wa sekta ya kilimo inayojumuisha mifugo, mazao na uvuvi katika Pato la Taifa ni asilimia 28.2 japo uwekezaji wa Serikali katika sekta hii ni mdogo ukilinganisha na sekta nyingine ambazo Serikali inawekeza kwa asilimia kubwa.

Aidha, sekta hii ya kilimo inaa jiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania, hivyo basi, ni wazi uwekezaji wa Serikali katika kilimo unaweza kuwa na manufaa makubwa hasa katika kupambana na umasikini. Mfano sekta hii inakua kwa wastani wa asilimia 5.3 lakini mchango wake ni asilimia 28.2. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika sekta hili ili iweze kukua zaidi na hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi kwenye Pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu ukuaji wa sekta ya viwanda nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji viwandani. Serikali ijielekeze katika kuondoa vikwazo vinavyozuia maendeleo ya viwanda nchini hasa kwa upande wa ushindani wa viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya nje ya nchi, ufinyu wa mitaji ya kifedha, ghamama kubwa za uzalishaji, uwepo wa miundombinu duni ya uzalishaji (nishati, maji na usafiri) na mlolongo wa taratibu au sheria zinazobadilikabadi lika mara kwa mara na uwepo wa uhusiano hafifu kati ya sekta ya viwanda na sekta nyingine. Ni vema mpango huu ukajielekeza katika kutatua vikwazo hivi pamoja na kuwa na mkakati maalumu wa kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwekeza katika ulinzi wa mwambao wa Pwani, kwa sababu imebainika kwamba biashara ya magendo inasababisha upotevu mkubwa wa mapato, Kamati inashauri kwamba uwepo

uwekezaji wa ununuzi wa boti kwa ajili ya *patrol*, mitambo ya kisasa ya ulinzi wa mipaka pamoja na kuwa na kikosi maalum kinachoshirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama kulinda mwambao wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchumi wa kidigitali, Kamati imebaini kwamba, kuna miala mingi ya fedha na malipo ambayo yanafanyika katika mitandao bila Serikali kupata mapato yoyote. Mfano, yamezuka maduka ya kimtandao (*online shops*) ambapo mmiliki anakawa hana leseni ya biashara lakini anaiza na kununua biashara za mamilioni bila kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maoni ya jumla ambayo nisingependa kuyasoma kwa sababu ya muda, naomba tu nihitimishe kwa kusema, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii illi niweze kuwasillisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali, nao wako hapo naomba watambuliwe kwenye kumbukumbu zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, natambua mchango mkubwa wa Sekretarieti ya Kamati kwa kutuhudumia vizuri hata kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU
MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA
PAMOJA NA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO
NA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango huu. Aidha, katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilipitia na kujadili Mpango wa miaka Tano (2016/2017 – 2020/2021), Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha miaka Mitatu (2016/2017 – 2018/2019) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Lengo la kupitia Taarifa hizi lilikuwa ni kupata mwelekeo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano kupitia Mipango ya Maendeleo ya Taifa inayoteklezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, aidha, pia kamati imepitia na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2020/21 ambao unatoa mwelekeo wa namna ya Bajeti ya Serikali utakavyoteklezwa pamoja na kubainisha maelekezo mahususi yanayopaswa kuzingatiwa na maafisa masuuli wa Wizara , Idara, Taasisi na Wakala wa Serikali na Mashirika ya Umma katika kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji za Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/21.

2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI JUMLA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi vinavyotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu (2016/2017-2018/2019) kwa lengo la kupata mtiririko wa utekelezaji wa viashiria hivyo kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali. Viashiria vya uchumi vilivyoofanyiwa uchambuzi ni Pato la Taifa, Mfumuko wa Bei, Mwenendo wa Thamani shilingi, Deni la Serikali, Urari wa Blashara, Hali ya Umasikini, Upatikanaji wa Chakula na mwenendo wa Sekta ya Fedha kama vilivyoainishwa katika jedwali Na. 1 hapo chini.

Jedwali Na. 1: VIASHIRIA VYA HALI YA UCHUMI KATIKA MWAKA 2016/2017 – 2017/2018

Na.	Kiashiria	Malengo ya Mpango wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021)	Hali ya Utekelezaji	
			2017/2018	2018/2019
1.	Ukuaji wa Uchumi	10.0	6.8	7.0
2.	Mfumuko wa bei	Wigo usiozidi tarakimu moja	4.3	3.2
3.	Deni la Serikali	-	Tsh. trillioni 50,05	Tsh. trillioni 53,05
4.	Mwenendo wa Thamani ya shilingi	2,185.62	2,276.26	2,300.62
5.	Urari wa blashara (usd bilioni)	-	189.1 (Agosti 2018)	-959.6 (Agosti 2019)
6.	Ukuaji wa sekta ya kilimo	7.6	5.6	5.3
7.	Hali ya umasikini	16.7	28.2	26.6
8.	Mwenendo wa Viwango vya riba	-	16.84	16.36
9.	Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi	-	8.0 (Aprili 2018)	10.6 (Aprili 2019)
11.	Ujazi wa Fedha (M3)	-	6	7.7

Chanzo Wizara ya Fedha na Mipango.

2.1. Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ukuaji wa Pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo veya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka 2018 ukuaji wa Pato la Taifa katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa kwa wastani wa **asilimia 5.6** ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa **asilimia 4.3** kwa mwaka 2017.

Aidha, Pato la Taifa la Tanzania limekuwa kwa kiasi cha **asilimia 7.0** kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na **asilimia 6.8** kwa mwaka 2017. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi ni wa kuridhisha kuelekea kufikia malengo ya kiwango cha juu cha **asilimia 10** ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi na kubaini kwamba kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Pato la Taifa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji hasa katika miundombinu (kama vile ujenzi wa reli, barabara na viwanja veya ndege), upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika, kuimarika kwa huduma za usafirishaji, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha hadi kufikia nusu ya kwanza ya mwaka 2019 sekta zilizokuwa na viwango vikubwa veya ukuaji ni pamoja na ujenzi (asilimia 16.5), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 13.7), habari na mawasiliano (asilimia 10.7), maji (asilimia 9.1) pamoja na usafirishaji mizigo (asilimia 9.0).

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo licha ya kuwa imeajiri zaidi ya **asilimia 65** ya Wananchi na kuchangia **asilimia 28.2** ya Pato la Taifa, bado imekuwa kwa kiwango kidogo cha **asilimia 5.3**. Hivyo, Kamati inaona bado kuna haja ya Serikali katika Mpango huu kuendelea kusaidia kuwezesha sekta ya kilimo pamoja na sekta za ujenzi, biashara, uzalishaji viwandani na uchukuzi ambazo kwa pamoja zinachangia wastani wa theluthi mbili (asilimia 66) katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha mwongozo haujaweza kutoa takwimu za mchango wa sekta ya ufugaji na uvuvi, maliasili

na utalii ambazo kwa pamoja zina mchango mkubwa katika Pato la Taifa.Ni vema takwimu hizo zikaainishwa ili Bunge liweze kutoa maoni na ushauri ipasavyo.

2.2. Mfumuko wa bei

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha chini na kubaki katika wigo wa tarakimu moja. Katika ukanda wa Afrika mashariki Mfumuko wa bei ulikuwa kwa wastani wa kiwango cha **asilimia 5.6** kwa mwaka 2018. Nchini mfumuko wa bei uliendelea kuwa ndani ya wigo huo ambapo kiwango cha mfumuko wa bei ulikuwa kwa **asilimia 3.4** na unatarajiwa kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja katika mwaka 2020/2021. Mfumuko wa bei katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kiasi kikubwa unategemea hali ya hewa na upatikanaji wa chakula. Hivyo, bado kuna haja ya kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na chakula cha kutosha hasa ukizingatia hali ya mafuriko yanayoendelea nchini pamoja na kuimarissha ugavi wa nishati (hasa mafuta ya petrol) ili kudhibiti mwenendo wa ukuaji wa mfumuko wa bei.

2.3. Mwenendo wa thamani ya shilingi

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani umekuwa tulivu kutokana na usimamizi na utekelezaji madhubuti wa Sera za Fedha na Bajeti. Hata hivyo, tathmini ya Kamati inaonesha kuwa kumekuwa na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya marekani kwa kiwango cha **asilimia 0.6**. Mwezi Agosti 2018 Dola moja ya Marekani ilibadilishwa katika kiwango cha **shilingi 2,273.7** hadi kufikia Agosti 2019 dola hiyo ilibadilishwa kwa **shilingi 2,289.1**. Viwango hivi ni zaidi ya lengo la **shilingi 2,185.22** iliyojiwekea Serikali katika malengo yake ya miaka mitano. Kamati inashauri Serikali ili kuwa na suluhisho la kudumu la kuimarissha thamani ya shilingi dhidi ya dola ya marekani ni kuongezee mauzo ya bidhaa na huduma nje ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara. Aidha, msisitizo uwekwe zaidi kwenye uzalishaji na uuzaaji nje wa mazao ya biashara kama vile ya kahawa, korosho, karafuu, pamba, tumbaku, chai, mkonge, pareto pamoja na madini. Ni muhimu Serikali ikaanza kutumia soko la bidhaa

(TMX-Tanzania Merchantile Exchange) ili kuhakikisha tunakuwa na uhakika wa masoko ya mazao yetu ya biashara na yale ya asili.

2.4. Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba kumekuwa na ongezeko la Deni la Serikali kutoka **shilingi bilioni 49,283.44** Agosti, 2018 hadi kufikia **shilingi bilioni 52,303.04** ikiwa ni ongezeko la **shilingi bilioni 3,019.6** sawa na **asilimia 6.1** ndani ya kipindi cha miezi 12. Aidha, mchanganuo wa deni lote unaonesha kuwa asilimia **72** ni deni la nje na asilimia 28 ni deni la ndani. Pamoja na kwamba deni hilo ni himilivu kwa viashiria vyote, Kamati inaona kuwa bado kuna haja ya kuangalia upya uhimilivu wa deni hilo ukizingatia kuwa bado kuna mwenendo wa kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola hali inayopelekea deni hilo kuongeza ndeni wakati wa ullipaji wake.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuongezeka kwa deni hili kunapunguza uwezo wa taasisi za fedha kutoa mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kuvuruga soko la fedha. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kudhibiti Deni la Serikali kwa kutafuta vyanzo vingine vya mapato ya Serikali hasa yale ya kodi ya ushuru wa forodha, mapato yasiyo na kodi pamoja na kuangalia misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje.

2.5. Huduma za kifedha.

2.5.1. Ukwasi wa Mabenki

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, sekta ya benki nchini imeendelea kuwa imara, thabitin na yenye kutengeneza faida ikiwa na mtaji wa juu ya ukomo unaohitajika kisheria. Mathalani, hadi kufikia mwezi agosti 2019 uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za Benki umefikia **asilimia 16.8** ukilinganisha na **asilimia 10** ya kisheria. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa hatua hii itakuwa imefikiwa kutokana na; **Kwanza** mabenki kuwa na hofu ya kukopesha sekta binafsi kutokana na historia ya mikopo chechefu katika mwaka 2016 hadi 2018; **Pili**, Sekta Binafsi nchini imekosa mwamko wa kuchukua mikopo kwenye mabenki kutokana na mwenendo

wa biashara kutokuwa imara; Na **Tatu** viwango vyatya riba vimeendelea kuwa vikubwa. Hivyo kamati inaishauri Serikali kufanya kazi changamoto hizi ili kuleta ufanisi katika mifumo ya kibenki pamoja na sekta ya fedha pamoja na kubaini kinachosababisha mabenki yawe na ukwasi zaidi ya kiwango kinachohitajika kisheria.

2.5.2. Riba za Mabenki

Mheshimiwa Spika, moja ya viashiria vyatya ufanisi wa mfumo wa kibenki ni tofauti ya viwango vyatya riba katika ya riba za amana na mikopo. Kuwepo kwa tofauti kubwa ni kielelezo (pamoja na mambo mengine) cha kukosekana kwa ufanisi katika sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imechukua kuchukua hatua mbalimbali na madhubuti kwa lengo la kuongeza ufanisi katika sekta ya fedha kwa kuongeza ukwasi kwa mabenki kwa kupunguza *discount rate* kutoka **asilimia 12** hadi **asilimia 9** na sasa imefikia **asilimia 7**. Pamoja na hatua zote hizo, kiwango cha riba kwenye mikopo binafsi kimepungua kwa **asilimia 1.87** tu (kutoka asilimia 17.09 Mwezi, Agosti 2018 hadi kufikia **asilimia 16.77** Mwezi Septemba 2019). Aidha, riba inayotozwa kwenye amana ni wastani wa **asilimia 3** na riba inayotozwa kwenye mkopo ni wastani wa **asilimia 16** (sawa na tofauti ya asilimia 13) Hii inaashiria kuwa bado kuna tatizo la ufanisi katika viwango vyatya riba vinavyotozwa kwenye riba za amana na mikopo. Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo; **kwanza**, kuangalia gharama zinazotozwa kwenye huduma zinazotolewa na mabenki; **Pili**, kuangalia vyanzo vikuu vyatya mapato ya mabenki pamoja na vihatarishi vinavyoikabili sekta; **Na Tatu**; kuangalia kiasi kikubwa cha mikopo ya sekta binafsi kinaelekezwa kwenye sehemu gani? (Shughuli binafsi? biashara? uzalishaji viwandani? au kilimo?).

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu ujielekeze kutatua changamoto hii ili kuongeza ufanisi wa mfumo wa kibenki kupunguza tofauti ya viwango vyatya riba katika ya riba za amana na mikopo na hivyo kuchochaea ukuaji wa mikopo ya sekta binafsi.

2.5.3. Mikopo kwa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa 2018 kupitia Tamko la Sera ya Fedha, Serikali ilijiwekea lengo la ukuaji wa mikopo ya Sekta Binafsi kufikia **asilimia 11.5** ifikapo Agosti 2019. Pamoja na tamko hilo, lengo hilo halijaweza kufikiwa, kwani mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka kutoka **asilimia 5.2** mwezi agosti mwaka 2018 hadi **asilimia 8.2** mwezi agosti 2019. Hivyo mwongozo huu ujielekeze kuanisha sababu zilizopelekea kutofikia kwa lengo lilitokusudiwa kwa kipindi husika.

3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2020/2021 uliooandalliwa kwa mujibu wa Kifungu cha Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia Sheria, Sera, Kanuni na Miongozo iliyopo wakati wa uandaaji, utekelezaji, uwasilishaji na utoaji taarifa wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Mwongozo umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ikiwemo kuandaa mipango inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha, udhibiti wa matumizi yasiyo ya lazima, matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao (GePG), uingizaji wa takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep, miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Halmashauri (SGRP) pamoja na ulipaji na udhibiti wa ulimbikizaji wa madeni.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021, Sura ya Bajeti inaonyesha kuwa, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 34.36** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.78** ikilinganshwa

na bajeti ya mwaka 2019/20 ya **shilingi triliuni 33.12**. Mapato ya ndani yanatarajia kuwa **shilingi triliuni 23.46** ikiwa ni sawa na **asilimia 68.3** ya bajeti. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni **shilingi triliuni 19.76**, mapato yasiyo ya kodi **shilingi triliuni 2.89** na mapato ya Halmashauri **shilingi bilioni 803.76**. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha **shilingi triliuni 5.212** zikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja ya kuwa Serikali imeanisha kiasi cha fedha itakachotumia katika bajeti ijayo, bado mwongozo huu haujatoa ufumbuzi wa upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wa kibajeti ambazo kwa kiasi kikubwa huelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inashauri mwongozo ujielekeze katika kutatua changamoto hii inayojirudia kila mwaka. Sambamba na hili serikali ijielekeze katika kukopa vyanzo vya nje vya fedha vyenye masharti nafuu ili kusaidia sekta binafsi kuweza kukopa ndani na kupata mikopo kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, msisitizo uelekezwe kwenye kuimarisha mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji mapato pamoja na kuimarisha taarifa za walipa kodi kutoka katika kanzidata mablimbali ili kuwa na mapato endelevu pamoja na kuimarisha makusanyo ya ndani. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kukamilisha utekelezaji wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kieletroniki la Tanzania (TeSWs) kwa lengo la kurahisisha upitishaji wa mizigo katika mipaka na kupunguza gharama ya kufanya biashara nchini. Aidha Serikali ihakikishe kila halmashauri zinakusanya mapato yake kwa njia ya Mfumo wa Serikali wa kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG) .

Mheshimiwa Spika, pamoja ya kuwa mikopo chechefuimeendelea kupungua, mapendekezo ya mwongozo bado hayajaweza kuanisha maeneo ya msingi yatakayowezesha taasisi za fedha zitakavyoweza kutatua tatizo la uhaba mkubwa wa Mitaji ya kusaidia uwekezaji na biashara ili kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania. Pamoja na uwingi wa taasisi za fedha na mabenki nchini bado wananchi wengi

hawajapata fursa ya kutumia huduma za kifedha kwa ufanisi katika shughuli zao za kipato na kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, eneo moja ambalo ni changamoto kubwa ni lile la maoteo ya Mapato na Matumizi. Mapendekezo yamegusia tu kwamba mapato yatakusanywa kwa **asilimia 14.8** kama uwiano na Pato la Taifa na matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia **asilimia 21.7** ya Pato la Taifa. Hata hivyo, mapendekezo ya mwongozo hayajaeleza ni nini kifanyike hadi tufike kukusanya mapato ya **asilimia 18** au **19** au hata **20** ya Pato la Taifa kwa lengo la kuziba nakisi ya bajeti na hivyo kuwa endelevu katika kukuza uchumi wetu kwa kasi nzuri. Makusanyo bado yanaendelea kuwa madogo kuliko matumizi.

4.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19, Serikali ilijielekeza kutekeleza vipaumbele vya kuendeleza viwanda vya kukuza uchumi ambavyo vitaimarishwa na kasi kubwa ya kukua uchumi; miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kukua (flagship projects) na maeneo yanayolenga kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu, kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na kusimamia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza haya, Serikali ilipanga kutumia **shilingi bilioni 11,833.4** (shilingi bilioni 9,698.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 2,134.6 fedha za nje) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/19. Hadi kufikia juni 2019, Jumla ya **shilingi bilioni 7,949.3** zilitolewa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 67.2** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha kwa mwaka 2019, Serikali ilitenga jumla ya **shilingi bilioni 12, 248.6** (sawa na asilimia 37 ya bajeti) kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Septemba 2019 kiasi cha **shilingi bilioni 1,875.1** kimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo Mifuko ya Reli, REA na Maji (bilioni 108.431); Mikopo ya wanafunzi (bilioni 65.17); Ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege (bilioni 65.07), ughramiaji wa miradi ya maendeleo ya halmashauri (bilioni 5.68); malipo ya mkandarasi Terminal III (bilioni 140.89) pamoja na mradi wa kufufua umeme wa maji wa Mwalimu Julius Nyerere n.k. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo takwimu zinaonesha kuwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha kiasi kinachokuwa kimetolewa kwenye miradi ya maendeleo kinafikia kati ya asilimia 60-70. Hivyo ni dhahiri baadhi ya miradi mingine ya maendeleo inakuwa inaanathirika na utekelezaji wake kutokana na changamoto upatikanaji wa fedha za ndani na za nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeo. Mfano Miradi wa Makaa ya mawe Mchuchuma, vanadium, Titanium na chuma- Liganga, Mradi wa Kiwanda cha Matairai Cha *General tyre*, Kurasini Logistic Centre pamoja na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, aidha bado kuna urasimu katika kutekeleza miradi ya maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ/ SEZ) hasa kwa upande wa kukamilika mikataba na ulipaji wa fidia mfano mradi wa bagamoyo, eneo la uwekezaji kigoma, Mtwara na mengine. Pia bado kuna uendelezaji hafifu wa maeneo ya Kanda maalumu za uwekezaji kama vile Dodoma, Ruvuma, Manyara, Mara, Manyoni na Tanga

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni upatikanaji wa mapato ya kutosha kuweza kugharamia miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imeanishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hivyo ni mategemeo ya Kamati kuwa mwongozo wa Mpango na Bajeti utahakikisha maeneo ya upatikanaji wa mapato yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 yatasimiwa ipasavyo ili kuhakikisha fedha zinapatikana katika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyaweka wazi maeneo haya, Mapendekezo ya Mpango wa maendeleo yaainishe mambo kadhaa, kwa mfano vipaumbele tulivyojiwekea vimetekelawa kwa kiwango gani? Vipaumbele viyi vibaki kama vilivyo au viyi vinahitajika vibadilike kutokana na hali ya kiuchumi na upatikanaji wa fedha. Aidha, kama tunataka kufikia malengo tuliojiwekea nini kifanyike na pale ambapo hatujafanya vizuri tufanye nini ili kutimiza malengo tuliojiwekea katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hali hii itatoa taswira ya mwelekeo tunaoelekeea na hivyo hapo badee kufanya tathmini bora ya utekelezaji.

5.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 na ingependa kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

5.1. Utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Kielelezo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia na kutekeleza kwa mafanikio miradi mikubwa ya kielelezo ilioainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama vile ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge, Mradi wa Kufua Umeme wa Mwl. Julius Nyerere (MW 2115), Mradi wa kuboresha shirika la ndege la ATCL na ujenzi wa miundombinu ya barabara. Aidha pamoja na pongezi hizi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

5.2. Ujenzi wa Reli ya Kati na Matawi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Reli (Standard Gauge) kutoka Dar es Salaam-Morogoro na Morogoro-Makutupora. Hata hivyo Mapendekezo ya Mpango hayaoneshi moja kwa moja mkakati wa ujenzi wa matawi vipande vilivybaki katika ujenzi wa matawi mengine ya Reli hiyo yenye urefu Km1,815 pamoja na matawi yake. Kiuchumi Reli hii inatakiwa ifike katika Mikoa ya Mwanza na Kigoma ili iweze kuunganisha nchi jirani za Rwanda, Burundi,

Uganda na Jamhuri ya Watu wa Congo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na juhudhi za kutafuta mikopo kwa ajili ya kukamilisha matawi yaliyobaki ya Makutupora-Tabora, Tabora-Kigoma na Tabora-Mwanza. Aidha ukamilishaji wa Reli hii utapelekea kuimarisha huduma ya usafirishaji wa mizigo kupitia bandari zetu za Dar es Salaam, Mwanza na Kigoma.

5.3. Uimarishaji na uendelezaji wa Miundombinu wa Viwanja vya Ndege pamoja na Shirika la ATCL.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti inapongeza hatua ya Serikali ya kuimarisha Shirika la Ndege -ATCL ambalo hapo awali lilikuwa halifanyi kazi vizuri. Ili shirika hili lijiendeshe kwa faida, Kamati inaishauri Serikali;

- i. Kuongeza miruko mipyä ya ndani na nje ya nchi (route) amoja na kurejesha safari ya Afrika ya Kusini;
- ii. Kuboresha viwanja vya ndege vya ndani ikiwa pamoja na kuweka taa ili kuongeza idadi ya miruko ya usiku;
- iii. Kuendelea kuimarisha menejimenti ya shirika pamoja na kuboresha chuo cha marubani kwa lengo la kuboresha mafunzo ya urubani hapa nchini;

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zitasaidia kuimarisha Shirika la Ndege -ATCL na hivyo kujiendesha kwa faida na kusaidia upatikanaji wa mapato ya Serikali.

5.4. Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere (MW 2,115)

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji pamoja na miundombinu yake. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika na hivyo kusaidia maendeleo ya viwanda pamoja na kuendesha mitambo ya treni ya mwendokasi. Aidha, Kamati inapongeza Serikali kwa kuona fursa ya utalii katika eneo hili na hivyo kuweza kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. Hatua hii itafungulia utalii katika mikoa ya kusini pamoja na kuboresha

miundombinu ya maeneo husika. Hivyo mapendekezo ya Mpango yajielekeze katika kuainisha mpango bora wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya kupata maeneo ya uwekezaji wa kitalii, kilimo cha umwagiliaji pamoja na maeneo ya kuanzisha viwanda vidogovidogo.

5.5. Upatikanaji wa vyanzo vya mapato vya kugharamia Mpango

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 unategemea kwa kiasi kikubwa cha upatikanaji wa rasilimali fedha. Takwimu zinaonesha kuwa ugharamiajai wa mipango iliyopita imegawanyika katika vyanzo vikuu vitatu yaani; Moja; mapato kutoka Serikali kuu yatotakanayo na mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; Pili, Mikopo (ndani na nje); Tatu, Sekta Binafsi kutoka ndani na ile inayotokana na uwekezaji kutoka nje (Foreign Direct Investment). Serikali imetoa taarifa kuwa itatumia kiasi cha shilingi bilioni 12,699.4 kwa mwaka 2020/21 kugharamia miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha shilingi bilioni 10,163.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,536 ni fedha za nje. Aidha takwimu zinaonesha kuwa Serikali hukusanya na kutumia kati ya billioni 8,000 hadi bilioni 9,000 hivyo ni wazi kwamba lengo la kutumia wastani wa shilingi bilioni 12,699.4 kwa mwaka liliokuwa limewekwa kwenye mpango halitafikiwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuanisha namna ambavyo itapata na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi (FDI) kushiriki katika utekelezaji wa mpango pamoja na kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki na Sekta ya Umma katika kugharamia na kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi. Aidha msisitizo uelekezwe katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kuititia vyanzo vypya vya kodi, hati fungani, kuongeza mitaji kwa taasisi zake za fedha pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kijumuiya na kikanda. Hatua hizi zitasaidia katika kupata mapato yatakayo gharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha bado Serikali itaendelea kukopa katika soko la fedha la ndani ili kuziba

nakisi ya Bajeti kwa kupitia dhamana Serikali na hati fungani. Hatua hii itasababisha mabenki kupunguza kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi na hivyo kuathiri soko la fedha. Kamati inaishauri Serikali ijielekeze zaidi katika kuongeza udhamini wa wakopaji wadogo (*credit guarantee schemes*) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenyewe (*lease finance*) kwa lengo la kusaidia sekta binafsi kushiriki katika maendeleo ya nchi. Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi Soko la Mitaji (*Liberization of Capital Market*) ili kupunguza athari za Serikali kukopa kwenye soko la ndani. Aidha, inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ikamilishe zoezi la kufanyiwa Tathmini ya Uwezo wa kukopa na Kulipa (*Credit Rating*) ili kupanua wigo wa Sekta Binafsi na Serikali kukopa kutoka katika vyanzo vyta fedha vya nje kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Aidha, vyanzo vingine vya mapato ambavyo Serikali inaweza kutumia kugharamia miradi ya maendeleo ni kupitia vyanzo mbadala kama vile mikopo maalum ya maendeleo, mifuko maalum ya Serikali, hati fungani za miundombinu na mapato yatokanayo na sekta ya uvuvi, madini utalii na huduma. Pia, Serikali iendelee kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework-DCF*) ili kukuza mahusiano ya kimaendeleo na hivyo kusaidia upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wa kibajeti.

5.6. Ushirikishwaji wa Wananchi katika kuchangia Maendeleo ya jamii

Mheshimiwa Spika, Katika mpango unaopendekezwa na Serikali moja ya jambo ambalo limebainishwa kama hatua ya kukabiliana na Changamoto ya Mapato ni kuendelea kuhamasisha Watanzania kuchangia katika maendeleo yao wenyewe. Kamati inakubaliana na hatua hii kwasababu kuu mbili; **kwanza** ni lazima Watanzania tuendeleze utamaduni wetu wa kuchangia katika maendeleo yetu wenyewe; **Pili** hatua ya Serikali kutoa elimu bila malipo haiondoi jukumu la mzazi kuchangia katika ujenzi wa madarasa, vyoo, nyumba za walimu na Ofisi na pale inapobidi ni vyakula vya shule. Jambo ambalo kamati inaishauri Serikali ni kuweka

mwongozo ambao utatumika kwa Halmashauri zote nchini ili zoezi la uchangiaji lisiwe kandamizi au linalonyanyasa wananchi kutokana na hali zao.

5.7. Uwekezaji wa Serikali katika Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, mchango Sekta ya Kilimo inayojumuisha mifugo, mazao na uvuvi katika Pato la Taifa ni asilimia 28.2 japo uwekezaji wa Serikali katika Sekta hii ni mdogo ukilinganisha na Sekta nyingine ambazo Serikali inawekeza kwa asilimia kubwa. Adha,Sekta hii ya kilimo inaaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. Hivyo basi ni wazi uwekezaji wa Serikali katika kilimo unaweza kuwa na manufaa makubwa hasa katika kupambana na umasikini. Mfano Sekta hii inakuwa kwa wastani wa asilimia 5.3 lakini mchango wake ni asilimia 28.2 Kamati inashauri Serikali kuwekeza zaidi katika sekta hii ili iweze kukua zaidi na hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi kwenye Pato la Taifa kupitia.

5.8. Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa mapendekezo ya Mpango huu yaanishe mikakati ya Serikali katika kupanga matumizi bora ya ardhi ukizingatia kuwa idadi ya watu inazidi kuongezeka wakati matumizi ya ardhi yanaendelea kuongezeka. Hatua hii itasaidia vizazi vijavyo kuweza kupata ardhi pamoja na kulinda maliasili zilizopo kama vile misitu, vyanzo vya maji, mabonde na rasilimali nyinginezo. Aidha, sambamba na hili matumizi mengine ya ardhi lazima yaanishwe hasa yanayohusu ujenzi wa miundombinu, viwanda, kilimo pamoja na malisho ya mifugo.

5.9. Ukuaji wa Sekta ya Viwanda nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji viwandani. Serikali ijielekeze katika kuondoa vikwazo vinavyozuia maendeleo ya viwanda nchini hasa kwa upande wa ushindani wa viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazosalishwa na viwanda vya nje ya nchi, ufinyu wa mitaji ya kifedha, gharama kubwa za uzalishaji, uwepo wa miundombinu duni ya uzalishaji (nishati, maji na usafiri) na mlolongo wa taratibu au sheria zinazobadilika mara kwa

mara; na uwepo wa uhusiano hafifu kati ya sekta ya viwanda na sekta nydingine za kiuchumi. Ni vema Mpango huu ukajielekeza katika kutatua vikwazo hivi pamoja na kuwa na mkakati maalumu wa kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa viwandani.

5.10. Usimamizi, ufuutiliaji na utoaji wa taarifa.

Mheshimiwa Spika, ili Mpango huu ufanikiwe katika utekelezaji wake, Serikali lazima iendelee kuboresha usimamizi, ufuutiliaji na utoaji wa taarifa endelevu za utekelezaji dhidi ya hatua ya malengo yatakayokuwa yanafikiwa. Kamati inasisitiza Mpango huu ujielekeze katika utaratibu maalumu wa kuchanganuo kwa kina taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kujua hatua inayofikiwa kwa kila mradi. Hatua hizi zitasaidia kufanya tathmini za utekelezaji wa miradi husika.

5.11. Kuwekeza katika ulinzi wa mwambao wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, kwasababu imebainika kwamba biashara ya magendo inasababisha upotevu mkubwa wa mapato. Uwekezaji huo ni ununuzi wa boti kwa ajili ya *Patrol*, mitambo ya kisasa ya ulinzi wa mipaka pamoja na kuwa na kikosi maalumu kinachoshirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama kulinda mwambao huo.

5.12. Uchumi wa kidijiti “Digital Economy”.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba kuna miala mingi ya fedha na malipo ambayo inafanyika katika mitandao bila Serikali kupata mapato yoyote. Mfano. Yamezuka maduka ya kimtandao “online shops” ambapo mmiliki anakuwa hana leseni ya biashara lakini anaauza na kununua biashara za mamillioni bila kulipa kodi stahiki.

6.0. MAONI YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsus, Kamati inashauri maeneo yafuatayo yaongezwe kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21: -

- i. Reli ya Mtwara Mbambabay na matawi yake ya kwenda Liganga na Mchuchuma;

- ii. Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi ya asili (LNG) – Lindi;
- iii. Mradi wa Magadi Soda Engaruka katika Ziwa Manyara;
- iv. Uanzishwaji wa maeneo maalum ya uwekezaji Bagamoyo unaojumuisha ujenzi wa bandari;
- v. Miradi mipya ya uchimbaji wa madini ya Gesi (Mikubwa na Midogo);
- vi. Kiwanda cha Gesi na Kemikali katika Mkoa wa Mtwara;
- vii. Mradi wa Kuboresha mazingira ya Biashara ya bidhaa za nguo na mavazi;
- viii. Viwanda vya Nyama na Ngozi Ruvu;
- ix. Mradi wa Skimu ya umwagiliaji nchini;
- x. Serikali iainishe katika Mapendekezo ya Mradi Program zitakazowezesha Digital Economy kuleta manufaa zaidi nchini;
- xi. Serikali iongeze katika Mapendekezo Mradi wa uanzishwaji wa Mnada/Masoko ya chai, pamba na Kahawa nchini ili kuacha kutumia mnada unaofanyika Kenya;
- xii. Serikali iongeze katika Mapendekezo ya Mpango Mradi wa kuboresha zao la Zabibu na "Value Chain yake (page 159 – FYDP II);
- xiii. Serikali iongeze katika Mapendekezo ya Mpango Mradi wa Kuboresha Mifumo ya kuuza Mazao ikiwemo kuboresha na kutumia "Tanzania Merchantile Exchange" (TMX) kwa mazao yote yanayozalishwa nchini;
- xiv. Serikali iongeze katika Mapendekezo ya Mpango Mradi wa Kuanzisha soko la hisa la Madini.

7.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Makamu Mwenyekiti
2. Mhe. David Ernest Silinde, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Shally J. Raymond, Mb - Mjumbe

25. Mhe. Jummane Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Joseph Kakunda - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, natambua mchango mkubwa wa Sekretariati ya Kamati kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Mashimba M. Ndaki, Mb

MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

05 Novemba, 2019

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kuja kusoma taarifa ya Kamati yako wewe mwenyewe. Tunakushuruku sana kwa kusoma kwa umakini mkubwa na kwa kutumia muda vizuri. (*Makofii*)

Sasa baada ya Kamati ya Bajeti iliyopitia Mapendekezo haya kwa niaba yetu kutoa taarifa yake, taarifa nzuri, nimuite mtoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali karibu.

MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru sana lakini naona *e-Mtandao* inachelewa kwa muda ndiyo maana tumeshindwa kuja na *iPad* zetu.

MWENYEKITI: Haichelewi, kila kitu kiko.

MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MPANGO: Hapa haipo, haipo *serious*.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MPANGO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema mpaka baada ya dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya na uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Bunge tukiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkutano huu wa Bunge...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwashakikisheni kwa sasa hii hotuba ipo katika *tablets* zenu. Kwa hiyo, ye ye aendelee kusoma makaratasilakini nataka kuwashakikisheni hilo ili muweze kufuatilia. Mheshimiwa Silinde, endelea.

MHE. DAVID E. SILINDE - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MPANGO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkutano huu wa Bunge unaofanyika mwezi Novemba 2019, kipindi ambacho tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kuzungumzia mambo mambo machache kuhusu uchaguzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawapongeza wananchi wote waliotumia haki yao ya kikatiba kujitokeza kujianidikisha ili kushiriki katika uchaguzi wa viongozi wanaowataka. Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwashimiza wananchi wote walijitokeza kushiriki kwa wingi kupiga kura siku ya tarehe 24 ambazo sisi hatutakuwepo. Tatu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuititia Wasimamizi wa Uchaguzi huo, kusimamia kwa haki zoezi la upigaji kura,

uhesabuji kura na kumtangaza mshindi halali kwa mujibu wa muonekano halisi wa kura zilizopigwa. Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawakumbusha wananchi kuchagua viongozi bora watakaojinadi kwa sera madhubuti zitakazowanasua katika vifungo vya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge ambao umeangukia katika kipindi cha mwezi Oktoba – Novemba na kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Bunge hili linakaa kama Kamati ya Mipango ili kujadili na kuishauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha unaofuata (2020/2021).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati dhima ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), ni Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochaea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu tunaingia mwaka wa tano na wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa, hali ya uchumi na maendeleo ya watu katika kaya hapa nchini ikiwa ni mbaya zaidi kuliko kipindi kilichotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021), Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilifanya mapitio mafupi ya hoja za msingi ilizoziuba katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo katika miaka mitatu iliyopita na ambazo hazijafanyiwa kazi mpaka sasa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani itafanya uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa miaka mitatu ili kuona kama kuna uhalisia kati ya kile ambacho Serikali inakihubiri kwamba imepata mafanikio makubwa au kuna utofauti. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani itafanya mapitio ya Mapendekezo ya Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kutoa maoni na mapendekezo yake kwa ajili ya utekelezaji bora wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambazo mpaka sasa hazijafanyiwa kazi. Yapo mambo kadhaa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali hii kwa miaka minne mfululizo sasa ambayo yangesaidia kutekeleza mipango yetu ya maendeleo kwa ufanisi lakini Serikali imegoma kuyafanya kazi. Mambo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo. Tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012-2015/2016) na kwa miaka yote minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo (2016/2017 – 2020/2021), Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikisisitiza Serikali kuleta Muswada wa Sheria Bungeni ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya nchi ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wowote unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikuwa pendekezo la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wala halikuwa ombi, bali ni sharti la kikatiba, na kazi ya Upinzani ilikuwa ni kuikumbusha Serikali kutimiza wajibu huo wa kikatiba. Lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kuisaidia Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kisheria wa utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo ili kudhibiti vikwazo vinavyoendelea kukwamisha utekelezaji wa mipango hiyo na hivyo kuifanya Serikali iweze kufikia malengo iliyokusudia kufikia wakati wa kutekeleza mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia hiyo njema ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali, Serikali hajjawahi hata mara moja kutekeleza wajibu huo wa kikatiba na ikiwa tunaingia mwaka wa kumi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi na Mitano, uliogawanywa katika vipindi vitatu vyaa miaka mitano mitano (Mpango wa Kwanza 2011/2012 - 2015/2016, Mpango wa Pili 2016/2017 – 2020/2021 na Mpango wa Tatu ambao

tunakwenda wa 2021/2022 – 2025/2026. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilieleza jinsi Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulivyoshindwa kufikia malengo yake kwa takriban asilimia 50 kutokana na kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wake ambapo mambo yalikuwa yakifanyika kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari ya kushindwa kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo kwa Miaka Mitano ni kubwa zaidi kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imeacha utamaduni wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na badala yake utashi na maelekezo ya viongozi ndiyo yanachukuliwa kama dira ya kuiongoza nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inathubutu kusema kwamba Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo umefeli kwa kuwa tunaingia mwaka wa mwisho wa utekelezaji wake ikiwa malengo yake makubwa hayajafikiwa hata robo. Lengo kuu la Mpango wa Pili lilikuwa ni kuhakikisha kwamba Tanzania inaingia katika uchumi wa kipato cha kati. Serikali iwaambie wananchi ni viashiria gani vyta uchumi wa kipato cha kati vimeanza kuonekana ikiwa ajira na fursa za kiuchumi kwa wafanyabiashara na wakulima zimebanwa na vipato vyta wananchi vimeporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lingine la Mpango wa Pili lilikuwa ni kuziimarisha Serikali za Mitaa katika kupanga na kutekeleza mipango yao. Serikali ijpime imefikia lengo hilo kwa kiwango gani ikiwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zimenyang'anywa vyanzo vyta mapato na kuzifanya kuwa omboomba kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lingine ilikuwa ni kuboresha viwango vyta maisha ya watu. Serikali ijpime imefikia lengo hilo kwa kiwango gani ikiwa wananchi wanalia ukata na ugumu wa maisha kiasi cha kushindwa kumudu gharama za milo mitatu kwa siku. Bado baadhi ya wananchi wanaishi chini ya dola moja kwa siku. Je, hayo ndiyo maisha bora kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, si nia ya Kambi Rasmi ya Upinzani kufanya tathmini ya kila lengo, isipokuwa inataka kusisitiza kwamba tunashindwa kuflikia malengo hayo kwa kuwa utekelezaji wa malengo hayo hauna mwongozo wa kisheria na pia watekelezaji wanajua kwamba hata wasipofikia malengo hayo hawawajibiki kisheria. Ndiyo maana bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwamba, kama Serikali itaendelea kupuuzia matakwa ya Katiba ya nchi ya kutaka kuwe na sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mipango yetu ya Maendeleo tutakuwa tukipanga mipango ambayo haitkelezeki na hivyo kuendelea kutumia vibaya fedha za umma kutekeleza mipango ambayo haifiki malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kutoteketeza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Hoja nyngine ya msingi ambayo imekuwa Kikwazo Kikubwa katika utekelezaji bora wa Mipango ya Maendeleo hapa nchini ni tabia sugu ya Serikali kutoteketeza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kama ilivyopitishwa na Bunge. Hii ni hoja ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiipigia kelele tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Kwanza wa Taifa wa Maendeleo mpaka kipindi hiki cha utekelezaji wa Mpango wa Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo la kubishaniwa kwamba Mpango wowote unaoweza kutekelezwa unahitaji bajeti (kwa maana ya fedha za kutekeleza mpango huo). Hata hivyo, pamoja na ukweli na uhalisia huo Serikali yetu kwa muda mrefu imekuwa ikitoa fedha pungufu ya zile zilizoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ya maendeleo inayokuwa imepangwa kwa mwaka wa fedha husika. Mbaya zaidi fedha hizo hutolewa kwa kuchelewa na hivyo kushindwa kutekeleza kazi zilizokuwa zimepangwa kwa wakati na muda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si nia yetu kutoa mifano mingi ya namna Serikali inavyofanya utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo, lakini kwa ajili ya kuipa nguvu hoja yetu hii tutatoa mifano ya miaka mitatu iliyopita kwa baadhi ya

Wizara hususan zile zinazogusa maisha ya wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara hii bilioni 100.527 lakini hadi Machi, 2017 zilikuwa zimetolewa bilioni 2.25 sawa na asilimia 2 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hii ina maana kwamba takribani asilimia 98 ya bajeti hiyo kwa mwaka huu haikutekelezwa. Mwaka 2017/2018 zilitengwa bilioni 150 lakini hadi kufikia Machi, 2018 shilingi bilioni 16.5 tu ndizo ambazo zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 11 tu ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa. Hii ina maana kwamba asilimia 89 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya kilimo ilikuwa haijatekelezwa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta ya Kilimo ni shilingi bilioni 98 lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2019 ni bilioni 41 ikiwa sawa na asilimia 42 ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa. Hii ina maana ya kwamba asilimia 58 ya bajeti ilikuwa haikutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvumi. Kwa mujibu wa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara hii iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 4 lakini fedha zilizotolewa ilikuwa ni shilingi millioni 130 tu sawa na asilimia 3.2. Hii ina maanisha kwamba asilimia 97 ya bajeti ilikuwa haijatekelezwa. Mwaka 2017/2018, Wizara hii ilitengewa tena jumla ya shilingi bilioni 4 kama fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo na uvumi lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018 hakuna hata shilingi moja ambayo ilikuwa imepokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta hizo. Hii ina maana kwamba asilimia 100 ya fedha za bajeti ya maendeleo zilikuwa hazijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Mifugo na Uvumi ilikuwa kama ifuatavyo:- Mifugo ilitengewa shilingi bilioni 5. Hadi kufikia Machi fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 2 sawa na asilimia 43, hivyo, asilimia 57 ya bajeti ilikuwa haikutekelezwa. Uvumi iliyokuwa imetengwa shilingi bilioni 7.12,

fedha iliyokuwa imetolewa ilikuwa ni shilingi bilioni 4 sawa na asilimia 56, hivyo, asilimia 43 ya bajeti ilikuwa hajatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni Wizara mbili tu kama mfano lakini ukifanya tathmini ya utoaji wa fedha za maendeleo kwa Wizara nyingine hali ni hiyo hiyo. Hakuna Wizara inayopata fedha zote za maendeleo kwa asilimia 100. Kwa mwenendo huo, hakuna muujiza wowote unaoweza kutendeka ili Mipango yetu ya Maendeleo iweze kutekelezwa kwa ufanisi ikiwa Serikali haitoi fedha zote za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya fedha nje ya Mpango wa Bajeti. Kama nilivyosema hapo awali, ili Mpango wowote wa Maendeleo uweze kutekelezwa unahitaji bajeti. Hilo halitoshi, inahitaji pia nidhamu ya matumizi ya bajeti hiyo. Kama mpango umeainisha mambo kumi ya kutekeleza na ikatengwa bajeti ya kutosha kutekeleza mambo hayo kumi kutumia fedha yote katika bajeti hiyo kwa ajili ya kutekeleza mambo mengine ambayo hayakuwa yameainishwa katika Mpango husika, huko ni kuvuruga Mpango na huko ni kukosa nidhamu ya matumizi ya bajeti iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya kutekeleza mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano mingi ya miradi iliyotekelawa nje ya mpango jambo ambalo liliathiri bajeti ya utekelezaji wa miradi ambayo ilikuwa ndani ya Mpango. Kwa mfano, ujenzi wa ukuta Mererani, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Chato, zoezi zima la kuhamia Dodoma na miradi iliyotumia fedha nyingi za umma ambazo hazikuwepo kwenye Mpango. Kwa vyovvoste vile, ipo miradi iliyokuwa kwenye mpango ambayo haikutekelezwa kutokana na fedha nyingi kutumika kugharamia miradi mingine tofauti ambayo haikuwepo katika mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji katika masuala ya fedha. Pamoja na mambo mengine yote, uwajibikaji ni sifa ya msingi kabisa inayopelekea ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wowote wa Maendeleo. Wanazuoni wa mausala ya utawala bora wanasema kwamba; naomba

kunukuu "*Accountability is the obligation of powers holders to take responsibilities for their actions*". Hii ina maana ya kwamba uwajibikaji ni ile hali ya wenyewe madaraka kutambua kwamba wamekosea na kuchukua hatua ya kuwajibika kwa makosa waliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikipigia sana kelele suala hili la uwajibikaji katika masuala ya fedha kutohana na kitendo cha Serikali kutokuonekana dhahiri iikywepa majukumu katika mchakato mzima wa usimamizi wa Mipango ya Maendeleo. Kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza na kwa miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani ilionesha jinsi Serikali ilivyokwepa uwajibikaji kwa kusimamia utekelezaji wa Mipango. Mosi, kwa kushindwa kuleta Bungeni Muswada kwa ajili ya Kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kama Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba inavyoolekeza. Pili, kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti ili kuondoa vipengele viliviyokuwa vinaibana Serikali kuwajibika katika masuala ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwamba kitendo cha Serikali kufanya marekebisho Sheria ya Bajeti ambayo inatoa mwongozo wa uwajibikaji wa kifedha na kibajeti katika kutekeleza miradi ya maendeleo ni uthibitisho tosha wa Serikali kukwepa wajibu huo. Itakumbukwa kwamba, mwaka 2018, Serikali ilileta mapendekezo ya kuvifanyia marekebisho vifungu vya 41, 53, 56, 57 na 63 vya Sheria ya Bajeti ya 2017 kwa kuondoa wajibu wa Serikali wa kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bungeni ripoti ya matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka ya mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi mitatu) ambapo sasa ripoti hiyo itakuwa ya nusu mwaka wa mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi sita).

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwaka 2018, Serikali ilileta mapendekezo ya kuvifanyia marekebisho vifungu vya 41, 53, 56, 57 na 63 vya Sheria ya Bajeti ya 2017

kwa kuondoa wajibu wa Serikali wa kuwasilisha kwa Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bungeni ripoti ya matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka ya mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi mitatu) ambapo sasa ripoti hiyo itakuwa ya nusu mwaka wa mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi sita).

Mheshimiwa Spika, naenda kipengele (c) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita. Uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita, umebaini utekelezaji wa miradi hiyo haujawahi kufikia nusu, asilimia 50 ya malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. Hii inatokana na ukweli kwamba kwa miaka mitatu mfululizo yaani 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019 fedha ya kutekeleza miradi ya maendeleo hajawahi kufikia asilimia 50 ya bajeti ya maendeleo inayokuwa imeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukifanya rejea ya Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya miaka husika, utaona kwamba, katika mwaka wa fedha 2016/2017 bajeti ya maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge ilikuwa ni shilingi trilioni 11.820. Hata hivyo, fedha iliyokuwa imetolewa na kutumika hadi kufikia Februari, 2017 ilikuwa shilingi trilioni 4.168 sawa na asilimia 35 ya bajeti yote ya maendeleo. Hii ina maana kwamba asilimia 64.7 ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa kwa mwaka huo hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, bajeti ya maendeleo iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi trilioni 11.99, lakini hadi kufikia Januari, 2018 fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi trilioni 3.608 sawa na asilimia 30.1 ya bajeti yote ya maendeleo. Hii inatoa picha kwamba; asilimia 70 ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka huo haikutolewa na kwa maana hiyo, miradi ya maendeleo kwa mwaka husika haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tofauti na miaka hiyo miwili; mwaka wa fedha 2018/2019, kulikuwa na mwamko kidogo,

ambapo kati ya shilingi triliuni 12.01 zilizokuwa zimetengwa kama bajeti ya maendeleo, shilingi triliuni 5.44 zilikuwa zimeshatolewa hadi kufikia Aprili, 2019 na kufanya bajeti ya maendeleo kwa kipindi hicho kuwa imetekelawa kwa asilimia 45.29. Hata hivyo, pamoja na ongezeko la utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho, ukweli unabaki kwamba asilimia 54.71 ya fedha za miradi ya maendeleo hazikutolewa na kwa misingi ile ile, miradi ya maendeleo haikutekelezwa kwa asilimia 54.7.

Mheshimiwa Spika, ukitafuta wastani wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa miaka husika, utagundua kwamba, bajeti ya maendeleo imekuwa ikitekelezwa kwa wastani wa asilimia 36. Tafsiri ya tarakimu hiyo, ni kwamba, wastani wa asilimia 63.2 ya fedha za miradi ya maendeleo zimekuwa hazitolewi na Serikali na kwa sababu hiyo, miradi ya maendeleo imekuwa haitekelezwi kwa wastani wa asilimia 63.2 kwa miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Spika, (d) mipango ya maendeleo haiweki kipaumbele katika sekta zenyetija kubwa katika uchumi. Ukitazama vipaumbele vya Serikali katika Mipango ya Maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita, utagundua kwamba vipaumbele hivyo hivijaweka msukumo kwenye sekta zenyetija kubwa katika uchumi kwa maana ya sekta zinazogusa maisha ya watu wengi kiuchumi na sekta zenyetija kuchechemua ukuaji wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya uelewa wa wananchi sekta zenyetija kuchochaea ukuaji wa sekta nyingine ni kama vile kilimo ambacho huchochaea ukuaji wa sekta ya viwanda kwa mfano kilimo cha miwa huchochaea ukuaji wa viwanda vya sukari; mifugo kwa viwanda vya ngozi na viwanda vya maziwa; viwanda vya kukamua mafuta vinategemea kilimo cha mazao ya mbegu za mafuta kama vile alizeti, ufuta, mawese, pamba, karanga; Viwanda vya nguo kutegemea kilimo cha pamba na Viwanda vya Sigara kutegemea kilimo cha tumbaku.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, umebaini kwamba bajeti kwa mwaka huo imejikita kwenye maendeleo ya vitu na sio maendeleo ya watu. Miradi iliyopewa kipaumbele katika mgawo huo, ni miradi ambayo haigusi moja kwa moja ustawi wa watu na pili ni miradi ambayo haichochei ukuaji wa sekta nydingine za kiuchumi ili kutanua wigo wa ajira na kuongeza kipato kwa wananchi. Kwa mfano, katika bajeti ya shilingi trilioni 33.1 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi trilioni 12.25, sawa na asilimia 37 ya bajeti yote; ikiwa shilingi trilioni 9.74 ni fedha za ndani na kiasi cha shilingi trilioni 2.51 ni fedha za nje. Mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo ambavyo umeanishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwa ajili ya kutilia nguvu hoja ya uwekezaji katika sekta au miradi yenye tija kubwa katika uchumi nitazungumzia sekta chache zenye mchango mkubwa katika uchumi, lakini zimesahauliwa katika Mipango ya Maendeleo kwa maana ya kutengewa fedha za kutosha ili kukuza sekta hizo. Baadhi ya Sekta hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo; kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Kilimo lisilo la Kiserikali *ANSAF* ni kwamba kilimo ndicho mhimilli mkuu katika uchumi wa nchi yetu. Taarifa hiyo inaeleza kuwa, Sekta hiyo inachangia takriban asilimia 25.3 ya Pato la Taifa na 30% ya mauzo nje ya nchi na 65% ya malighafi zinazotumika katika viwanda vyetu. Aidha, sekta hiyo inatoa ajira kwa 65.5% ya Watanzania, ambao kati ya nguvu kazi hiyo, 53% ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaendelea kuonesha kuwa asilimia 80 ya Watanzania maskini wanaendesha maisha yao kwa kutegemea sekta hii ya kilimo. Hivyo basi huu ni ukweli wa wazi kwamba Serikali bado hajjaweka mkazo stahiki katika kuhakikisha sekta hii ya kilimo inaboresha uchumi wa Tanzania. Hii inadhihirishwa na uhalisia wa kudidimia kwa sekta hii kadiri miaka inavyokwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Taifa (NBS) pamoja na Wizara ya Kilimo zinaonesha kuwa tangu 2014 hadi 2016 ukuaji wa kilimo ulikuwa unashuka kutoka 3.4% kwa mwaka 2014 hadi 2.3% mwaka 2015. Kufikia Disemba ukuaji uliongezeka hadi kufikia 3.1 kwa kulinganisha na 1.7% kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2016. Ukuaji ambao ni chini ya lengo la Malabo ambalo nchi yetu ilishaini mkataba huo wa 6%.

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali Azimio la Malabo la kuhakikisha kwamba Sekta ya Kilimo inakuwa kwa asilimia sita kila mwaka, azimio hilo lilitaka nchi washirika kuhakikisha pia wanatenga asilimia 10 katika bajeti za nchi zao kwenda kwenye kilimo. Hata hivyo tangu kuitishwa kwa azimio hilo, Tanzania haijawahi hata mara moja kufikia kiwango hicho cha bajeti lakini vile vile lengo la asilimia sita la ukuaji.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huo wa utengaji bajeti finyu katika sekta ya kilimo, unatoa taswira hasi kwamba, itakuwa vigumu sana kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na pia kuwa ya uchumi wa kati. Utengaji na utolewaji wa fedha ndio jambo pekee litakaloweza kuibadilisha sekta hiyo na hivyo kuigeuza Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo Barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Inakadiriwa kuwa zaidi ya 50% ya Watanzania hutegemea mifugo kama sehemu au vipato vyao vyote. Sekta ya mifugo huchangia katika kufikia njozi za maendeleo ya Taifa ya 2025, kwa kuongeza kipato, fursa za ajira na afya ya jamii. Sekta ya mifugo ni mhimili wa ukuaji wa uchumi nchini Tanzania ambako 50% ya kaya hutegemea aina fulani ya mifugo kama chanzo cha sehemu au kipato chao chote.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Kilimo lisilo la Kiserikali - ANSAF ni kwamba mchango wa sekta hii kwa pato la Taifa ni kati ya 7.4% hadi 10%, ingawa kuna uwezekano wa fursa nyingi zaidi. Licha ya mchango huo

mkubwa katika uchumi wa Taifa, uwekezaji katika sekta hii umekuwa hauridhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ukitazama utekelezaji wa bajeti za maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita katika sekta hii utagundua kuwa sekta hii haipewi kipaumbele na Serikali na tulishatoa mifano kwa kila mwaka husika na inaweza ikasomwa hivyo katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo la Taifa limeshindwa kusimamia mkakati wa kufufua viwanda nchini. Kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano ni kwamba, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) ndilo lilipewa jukumu la kuongoza nchi kuelekea Uchumi wa Viwanda. Kwa sababu hiyo, *NDC* inatakiwa kuongezewa uwezo ili iweze kuainisha, kukuza na kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati ya viwanda ili peke yake au kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali itakuwa inapitisha fedha zake za maendeleo ya viwanda kwenye shirika hilo au kulidhamini liweze kukopa kama chombo kilichopewa dhamana ya kuliongoza Taifa katika mkakati wake wa maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni miaka minne sasa imepita katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kazi zilizofanywa na *NDC* hadi sasa kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa viwanda. Katika kutekeleza wajibu huo, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa pia kujua ni viwanda vingapi ambavyo *NDC* imesimamia ujenzi wake na viwanda hivyo vimezalisha ajira kiasi gani kwa Watanzania kama liliyuo lengo la Mpango na kama Taifa tumefikia asilimia ngapi ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelazimika kuhoji uwajibikaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) kwa kuwa imebainika kuwa kuna miradi ya kimkakati

ya maendeleo ya viwanda katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ambayo ilikuwa imewekewa ukomo wa muda wa utekelezaji. Miradi hiyo hajatekelezwa mpaka sasa licha ya ukomo wa muda kumalizika na licha ya shirika kuwepo na kuendelea kupokea fedha za serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo ya viwanda. Miongoni mwa miradi hiyo, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bagamoyo - SEZ ulitakiwa kuanza ujenzi wa bandari Januari, 2017 na kumalizika 2020, ukanda wa viwanda mwambao wa bandari ilitakiwa viwanda kumi viwe vinafanyakazi 2020 na katika hilo ajira zilizotarajiwaa kwa kipindi hicho cha 2020 ni ajira 20,000.

Mheshimiwa Spika, imebaki takriban miezi miwilli kufikia mwaka 2020 Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ujenzi wa viwanda kumi katika mwambao wa eneo la kimkakati la kiuchumi la Bagamoyo umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kurasini *Logistics Centre* ambaao tayari ulipanga uwe umekalimika mwaka 2018, lakini mpaka sasa haupo na ulikuwa unatarajia kuajiri watu 25,000.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kufua Chuma Liganga; mradi huu uliwekewa ukomo kukamilika mwaka 2018/2019 ambaao umeshapita lakini mpaka sasa haupo.

Mheshimiwa Spika, upo pia mradi wa Mkujju *Uranium* ambaao kwa mujibu wa mpango ulitakiwa kujengwa toka mwaka 2016 na pia ultarajiwaa kuzalisha ajira za uhakika 4,000 na wakati wa ujenzi ajira hizo zingeongezeka hadi kufikia 15,000.

Mheshimiwa Spika, Shirika letu la *STAMICO* na lenyewe tumeshalianishia humo ndani na kueleza. Kwa hiyo naomba niende katika mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kama hitimisho.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iheshimu na itekeleze matakwa ya ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Nchi yanayoitaka kuleta Muswada wa Sheria Bungeni kwa ajili ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Serikali ijijengee utamaduni na nidhamu ya kutekeleza bajeti za maendeleo kwa ukamilifu kama zinavyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iache tabia ya kutumia fedha nje ya bajeti (*Reallocation of Budget*) iliyoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ambayo haijaainishwa kwenye mpango wa Maendeleo huko ni kuuvuruga mpango.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali iweke kipaumbele katika miradi au sekta zinazogusa maisha ya watu wengi na zenye kuchochlea ukuaji wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ijenge na kuwezesha mazingira rafiki ya kisiasa (*fair and friendly political situation*) ili kudumisha amani ya nchi na hivyo kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali ikubali kuupokea na kuufanya kazi mfumo mpya wa uchumi wa Soko Jamii ambao unaipa nafasi sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa uchumi tofauti na ilivyo sasa ambapo uchumi unahodhiwa na kuendeshwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba hotuba yetu yenye kurasa 56 iinge katika *hansard* yako.

Mheshimiwa Spika, baada ya maeneo hayo naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU
MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA
KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 94(5) (a) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya na uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Bunge tukiwa salama.

2. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Mkutano huu wa Bunge unafanyaika mwezi Novemba 2019, kipindi ambacho tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pia; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kuzungumzia mambo manne kuhusu uchaguzi huo:-

i. Kwanza, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawapongeza wananchi wote waliotumia haki yao ya kikatiba; na kujitokeza kujianandikisha ili kushiriki katika uchaguzi wa viongozi wanaowataka.

ii. Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawahimiza wananchi wote waliojiantikisha kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura tarehe 24 Novemba, 2019 na kupiga kura.

iii. Tatu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wasimamizi wa Uchaguzi huo, kusimamia kwa haki zoezi la upigaji kura, uhesabuji kura na kumtangaza mshindi halali kwa mujibu wa matokeo halisi ya kura zilizopigwa.

iv. Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawakumbusha wananchi; kuwachagua viongozi watakaojinadi kwa sera madhubuti zitakazowanasua kwenye vifungo vya umasikini uliokithiri (umaskini ambao mwananchi hana uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku; hana nyumba

ya kuishi na wala hana nguo za kuva). Wawachague viongozi wenye sera zitakazowaondoa kwenye vifungo na giza la kupata na kusambaza habari kwa uhuru; wawachague viongozi watakaopigania haki na uhuru wao wa kukusanyika na kufanya mikutano ya hadhara kwa mujibu wa katiba ya nchi; wawachague viongozi watakaopaza sauti ili huduma bora za jamii kama vile maji safi, elimu na afya ziweze kumfikia kila mwananchi kwa utoshelevu na pia wawachague viongozi watakaowatetea dhidi ya vitisho, uonevu, unyanyasaji, na matukio mengine ya kigaidi kama vila utekaji na mauaji yanavyofanywa na vikundi vya watu '*wasiojulikana*'

3. Mheshimiwa Spika, huu ni Mkuutano wa 17 wa Bunge ambao umeangukia katika kipindi cha mwezi Oktoba – Novemba; na kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; Bunge hilli linakaa kama Kamati ya Mipango ili kujadili na kuishauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata (yani 2020/2021).

4. Mheshimiwa Spika, wakati dhima ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) ni Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochaea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu; tunaingia mwaka wa tano na wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa Taifa, hali ya uchumi na maendeleo ya watu katika kaya hapa nchini ikiwa ni mbaya zaidi kuliko awamu zote nne za Serikali zilizotangulia.

5. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni ya mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 -2020/21); Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itafanya mapitio mafupi ya hoja za msingi ilizozibua katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita na ambazo hazijafanyiwa kazi mpaka sasa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani itafanya uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya

Maendeleo kwa miaka mitatu ili kuona kama kuna uhalisia kati ya kile Serikali inachokihubiri kwamba imepata mafanikio makubwa au kuna hadithi tofauti. Tatu Kambi Rasmi ya Upinzani itafanya mapitio ya Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kutoa maoni na mapendekezo yake kwa ajili ya utekelezaji bora wa Mpango huo.

B. MAPITIO YA HOJA MBALIMBALI ZILIZOIBULIWA NA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI AMBAZO MPAKA SASA HAZIJAFANYIWA KAZI

6. **Mheshimiwa Spika**, yapo mambo kadhaa ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali hii kwa miaka minne mfululizo sasa; ambayo yangesaidia kutekeleza Mipango yetu ya Maendeleo kwa ufanisi; lakini Serikali imegoma kuyafanya kazi. Mambo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

i. **Kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo:-**

7. **Mheshimiwa Spika**, tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12-2015/16); na kwa miaka yote minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo 2016/17 – 2020/2021; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiisisitiza Serikali kuleta Muswada wa Sheria Bungeni ili kukidhi matakwa ya ibara ya 63(3) (c) ya Katiba ya Nchi ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wowote unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano.

8. **Mheshimiwa Spika**, hili halikuwa pendekezo la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wala halikuwa ombi; bali ni sharti la kikatiba; na kazi ya Upinzani ilikuwa ni kuikumbusha Serikali kutimiza wajibu huo wa kikatiba. Na lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kuisaidia Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kisheria wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ili kudhibiti vikwazo vinavyoweza kukwamisha utekelezaji wa mipango hiyo na hivyo kuifanya Serikali iweze kufikia malengo iliyokusudia kuyafikia katika mipango hiyo.

- 9.** **Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia hiyo njema ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali, Serikali hajjawahi hata mara moja kutekeleza wajibu huo wa kikatiba; ikiwa tunaingia mwaka wa kumi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi na Mitano, uliogawanywa katika vipindi vitatu vya miaka mitano mitano (yaani mpango wa kwanza 2011/12 -2015/16; mpango wa pili 2016/17 – 2020/21 na mpango wa tatu 2021/22 – 2025/26).
- 10.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilieleza jinsi Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) ulivyoshindwa kufikia malengo yake kwa takriban asilimia 50, kutokana na kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wake ambapo mambo yalikuwa yakifanyika kiholela.
- 11.** **Mheshimiwa Spika**, hatari ya kushindwa kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2016/17 – 2020/21) ni kubwa zaidi kwa kuwa Serikali hii ya awamu ya tano imeacha utamaduni wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, na badala yake utashi na maelekezo ya viongozi; na hasa kiongozi mmoja; ndio yanachukuliwa kama dira ya kuiongoza nchi.
- 12.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inathhubutu kusema kwamba; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo umefeli kwa kuwa tunaingia mwaka wa mwisho wa utekelezaji wake ikiwa malengo yake makubwa hayajafikiwa kwa hata robo. Lengo kuu la Mpango wa Pili lilikuwa ni kuhakikisha kwamba Tanzania inaingia katika uchumi wa kipato cha kati. Serikali iwaambie wananchi, ni viashiria gani vya uchumi wa kipato cha kati vimeanza kuonekana ikiwa ajira na fursa za kiuchumi kwa wafanyabiashara na wakulima zimebanwa na vipato kwa wananchi vimeporomoka?
- 13.** **Mheshimiwa Spika**, lengo jingine la Mpango wa Pili lilikuwa kuziimarisha Serikali za Mitaa katika kupanga na kutekeleza mipango yao. Serikali ijipime imefikia lengo hilo kwa kiwango gani ikiwa imezifilisi mamlaka za Serikali za Mitaa

kwa kuzinyang'anya vyanzo vya mapato na kuzifanya kuwa ombaomba kwa Serikali Kuu? Lengo jingine lilikuwa ni kuboresha viwango vya maisha ya watu. Serikali ijipime imefikia lengo hilo kwa kiwango gani ikiwa kila mwananchi analia ukata na ugumu wa maisha kiasi cha kushindwa kumudu gharama za milo mitatu kwa siku. Bado wapo wananchi wanaoishi chini ya dola moja kwa siku!! Je, hayo ndio maisha bora kwa watanzania?

14. Mheshimiwa Spika, si nia ya Kambi Rasmi ya Upinzani kufanya tathmini ya kila lengo, isipokuwa inataka kusisitiza kwamba tunashindwa kufikia malengo hayo kwa kuwa utekelezaji wa malengo hayo hauna mwongozo wa kisheria; na pia watekelezaji wanajua kwamba hata wasipofikia hayo malengo hawawajibiki kisheria. Ndio maana bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwamba; kama Serikali itaendelea kupuuzia matakwa ya Katiba ya Nchi ya kutaka kuwe na sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mipango yetu ya Maendeleo; tutakuwa tukipanga mipango ambayo haitekelezeki na hivyo kuendelea kutumia vibaya fedha za umma kutekeleza mipango ambayo haifiki malengo yake.

ii. Kutotekeliza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

15. Mheshimiwa Spika, hoja nyagine ya msingi ambayo imekuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji bora wa Mipango ya Maendeleo hapa nchini ni tabia sugu ya Serikali ya kutotekeliza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kama ilivyopitishwa na Bunge. Hii ni hoja ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiipigia kelele tangu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo mpaka kipindi hiki cha utekelezaji wa Mpango wa Pili.

16. Mheshimiwa Spika, si jambo la kubishaniwa kwamba; ili Mpango wowote uweze kutekelezwa unahitaji bajeti (kwa maana ya fedha za kuutekeleza mpango huo). Hata hivyo, pamoja na ukweli na uhalisia huo; Serikali yetu kwa muda mrefu, imekuwa ikitoa fedha pungufu ya zile zilizoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ya maendeleo inayokuwa imepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha husika. Mbaya zaidi fedha hizo hutolewa kwa kuchelewa na hivyo

kushindwa kutekeleza kazi zilizokuwa zimepangwa kwa wakati au muda husika.

17. Mheshimiwa Spika, si nia yetu kutoa mifano mingi ya namna Serikali inavyofanya utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo; lakini kwa ajili ya kuipa nguvu hoja hii tutatoa mifano ya miaka mitatu iliyopita kwa baadhi ya Wizara hususan zile zinazogusa maisha ya wananchi wengi zaidi:-

(a) Wizara ya Kilimo:-

- Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 100.527 lakini hadi Machi, 2017 zilitolewa shilingi bilioni 2.252 sawa na asilimia 2.22 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hii ina maana kwamba takribani asilimia 98 ya bajeti hiyo haikutekelezwa.
- Katika mwaka wa fedha 2017/18; Wizara hii iliidhinishiwa na Bunge fedha za maendeleo jumla ya shilingi bilioni 150.253 (**150,253,000,000/-**) lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018; ni shilingi bilioni 16.5 tu (**16,520,540,444/-**) zilikuwa zimetolewa ikiwa ni sawa na **asilimia 11 tu** ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa. Hii ina maana kwamba asilimia 89 ya bajeti ya maendeleo katika sekta ya kilimo haikutekelezwa.
- Katika mwaka wa fedha 2018/19, fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta ya Kilimo ni shilingi **bilioni 98.119**, lakini fedha iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2019 ilikuwa ni shilingi **bilioni 41.222** ikiwa ni asilimia 42 ya bajeti iliyoidhinishwa. Hii ina maana asilimia 58 ya bajeti ya maendeleo haikuekelezwa.

(b) Wizara ya Mifugo na Uvuvi:

- Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 4 lakini zilizotolewa ni shilingi milioni 130 tu sawa na asilimia 3.25 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Hii ina maana kwamba takribani asilimia 97 ya bajeti hiyo haikutekelezwa.

- Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Wizara hii iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 4 (**4,000,000,000/=**) kama fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo na uvuvi; lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018 hakuna hata shilingi moja ambayo ilikuwa imepokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta hizo. Hii ina maana pia kwamba asilimia 100 ya bajeti ya maendeleo katika sekta za mifugo na uvuvi ilikuwa ni hewa!
- Katika mwaka wa fedha 2018/19; bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikuwa kama ifuatavyo:-
 - **Mifugo:** Fedha iliyotengwa ilikuwa shilingi bilioni 5. Iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2019 ilikuwa shilingi bilioni 2.173 sawa na asilimia 43. Hivyo, asilimia 57 ya bajeti hiyo haikutekelezwa.
 - **Uvuvi:** Fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 7.126, iliyotolewa ni shilingi bilioni 4.012 sawa na asilimia 56.3. Kwa hiyo, asilimia 43.7 ya bajeti hiyo haikutolewa.

18. Mheshimiwa Spika, Hizi ni Wizara mbili tu kama mfano. Lakini ukifanya tathmini ya utoaji wa fedha za maendeleo kwa Wizara nyingine hali ni hiyo hiyo. Hakuna Wizara inayopata fedha zote za maendeleo kwa asilimia 100. Kwa mwenendo huo, hakuna muujiza wowote unaweza kutendeka ili Mpango yetu ya Maendeleo iweze kutekelezwa kwa ufanisi, ikiwa Serikali haitoi fedha zote za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

iii. Matumizi ya Fedha nje ya Mpango wa Bajeti (Budget Reallocation):-

19. Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, ili mpango wowote wa maendeleo uweze kutekelezwa unahitaji bajeti; lakini hilo halitoshi; inahitajika pia nidhamu ya matumizi ya bajeti hiyo. Kama mpango umeainisha mambo kumi ya kutekeleza na ikatengwa bajeti ya kutosha kutekeleza mambo hayo kumi; kutumia fedha yoyote katika bajeti hiyo kwa ajili ya kutekeleza mambo mengine ambayo hayakuwa yameainishwa katika Mpango husika; huko ni

kuuvuruga Mpango; na huko ni kukosa nidhamu ya matumizi ya bajeti iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya kuutekeleza mpango husika.

20. Mheshimiwa Spika, hali kama hiyo inapotokea; inakuwa vigumu sana kufikia malengo ya Mpango uliokusudiwa kwa kuwa unakuwa umeshavurugwa tayari kwa kuingiza mambo mengine ambayo hayakuwepo awali.

21. Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi ya miradi iliyotekelawa nje ya Mpango jambo ambalo liliathiri bajeti ya utekelezaji wa miradi ambayo ilikuwa ndani ya Mpango. Kwa mfano, ujenzi wa ukuta kuzunguka migodi ya madini ya Tanzanite – Mererani; ujenzi wa Uwanja wa Ndege Chato; Zoezi zima la Serikali kuhamia Dodoma na kadhalika ni miradi iliyotumia fedha nyingi za umma ambazo hazikuwa kwenye Mpango wa Bajeti. Kwa vyovypote vile, ipo miradi iliyokuwa kwenye Mpango ambayo haikutekeleza kutokana na fedha nyingi kutumika kugharamia miradi ambayo haikuwa kwenye Mpango.

iv. Uwajibikaji katika Masuala ya Fedha

22. Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine yote, uwajibikaji ni sifa ya msingi kabisa inayopelekea ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wowote wa Maendeleo. Wanazuoni wa mausala ya utawala bora wanasema kwamba; naomba kunukuu "*Accountability is the obligation of power holders to take responsibility for their actions*". Hii maana yake ni kwamba, uwajibikaji ni ile hali ya wenye madaraka kutambua kwamba wamekosea na kuchukua hatua ya kuwajibika kwa makosa waliyoyafanya.

23. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikipigia sana kelele suala hili la uwajibikaji katika masuala ya fedha kutokana na kitendo cha Serikali kuonekana dhahiri ikikwepa kuwajibika katika mchakato mzima wa usimamizi wa Mpango ya Maendeleo.

24. Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo na kwa miaka yote

minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili; Kambi Rasmi ya Upinzani ilionyesha jinsi Serikali inavyokwepa uwajibikaji katika kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo; Mosi, kwa kushindwa kuleta Muswada Bungeni kwa ajili ya Kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kama Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba inavyoolekeza; lakini pili, kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti ili kuondoa vipengele vilivyokuwa vinaibana Serikali kuwajibika katika masuala ya fedha.

25. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwamba; *kitendo cha Serikali kuifanya marekebisho sheria ya bajeti ambayo inatoa mwongozo wa uwajibikaji wa kifedha/kibajeti (financial accountability) katika kutekeleza miradi ya maendeleo ni uthibitisho tosha wa Serikali kukwepa uwajibikaji.*

26. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwaka 2018, Serikali ilileta mapendekezo ya kuvifanya marekebisho vifungu vya 41, 53, 56, 57 na 63 vya Sheria ya Bajeti ya 2017 kwa kuondoa wajibu wa Serikali wa kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Bungeni ripoti ya matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka ya mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi mitatu) ambapo sasa ripoti hiyo itakuwa ya nusu mwaka wa mzunguko wa bajeti (yaani kila baada ya miezi sita).

27. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwamba; athari za marekebisho hayo ya sheria ya bajeti ilikuwa ni kudumaza ufuatiliaji thabiti (tight follow-up) wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali; na jambo hilo linaweza kupelekea utekelezaji mbovu wa bajeti kutokana na matumizi yasiyofaa au hata ubadhirifu wa fedha za umma. Sababu ya kueleza hivyo ilitokana na ukweli kwamba; ikiwa ripoti ya matumizi ya Serikali itatolewa kwa kila nusu mwaka wa utekelezaji wa bajeti, maana yake ni kwamba, ripoti hiyo itatoka wakati mchakato wa maandalizi ya mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata ukiwa umeshaanza. Kwa hiyo, ripoti hiyo inakuwa haisaidii katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa

fedha unaoendelea (current financial year) ili hatimaye kuweza kufanya makisio na maoteo ya bajeti inayofuata.

28. Mheshimiwa Spika, Kwa minajili ya kuwa na tija katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo; Kambi Rasmi ya Upinzani ilishauri na kupendekeza kwamba; Serikali ilete Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bajeti ili kurejesha vile vifungu vilivyokuwa vinaelekeza ripoti za matumizi ya fedha ziwe zinaletwa kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka). Kwa kufanya hivyo, kwanza kutakuwa na ufuatilaji madhubuti wa matumizi ya Serikali, lakini pia ripoti za robo mwaka, zitawezesha kufanya tathmini ya mwenendo wa utekelezaji wa bajeti na hivyo kuisadia Serikali kujipanga vizuri zaidi kwa bajeti zinazofuata”.

29. Mheshimiwa Spika, mpaka dakika hii ninapozungumza jambo hilo halijafanyiwa kazi; na mambo yanaendeleakama kawaida (business as usual). Kwa mtindo huo, hatuwezi kufanikiwa. Katika kusisitiza umuhimu wa uwajibikaji; aliyejewa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Koffi Annan aliwahi kusema katika Taarifa ya Africa Progress Report ya 2013 kwamba; “*Success will require leadership, transparency, and accountability, too. There is no substitute for public scrutiny in developing effective and equitable policies*”. Hii ina maana kwamba; mafanikio yanahitaji uongozi, uwazi na uwajibikaji pia. Haiwezekani kuwa na sera nzuri au mipango mizuri inayotekelzeza kama hakuna uwajibikaji kwa umma. Hivyo basi, Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi lina wajibu wa msingi tena wa kikatiba; wa kuwawajibisha wale wote wanaokwenda kinyume na Mipango ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

C. UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MIAKA MITATU ILIYOPITA

30. Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita umebaini kwamba; utekelezaji wa miradi hiyo haujawahi kufikia asilimia 50 (nusu) ya malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. Hii inatokana na

ukweli kwamba; kwa miaka mitatu mfululizo (yaani 2016/17; 2017/18 na 2018/19) fedha ya kutekeleza miradi ya maendeleo haijawahi kufikia asilimia 50 ya bajeti ya maendeleo inayokuwa imedhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

31. Mheshimiwa Spika, ukifanya rejea ya Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya miaka husika, utaona kwamba, katika mwaka wa fedha 2016/17 bajeti ya maendeleo iliyokuwa imedhinishwa na Bunge ilikuwa ni **shilingi trillioni 11.820**. Hata hivyo, fedha iliyokuwa imetolewa na kutumika hadi kufikia Februari, 2017 ilikuwa **shilingi trillioni 4.168** sawa na **asilimia 35.26** ya bajeti yote ya maendeleo. Hii ina maana kwamba asilimia 64.7 ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa kwa mwaka huo hazikutolewa. Tafsiri yake ni kwamba, miradi ya maendeleo kwa mwaka husika haikutekelezwa kwa asilimia 64.7.

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/18, bajeti ya maendeleo iliyokuwa imedhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi trillioni 11.999, lakini hadi kufikia Januari, 2018 fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi trillioni 3.608 sawa na asilimia 30.1 ya bajeti yote ya maendeleo. Hii inatoa picha kwamba; asilimia 70 ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka huo haikutolewa na kwa maana hiyo, miradi ya maendeleo kwa mwaka husika haikutekelezwa.

33. Mheshimiwa Spika, tofauti na miaka hiyo miwili; mwaka wa fedha 2018/19 kulikuwa na mwamko kidogo, ambapo kati ya shilingi trillioni 12.01 zilizokuwa zimetengwa kama bajeti ya maendeleo, shilingi trillioni 5.44 zilikuwa zimeshatolewa hadi kufikia Aprili, 2019; na hivyo kufanya bajeti ya maendeleo kwa kipindi hicho kuwa imetekelezwa kwa asilimia 45.29. Hata hivyo, pamoja na ongezeko la utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho, ukweli unabaki kwamba asilimia 54.71 ya fedha za miradi ya maendeleo hazikutolewa na kwa misingi ile ile, miradi ya maendeleo haikutekelezwa kwa asilimia 54.71.

34. Mheshimiwa Spika, ukitafuta wastani wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa miaka husika, utagundua kwamba, bajeti ya maendeleo imekuwa ikitekelezwa kwa wastani wa asilimia 36.8. Tafsiri ya tarakimu hiyo, ni kwamba, wastani wa asilimia 63.2 ya fedha za miradi ya maendeleo zimekuwa hazitolewi na Serikali; na kwa sababu hiyo, miradi ya maendeleo imekuwa haitekelezwi kwa wastani wa asilimia 63.2 kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita.

D. MIPANGO YA MAENDELEO HAIWEKI KIPAUMBELE KATIKA SEKTA ZENYE TIJA KUBWA KATIKA UCHUMI (MULTIPLIER EFFECT)

35. Mheshimiwa Spika, ukitazama vipaumbele vya Serikali katika Mipango ya Maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita, utagundua kwamba vipaumbele hivyo hivijaweka msukumo kwenye sekta zenye tija kubwa katika uchumi (kwa maana ya sekta zinazogusa maisha ya watu wengi kiuchumi na sekta zenye kuchechemua ukuaji wa sekta nyingine).

36. Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya uelewa wa wananchi; sekta zenye kuchochea ukuaji wa sekta nyingine ni kama vile kilimo ambacho huchochea ukuaji wa sekta ya viwanda; kwa mfano: Kilimo cha miwa huchochea ukuaji wa viwanda vya sukari, mifugo kwa viwanda vya ngozi, na viwanda vya maziwa, viwanda vya kukamua mafuta vinategemea kilimo cha mazao ya mbegu za mafuta kama vile Alizeti, Ufuta, Mawese, Pamba, Karanga, n.k. Viwanda vya nguo kutegemea kilimo cha Pamba, Viwanda vya Sigara kutegemea kilimo cha Tumbaku n.k.

37. Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 umebaini kwamba; bajeti kwa mwaka huo imejikita kwenye maendeleo ya vitu na sio maendeleo ya watu. Miradi iliyopewa kipaumbele katika mgawo huo, ni miradi ambayo haigusi moja kwa moja ustawi wa watu, na pili ni miradi ambayo haichochei ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi ili kutanua wigo wa ajira na kuongeza kipato kwa wananchi. Kwa mfano; katika bajeti ya shilingi triliioni 33.104; kwa mwaka wa fedha 2019/2020; fedha za maendeleo zilikuwa ni shilingi triliioni 12.25 sawa na asilimia 37

ya bajeti yote; ikiwa shilingi trillioni 9.74 ni fedha za ndani na kiasi cha shilingi trillioni 2.51ni fedha za nje.

38. Mheshimiwa Spika, mgawo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. shilingi trillioni 2.48 sawa na asilimia 20.245 ya bajeti yote ya maendeleo ni kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Reli kwa kiwango cha Kimataifa (SGR)
- ii. shilingi trillioni 1.44 sawa na asilimia 11.755 ya bajeti yote ya maendeleo ni kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme katika Mto Rufiji (Stiegler's Gorge Hydro Power Project) na
- iii. shilingi bilioni 500 sawa na asilimia 4.081 ya bajeti yote ya maendeleo ni kwa ajili ya kumalizia malipo kwa ajili ya ununuzi wa Ndege za Serikali.

39. Mheshimiwa Spika, miradi hiyo mitatu imechukua shilingi trillioni 4.42 ambayo ni sawa na asilimia 36.081 ya fedha zote za maendeleo. Hii miradi ipo kwenye Wizara mbili tu, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Nishati. Pamoja na miradi hiyo michache kuchukua sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo; bado miradi hiyo haina faida za moja kwa moja katika uchumi wa nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kwamba malighafi inayotumika kujenga SGR (Chuma na cement) karibu zote zinatoka nje ya nchi na hivyo fedha zinaondoka katika mzunguko wa ndani na kupelekwa nje kwa ajili ya ununuzi wa malighafi hizo. Aidha, ajira zinazozalishwa haziingizi chochote kwenye bajeti yetu kama kodi ya mshahara (PAYE) kwa kuwa wengi walioajiriwa katika mradi huo ni vibarua (casual labourers) ambao hawapo kwenye mfumo wa kodi. Kwa maneno mengine, hii ni miradi ambayo inanyonya uchumi wetu kwa kutoa fedha ndani na kuzipeleka nje; lakini pili haina multiplier effect katika kuchechemua au kuchochaea sekta nyingine za kiuchumi kama vile biashara na ajira.

40. Mheshimiwa Spika, Kutokana na bajeti hii kuweka kipaumbele katika maendeleo ya vitu badala ya maendeleo

ya watu; sekta nyingine zinazogusa maisha ya watu moja kwa moja zimepata mgawo mdogo sana wa fedha za maendeleo jambo linaloashiria kwamba Serikali hii haina mpango na maendeleo na ustawi wa watu kama ilivyojinasibu katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwamba ina Mpango wa kuboresha Maisha ya Watu. Hata hivyo, miradi na sekta ambazo Serikali inasema ndiyo vipaumbele vyake, nayo imepata mgawo mdogo jambo ambalo linaleta mkanganyiko kuhusu vipaumbele vyakaa Serikali. Mgawo wa fedha kwenye sekta hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ndiyo kipaumbele cha kwanza katika bajeti ya 2019/2020 Wizara hii, imetengewa shilingi bilioni 51.5 sawa na asilimia 0.42 ya bajeti nzima ya maendeleo.
- ii. Wizara ya Kilimo imetengewa shilingi bilioni 134.577 sawa na asilimia 1.098 ya bajeti ya yote maendeleo.
- iii. Wizara ya Elimu imepewa shilingi bilioni 863 ambayo ni sawa na asilimia 7.045 ya bajeti nzima ya maendeleo;
- iv. Afya imepewa shilingi bilioni 544.137 sawa na asilimia 4.44 ya bajeti yote ya maendeleo;
- v. Maji yamepewa shilingi bilioni 610.5 sawa na asilimia 4.98 ya fedha zote za maendeleo.

41. Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo huo wa mgawo wa fedha za maendeleo, ni dhahiri shahiri kwamba Serikali hii inayojinasibu kuwa ni ya wanyonge; haipendi wanyonge hao waishi kwa neema kwa kupata huduma bora za kijamii kama vile afya, elimu, maji safi na salama, au kuwekeza katika kilimo chao kinachowapatia ajira na chakula; isipokuwa inawekeza katika vitu ambayo hao wanyonge hawatakuwa na uwezo wa kuvitumia pia.

42. Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kutilia nguvu hoja ya uwekezaji katika sekta au miradi yenye tija kubwa katika uchumi nitazungumzia sekta chache zenye mchango

mkubwa katika uchumi lakini zimesahauliwa katika Mipango ya Maendeleo kwa maana ya kutengewa fedha za kutosha ili kuzikuza sekta hizo. Baadhi ya Sekta hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Sekta ya Kilimo

43. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Kilimo lisilo la Kiserikali – ANSAF¹ ni kwamba; kilimo ndicho mhimili mkuu katika uchumi wa nchi yetu. Taarifa hiyo inaeleza kuwa, Sekta hiyo inachangia takriban asilimia 25.3 ya Pato la Taifa (GDP), 30% ya mauzo nje ya nchi na 65% ya malighafi zinazotumika katika viwanda vyetu. Aidha sekta hiyo inatoa ajira kwa 65.5% ya Watanzania, ambao kati ya nguvu kazi hiyo, 53% ni wanawake.

44. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaendelea kuonesha kuwa asilimia 80 ya watanzania masikini wanaendesha maisha yao kwa kutegemea sekta hii ya kilimo. Hivyo basi huu ni ukweli wa wazi kwamba Serikali bado hajjaweka mkazo stahiki katika kuhakikisha sekta hii ya kilimo inaboresha uchumi wa Tanzania. Hii inadhihirishwa na uhalisia wa kudidimia kwa sekta hii kadiri miaka inavyokwenda mbele.

45. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Takwimu za NBS pamoja na Wizara ya Kilimo zinaonesha kuwa tangu 2014 hadi 2016 ukuaji wa kilimo ulikuwa unashuka kutoka 3.4% kwa mwaka 2014 hadi 2.3% mwaka 2015, kufikia disemba 2017 ukuaji uliongezeka hadi kufikia 3.1% kwa kulinganisha na 1.7% kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2016. Ukuaji ambao ni chini ya lengo la Malabo/CAADP² la 6%.

46. Mheshimiwa Spika, Ukiachilia mbali Azimio la Malabo la kuhakikisha kwamba Sekta ya Kilimo inakuwa kwa asilimia 6 kila mwaka; azimio hilo lilizitaka nchi washirika kuhakikisha pia wanatenga asilimia 10 katika bajeti za nchi zao kwenda kwenye Kilimo. Hata hivyo; tangu kuitishwa kwa azimio hilo, Tanzania hajjawahi hata mara moja kufikia kiwango hicho cha bajeti.

¹ ANSAF = Agricultural Non- State Actors Forum

² CAADP = Comprehensive Africa Agricultural Development Programme

- 47. Mheshimiwa Spika**, mwenendo huo wa utengaji bajeti finyu katika sekta ya kilimo, unatoa taswira hasi kwamba, itakuwa vigumu sana kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na pia kuwa ya uchumi wa kati. Utengaji na utolewaji wa fedha ndio jambo pekee litakaloweza kuibadilisha sekta hiyo na hiyvo kuigeuza Tanzania kuwa nchi yenyе uchumi wa viwanda.
- 48. Mheshimiwa Spika**, sambamba na bajeti pia takwimu zinatuonesha kuwa mikopo inayotolewa kwa sekta ya kilimo nayo imekuwa ikipungua kwa mfano kwa mwaka 2013 mikopo kwenye sekta ya kilimo ilikuwa ni 8.7%, 7.7% kwa mwaka 2015, na 6.9% kwa mwaka 2017.
- 49. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa viashiria vya ukuaji wa uchumi (economic performance indicators) ni kwamba ikiwa kilimo kitakuwa kwa wastani wa asilimia 6 kwa mwaka, kama makubaliano ya Malabo yanavyoolekeza; basi uchumi-jumla wa nchi unaweza kukua kwa kiwango cha kati ya asilimia 8 – 10 kwa mwaka; na mwenendo huo ndio unaoweza kuifanya Tanzania kufikia ndoto yake ya kuwa na uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Kinyume cha hapo lengo hilo la kufikia uchumi wa kati haliwezi kufikiwa. Kitendo cha Serikali yetu kwenda kinyume na makubaliano ya Malabo ya kutenga asilimia 10 ya Bajeti ya Taifa kwenda kwenye kilimo, kumezia kilimo chetu kukua kwa asilimia 6 kama ilivyotarajiwa na matokeo yake tumezia asilimia 30 ya vijana kupata ajira katika mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo (agricultural value chain) kama ilivyokusudiwa; na kwa sababu hiyo, tumezia uchumi-jumla wa nchi (Total National Economy) kukua kwa asilimia 8- 10 kama ilivyotarajiwa.

- 50.** Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa msisitizo kwa Serikali, kwamba Mpango wowote wa Maendeleo ambao hauweki kipaumbele katika Kilimo; mpango huo hauwezi kustawisha maisha ya watu, lakini pili mpango huo unaweza kudumaza ukuaji wa uchumi-jumla katika taifa.

ii. Sekta ya Mifugo

51. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo Barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Inakadiriwa kuwa zaidi ya 50% ya Watanzania hutegemea mifugo kama sehemu au vipato vyao vyote. Sekta ya mifugo huchangia katika kufikia njozi za maendeleo ya taifa ya 2025, kwa kuongeza kipato, fursa za ajira na afya ya jamii. Sekta ya mifugo ni mhimili wa ukuaji wa uchumi nchini Tanzania ambako asilimia 50 ya kaya hutegemea aina fulani ya mifugo kama chanzo cha sehemu au kipato chao chote.

52. Mheshimiwa Spika, Sekta ya mifugo inakua na kubadilika kwa haraka sana wakati huo huo mahitaji ya chakula na malighafi yatokanayo na mifugo ikiongezeka maradufu kunakochangiwa na ongezeko la idadi ya watu wa kipato cha kati pamoja na ukuaji wa miji. Uwezo na mchango wa sekta ya mifugo katika kufikia malengo ya maendeleo ni kiashiria cha fursa ya kipekee katika kuleta mabadiliko makubwa katika uchumi.

53. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Kilimo lisilo la Kiserikali la ANSAF ni kwamba; mchango wa sekta hii kwa pato la taifa ni kati ya 7.4% hadi 10%, ingawa kuna uwezekano wa fursa nyingi zaidi. Licha ya mchango huo mkubwa katika uchumi wa Taifa, uwekezaji katika sekta hii umekuwa hauridhishi hata kidogo.

54. Mheshimiwa Spika, ukitazama utekelezaji wa bajeti za maendeleo kwa miaka mitatu iliyopita katika sekta hii utagundua kuwa sekta hii haipewi kipaumbele na Serikali. Kwa mfano; mwaka wa fedha 2016/17 Wizara ya Mifugo na Uvuvi illidhinishiwa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 4 lakini zilizotolewa ni shilingi milioni 130 tu sawa na asilimia 3.25 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Hii ina maana kwamba takribani asilimia 97 ya bajeti hiyo haikutekelezwa. Halikadhalika, mwaka wa fedha 2017/18 Wizara hii ilitengewa shilingi bilioni 4 kama fedha za maendeleo lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2018 hakuna hata shilingi moja iliyokuwa imetolewa. Tafsiri ya jambo hili ni kwamba, asilimia 100 ya

bajeti ya maendeleo katika sekta za mifugo na uvuvi hazikutekelezwa.

55. Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, mwaka wa fedha 2018/19; bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Mifugo na Uvubi haikutekelezwa kwa ukamilifu wake. Kwa mfano kwa sekta ya mifugo, fedha iliyotengwa ilikuwa shilingi bilioni 5. Iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2019 ilikuwa shilingi bilioni 2.173 sawa na asilimia 43. Hivyo, asilimia 57 ya bajeti hiyo haikutekelezwa. Aidha, katika Sekta ya Uvubi, fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 7.126, iliyotolewa ni shilingi bilioni 4.012 sawa na asilimia 56.3. Kwa hiyo, asilimia 43.7 ya bajeti hiyo haikutolewa.

56. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa angalizo kwa Serikali kwamba; kama ina nia ya dhati ya kuuboresha uchumi wa nchi yetu kuwa wa kipato cha kati kufikia 2025, haina budi kuwekeza kwa wingi katika sekta zinazogusa maisha ya watu wengi kwa maana ya fursa za ajira, biashara na uzalishaji wa viwandani (manufacturing) na pia kwenye sekta zinazochochea ukuaji wa sekta nyingine kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi. Uwekezaji huo unatakiwa uonekane kwenye kutenga bajeti ya kutosha ya maendeleo katika sekta hizo na kutekeleza bajeti hiyo kwa ukamilifu.

E. SHIRIKA LA MAENDELEO LA TAIFA LIMESHINDWA KUSIMAMIA MKAKATI WA KUFUFUA VIWANDA NCHINI

57. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni kwamba, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ndilo lilipewa jukumu la kuongoza nchi kuelekea Uchumi wa Viwanda. Kwa sababu hiyo, NDC inatakiwa kuongezewa uwezo ili iweze kuainisha, kukuza na kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo ya viwanda ikiwa peke yake au kwa kushirikiana na sekta binafsi.

58. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali itakuwa inapitisha fedha zake za maendeleo ya viwanda kwenye Shirika hilo au kulidhamini liweze kukopa kama chombo kilichopewa dhamana ya kuliongoza taifa katika Mkakati wake wa Maendeleo ya Viwanda.

59. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni miaka minne sasa imepita katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kazi zilizofanywa na NDC hadi sasa katika kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa viwanda. Katika kutekeleza wajibu huo, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa pia kujua ni viwanda vingapi ambavyo NDC imesimamia ujenzi wake; na viwanda hivyo vimezalisha ajira kiasi gani kwa Watanzania kama liliivo lengo la Mpango; na kama Taifa tumefikia asilimia ngapi ya kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kat.

60. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelazimika kuhoji uwajibikaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kwa kuwa imebainika kuwa kuna miradi ya kimkakati ya maendeleo ya viwanda katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ambayo illkuwa imewekewa ukomo wa muda wa utekelezaji. Miradi hiyo hajatekelezwa mpaka sasa licha ya ukomo wa muda kumalizika na licha ya Shirika kuwepo na kuendelea kupokea fedha za Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo ya viwanda.

61. Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa miradi hiyo, ni kama ifuatavyo:-

i. **Mradi wa Bagamoyo - SEZ** ultakiwa kuanza ujenzi wa bandari Januari 2017 na kumalizika 2020, ukanda wa viwanda mwambao wa bandari ilitakiwa viwanda kumi (10) viwe vinafanyakazi 2020, na katika hilo ajira zilizotarajiwa kwa kipindi hicho cha 2020 ni ajira 20,000.

62. Mheshimiwa Spika, imebaki takriban miezi miwili kufikia mwaka 2020; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili; ujenzi wa viwanda kumi katika mwambao wa Eneo la Kimkakati la Kiuchumi la Bagamoyo umefikia wapi?

ii. **Mradi wa Kurasini Logistics Centre**

63. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, akiwasilisha Bungeni makadirio ya

mapato na matumizi ya fedha ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni kwamba, fedha ambazo tayari Serikali imeishazitoa kama fidia kwa wananchi waliokuwa wanamiliki maeneo hayo ya Kurasini kupitia NDC ni shilini 1 bilioni 101 na kaya zilizolipwa ni kaya 1,019.

64. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni kuwa mradi ulitakiwa kuwa umekamilika na kufanya kazi ifikapo Juni, 2018. Aidha, ilikadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2020; viwanda takribani 20 vya ndani vitakuwa vinauza bidhaa zake mahali hapo, ikiwa ni pamoja na ajira za moja kwa moja zipatazo 25,000 na ajira zisizo za moja kwa moja zipatazo 100,000 zitakazokuwa zimezalishwa kwa kipindi hicho.

65. Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 uliokuwa umepangwa kwa mradi huo kukamilika na kufanya kazi ulishapita, na mwaka 2020 uliokuwa umepangwa kwa ajira 25,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 100,000 kuzalishwa ni kama vile umeshafika kwa kuwa imebaki takriban miezi miwili tu kufikiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa pia Serikali ilieleze Bunge hili kuwa matarajio hayo yaliyokuwa yameainishwa katika Mpango wa Maendeleo yamefikiwa kwa kiwango gani.

iii. Mradi wa Kufua Chuma Liganga:-

66. Mheshimiwa Spika, mradi huu ultarajiwa kuwanufaisha wananchi 4000 kwa kutoa ajira za uhakika, na mradi ultarajiwa kuwa ungekuwa unafanyakazi kufikia mwaka wa fedha 2018/2019. Mradi huu uligemewa kuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja za chuma kwa mwaka.

67. Mheshimiwa Spika, ukomo wa muda uliowekwa kukamilika kwa mradi (yaani 2018/19) umeshapita. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali pia, kulieleza Bunge hili kuhusu maendeleo ya mradi huo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kueleza hali halisi na maendeleo ya mradi wa Kabanga Nickel, ambao ulitakiwa kuwa umekamilika ifikapo mwaka 2020.

68. Mheshimiwa Spika, upo pia mradi wa Mkusu Uranium ambao kwa mujibu wa Mpango ultakiwa kujengwa toka mwaka 2016 na pia ultarajiwa kuzalisha ajira za uhakika 4,000 wakati wa ujenzi ajira hizo zingeongezeka hadi kufikia 15,000 wakati mradi ungekuwa umekamilika. Hizi ni ajira nyingi kwa Watanzania, na hivyo ni jambo jema kama Serikali italieleza Bunge hili mradi huo uko katika hatua gani na ajira hizo zimezalishwa kwa kiasi gani hadi sasa.

69. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, mpango unaeleza changamoto katika sekta hii ndogo kuwa ni zana za kisasa za uvuvi, kutokuwepo na viwanda vyatia kuongeza thamani kwa bidhaa za uvuvi pamoja na soko. Matarajio katika kuondokana na changamoto hizo ifikapo mwaka 2020 ni kuimarisha masoko, kuongeza uzalishaji wa samaki wa kati ya tani 10,000 hadi 50,000 kwa mwaka. Pia katika kipindi hicho uvuvi utatoa ajira 15,000 kwa mwaka. Aldha, kwa kipindi hiki Meli za uvuvi 5 zilitakiwa kununuliwa.

70. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili; malengo ya kuzalisha tani 10,000 hadi 50,000 za samaki kwa mwaka; malengo ya kuzalisha ajira 15,000 katika sekta ya uvuvi na malengo ya kununua Meli tano za Uvuvi yamefikiwa kwa kiwango gani?

F. SHIRIKA LA TAIFA LA UCHIMBAJI WA MADINI (STAMICO) LIMESHINDWA KUISAIDIA NCHI KUPATA FAIDA KUTOKA KWENYE SEKTA YA MADINI

71. Mheshimiwa Spika, STAMICO ni moja kati ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini. Hili ni shirika linalomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja, ambalo lilianzishwa rasmi mwaka 1972 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (1969). Mwaka 2015 Shirika lilitanyiwa marekebisho makubwa ya kimuundo (restructuring) chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (mabadiliko ya uanzishwaji wa mashirika ya Umma) 2015.

72. Mheshimiwa Spika, STAMICO inamiliki makampuni kadhaa ya madini yakiwemo STAMIGOLD, Buhemba Gold, Makaa ya Mawe Kiwira n.k, kwa lengo la kuyaendesha kifaifa. Pia STAMICO imeingia ubia na Kampuni Tanzaniteone Mining Limited (TML) katika uchimbaji wa Tanzanite kule Mererani.

73. Mheshimiwa Spika, katika ubia wa uchimbaji Tanzanite, STAMICO imejikuta ikipata hasara kubwa kutokana na sababu mbalimbali kama zilivyobainishwa na katika taarifa ya Kamati Maalum ya Spika (Tanzanite), kama ifutavyo:-

Jedwali: Muhtasari wa hasara za ubia kati ya STAMICO na TML

Na.	MA ELEZO	KIASI
KIASI (TZS)		
1	Kutotekeleza kifungu cha 8(3) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 tangu sheria hiyo ilipoanza kutumika mwaka 2010 hadi mwaka 2013 kwa wakati kulisababisha hasara ya Shilingi 37,004,666,631.225/=	37,004,666,631.22
2	Shilingi 18,037,977,356/= ambazo ni makadirio yaliyofanywa na TRA ya kodi ya mapato na kodi nyingine kwa mwaka 2009 hadi 2013 ambazo hazikulipwa kutokana kampuni ya TML kupewa leseni ya ubia na STAMICO bila hati safi ya kodi (tax clearance).	18,037,977,356
3	Dola za kimarekeni 1,507,000/= sawa na Shilingi 3,350,061,000.00 ambazo ni deni la mrabaha ililiainishwa katika letter of intent wakati wa majadiliano ya Mkataba na halijalipwa hadi sasa.	3,350,061,000.00
4	Shilingi 11,696,748,875/= ni faida ambayo STAMICO wameikosa kuanzia mwaka 2013 hadi 2017 kutokana na Mkataba kuweka mfumo wa kukokotoa faida kwa kutumia mfumo wa faida mabaki (net residual profit) badala ya faida halisi (net profit).	11,696,748,875.00
5	Shilingi 16,920,115,297/= ni makadirio yaliyofanywa na TRA ya kodi ya mapato na kodi nyingine ambazo hajjalipwa kwa mwaka 2014 hadi 2017 kwa kisngizio kuwa kampuni ya TML haipatifaifa.	16,920,115,297.00
6	Shilingi 1,478,438,499.84/= ni bakaa ya mrabaha ambaa haujalipwa tangu 2013 hadi 2016.	1,478,438,499.84
7	Shilingi 65,847,831/= zinazotokana na utekelizaji mbovu wa Mkataba	65,847,831.00
8	Dola za kimarekeni 1,522,735.58/= sawa na Shilingi 3,385,041,194.34 zinazotokana na utekelizaji mbovu wa Mkataba	3,385,041,194.34
9	Tani 2 kilo 373 na gramu 9 za madini ya tanzanite yaliyozalishwa katika Kitalu C na kutoroshwa ambayo thamani yake haifahamiki.	-
10	Kiasi kisichofahamika cha kodi iliyokwepwa kutokana na kampuni ya Urafiki Gemstone EPZ Limited, TsavoriteOne Limited na Tanzanite Laboratory Limited kuuzwa kwa pamoja na kampuni ya TML.	-
JUMLA YA HASARA		91,938,896,684.40

Chanzo: Ukokotozi Kutokana na Takwimu na Taarifa Mbalimbali zilizopatikana kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA), Wizara ya Nishati na Madini na STAMICO.

74. Mheshimiwa Spika, hasara kama hii inatokea pia kwenye kampuni tanzu za STAMICO. Hii inatokana na changamoto zinazoikabili STAMICO ambazo ni uhaba wa rasilimali fedha zinazohitajika kuendesha shirika. Kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG 2019) STAMIGOLD kampuni tanzu ya STAMICO, imekuwa inajientesha kwa hasara takribani miaka 3 iliyopita kutohuna na madeni, uwekezaji mdogo na kampuni kutofanya shughuli za uzalishaji. Vivyo hivyo, Kifungu namba 9 cha Marekebisho ya Sheria ya Madini 2010, kupitia Sheria ya Marekebisho Anuai Sheria Na. 7, 2017, Sheria inaelekeza umiliki wa Serikali usiopungua asilimia 16 katika makampuni ya madini, ingawa, sheria au kanuni hazitoi mwongozo kuhusu mamlaka ipi ya Serikali itahusika na jukumu la kusimamia umiliki huo.

75. Mheshimiwa Spika, ni vyema pia tukakubaliana kuwa uchimbaji mkubwa unahitaji mtaji mkubwa na kwa hali halisi ya nchi yetu kutegemea kuwa Serikali iweke mtaji STAMICO ili shirika liweze kuwa shindani katika soko ni kujidanyanya wenyewe, na jambo hilo halitoweza kuwa na uhalisia katika hali ya uchumi wa nchi yetu ulivyo.

76. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuungana na mapendekezo ya wadau wa madini na wanaoitakia mema nchi yetu katika sekta hii ya madini na wanaotambua umuhimu wa STAMICO katika maendeleo ya rasilimali madini nchini, walipendekeza kama ifuatavyo:-

i. STAMICO ifanyiwe mabadiliko makubwa ya kimuundo na kimfumo ili iwe kampuni hodhi (Holding company) inayoweza kumiliki hisa au sehemu ya umiliki katika makampuni mengine ya migodi na pia iweze kukuza mtaji kwa kuingia makubaliano ya kimkakati na ya kiuwekezaji, ikiwezekana, kukopa na hata kukaribisha wadau (hasa wananchi) wenyewe nia ya kuwekeza katika vipaumbele vya Shirika. Aidha, iwapo kama STAMICO itabadiishwa na kuwa kampuni hodhi, itasaidia kukuza mtaji wake kwa haraka, pia itamwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali kufanya ukaguzi (katika Mashirika ya Umma na Makampuni Binafsi (kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia) na hatimaye kuweza kujiridhisha na

mwenendo wa mapato na matumizi ya makampuni hayo ambayo kwa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali hana uwezo wa kuyakagua kwa mujibu wa sheria.

ii. STAMICO ifanyiwe mabadiliko na ipewe jukumu la kusimamia na kuratibu umiliki wa asilimia 16 za Serikali katika makampuni ya madini kwa niaba ya Serikali.

iii. STAMICO ijitanue na kufanya utafiti na uwekezaji katika aina tofauti za madini kama vile "graphite", coal" na mengineyo kuliko kujielekeza zaidi katika dhahabu.

77. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kama STAMICO itaendelea kufanyakazi kwa muundo wa sasa ni dhahiri itakuwa ni taasisi inayofilisi nchi kwa kupoteza fedha za walipa kodi bila yenyewe kuzalisha, kwani itakuwa inazalisha hasara miaka yote. Kwa muktadha huo sekta yetu ya madini kuwanufaisha Watanzania itakuwa ni ndoto.

G. MAANDALIZI YA CHAGUZI ZA SERIKALI ZA MITAA 2019 NA UCHAGUZI MKUU 2020

▪ Madai ya Tume Huru ya Uchaguzi

78. Mheshimiwa Spika, ili Mipango ya Maendeleo katika Nchi iweze kutekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa ni lazima kuwe na mazingira rafiki ya kisiasa katika nchi. Kwa sababu hiyo, maridhiano katika michakato ya kisiasa, chaguzi huru na za haki, kuheshimiana na kuvumilliana kisiasa ni tunu na nyenzo muhimu za kudumisha amani na utulivu katika taifa. Matokeo ya mambo hayo, ni utulivu wa ndani mionganoni mwa wananchi ambaao huwafanya waweze kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo ni sehemu ya utekelezaji wa Mipango ya Taifa ya Maendeleo.

79. Hitaji la Tume Huru ya Uchaguzi ni kilio cha muda mrefu cha Taifa tangu mfumo wa vyama vingi urejeshwe mwaka 1992 na hoja hii imeletwa Bungeni kila mwaka kwa njia mbalimbali. Ni msingi wa haki, amani, demokrasia na maendeleo endelevu. Ni bahati mbaya sana kwamba, bado Serikali ya CCM imeendelea kupuuza jambo hili na kuendelea

kuwa na Tume ambayo muundo na weledi wake unapalilia na kutengeneza bomu litakalovuruga sana nchi yetu siku si nydingi hatua za makusudi zisipochukuliwa.

80. Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali utawala wa sheria, kujali na kutetea haki za binadamu ambayo ni miongoni mwa misingi mikuu ya demokrasia, sifa nydingine kuu ya demokrasia duniani ni chaguzi huru na za haki. Chaguzi huru na za haki ndizo zinazodhihirisha mamlaka ya wananchi katika kuamua namna wanavyotaka utawala wa nchi yao uwe. Kwa maneno mengine, chaguzi huru na za haki ndizo kitambulisho halisi cha demokrasia ya kweli.

81. Mheshimiwa Spika, mamlaka yoyote inayopatikana kwa njia nydingine bila kupitia chaguzi huru na za haki; mamlaka hiyo haiwezi kuwa ya kidemokrasia. Kwa vyovyote vile, mamlaka hiyo itakuwa ni ya ki-imla (udikteta) yenye kujali na kusimamia maslahi ya wachache na sio maslahi ya wananchi au maslahi ya taifa.

82. Mheshimiwa Spika, ili chaguzi ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa – ya kuweka uongozi au mamlaka halali inayokubalika na wananchi walio wengi, ni lazima chaguzi hizo ziratibiwe na chombo kinachoaminika na pande zote zinazoshiriki katika chaguzi hizo; chombo ambacho ni huru kisichoegemea upande wowote ili kujenga muafaka wa kitaifa na mustakabali mwema wa nchi. Chombo hicho si kingine bali ni Tume Huru ya Uchaguzi.

83. Mheshimiwa Spika, yapo mazingira mengi yanayodhihirisha kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi tuliyonayo sasa haiko huru na kwa sababu hiyo haina uwezo wa kuendesha chaguzi huru na za haki ndio maana tunadai Tume Huru kabla ya kuingia kwenye chaguzi. Kwa mfano Ibara ya 74(14) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema kwamba:-

"Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kuijunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kwamba kila mmoja wao atakuwa na haki ya kupiga kura

iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya katiba hii." Aidha Ibara ya 74(15) inasema kwamba:-

"kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (14) watu wanaohusika na uchaguzi ni; - (e) Wasimamizi wote wa Uchaguzi katika miji na wilaya zote."

84. Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, ambapo wakurugenzi walioeteuliwa na Mhe. Rais ni makada walioshindwa katika kura za maoni ndani ya CCM na wengine ni wale walioshindwa kwenye uchaguzi kupitia CCM; kuwapa dhamana watu hao ambao ni wanachama wa CCM kusimamia uchaguzi kunakwenda kinyume kabisa na matakwa ya ibara ya 74(14) inayopiga marufuku wasimamizi wa uchaguzi kuwa wanachama wa chama cha siasa. Tunazungumza jambo hili tukijua kuwa Serikali ilikata rufaa na kushinda dhidi ya uamuzi wa mahakama wa kuwazuia Wakurugenzi wa Halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi na kwamba imeshinda katika rufaa hiyo.

85. Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama hayo, Tume ya Uchaguzi haiwezi kujidai kwamba iko huru kwa kuwa maafisa wake wana mafungamano na chama cha siasa – CCM. Kwa mfano kisa cha Jaji Augustine Ramadhani, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kujitosa kwenye kinyang'anyiro cha Urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia CCM kinatoa picha ya wazi kwamba alikuwa mwanachama wa CCM wakati akiwa kiongozi mkuu wa Tume ya Uchaguzi. Hatua ya Jaji Ramadhani kujingiza kwenye siasa mara baada ya kustaafu kupitia chama kilichoko Ikulu, ni ushahidi tosha kuwa NEC na ZEC siyo vyombo huru na hivyo haviwezi kutenda haki katika chaguzi; lakini mbaya zaidi vinatenda kazi kinyume na Katiba.

86. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2010, kwenye kifungu cha 7(1) kinasema kuwa *"kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika chini ya usimamizi wa sheria hii, wasimamizi wa uchaguzi ni Wakurugenzi wa Jiji, Wakurugenzi wa Manispaa, Wakurugenzi wa Miji na Wakurugenzi*

Watendaji wa Wilaya." Kifungu cha 7(2) kinasema kuwa, "Na Tume yenye pia inaweza kuteua idadi ya maafisa wengine kuwa wasimamizi wa uchaguzi au wasaidizi wa usimamizi wa uchaguzi."

87. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hiyo ya uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi katika Wilaya au Majimbo ni Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, Miji na Majiji na katika ngazi za Kata wasimamizi wa uchaguzi ni Watendaji wa Kata na watendaji hawa wote ni watumishi wa Serikali na hivyo ni wateule wa Rais au Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambao kwa sasa Rais ndiye mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, hivyo Wakurugenzi wote na watendaji wa kata wako chini yake.

88. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya Uchaguzi ni kwamba wajumbe wote wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa, Mtendaji wake Mkuu na Maafisa wengine wote wa Tume hiyo huteuliwa na Rais wa nchi na hakika wote ni waajiriwa wa Serikali ya Chama Tawala. Kwa mantiki hiyo Rais anaweza kumuondoa katika madaraka mjumbe yejote wa Tume ya Uchaguzi akipenda kufanya hivyo wakati wowote. Na tukumbuke kwamba katika mchakato wa uchaguzi Rais naye anakuwa na maslahi kwa kuwa naye ni mgombea mtarajiwa.

89. Mheshimiwa Spika, kwa kuliona hili la mapungufu ya Tume ya Uchaguzi yanayosababisha uchaguzi kutokuwa huru na haki, Tume ya Jaji Nyalali kwenye taarifa yake, katika Ibara ya 592 ilisema kwamba, "*Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi sharti wachaguliwe na Bunge au Baraza la Wawakilishi.... Wakurugenzi wa Uchaguzi ambao watakuwa ni Makatibu wa Tume ya Uchaguzi nao sharti wachaguliwe na Bunge au Baraza la Wawakilishi baada ya kupendekezwa na Tume za Ajira zinazohusika.*"

90. Mheshimiwa Spika, sambamba na msisitizo huo wa Tume ya Jaji Nyalali, mwaka 1999 iliundwa Kamati nyingine ya kuratibu maoni kuhusu Katiba iliyoongozwa na Mheshimiwa

Jaji Robert Kisanga. Nayo Tume ya Jaji Kisanga ilisema yafuatayo:

"Muundo wa Tume ya Uchaguzi hauzingatii uwakilishi wa vyama vya siasa na kwamba Wajumbe wa Tume huteuliwa na Rais ambaye pia anaweza kuwa ni kiongozi wa chama cha siasa kinachotawala. Kwa sababu hiyo, Wajumbe wa Tume katika utendaji kazi wao ama watakuwa na upendeleo kwa chama husika au watakuwa wanalipa fadhila kwake. Wanaotoa hoja hii wanapendekeza kwamba kuwe na ama uwakilishi wa vyama vya siasa, ama kuwe na chombo kitakachochuja majina ya Wajumbe wa Tume kabla Rais hajawateua".

91. Mheshimiwa Spika, Rasimu ya Pili ya Katiba pamoja na Katiba Pendekewza kwenye ibara za 190 na 211 kwa mfuatano huo, zinaongelea kuhusu kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi, na jinsi Tume hiyo itakavyopatikana. Huo ni ushahidi mwagine kwamba Tume ya Uchaguzi iliyopo ina mapungufu makubwa na inaweza kuwa ndio chanzo cha kuliingiza Taifa kwenye machafuko ya kisiasa.

92. Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi ni chombo cha kufanya maamuzi. Vyombo hivi, kama ilivyo mahakama, huundwa kwa namna ambayo huaminiwa na wadau kuwa viko huru na haviwezi kuwa na upendeleo. Kwa hiyo kigezo cha kwanza na cha msingi ni namna gani UTEUZI wao unafanyika. Mchakato wa uteuzi unatakiwa uwe huru na wa haki, wa wazi na ulio shirkishi.

93. Mheshimiwa Spika, haiwezekani Mwenyekiti na Mtendaji wake Mkuu kuteuliwa kisirisiri na mtu mmoja tu na ambaye naye ni mgombea mtarajiwa, na chama chake kina wagombea kwa chaguzingazi zote, halafu Tume ikatangaza kuwa yenewe ni Tume Huru na kwamba haiingiliwi na mamlaka yoyote.

94. Mheshimiwa Spika, kigezo kingine cha Tume Huru ni uhuru wa rasilimali fedha ilionayo Tume husika. Tume ambayo kila mara inaomba fedha za kutekeleza majukumu yake kwa

mamlaka ambayo Tume inatakiwa iisimamie katika mchakato wa uchaguzi, ni dhahiri jambo hilo linaondoa uhuru wa Tume.

95. Mheshimiwa Spika, Tume Huru ni lazima iwe na Mfuko wake wa fedha ili iweze kuwa uhuru wa kifedha (financial independence) na kwamba haipigi magoti kwa yeoyote kuomba fedha. Hiki nacho ni kigezo muhimu cha uhuru wa Tume. Kinyume na hapo uhuru wa Tume unakuwa umewekwa rehani na hivyo haki kwa vyama shindani haiwezi kutendeka. Aidha, ni muhimu kwamba Tume ya Uchaguzi ikawa na wafanyakazi wake yenye we wa kutosha na ikawa wanawajibika kwa Tume na wala sio Mamlaka nyingine, kusimamia shughuli za uchaguzi.

96. Mheshimiwa Spika, kwa ushahidi uliooneshwa hapo awali ni kwamba kuna umuhimu mkubwa hasa katika mfumo huu wa vyama vingi nya siasa kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi ili kuziba uwezekano wowote ambao unaweza kuitumbukiza nchi yetu katika machafuko yatokanayo na kutoridhishwa na mwenendo wa mchakato wa chaguzi.

97. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya awali kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Tanzania Oktoba 2015, iliyotolewa na timu ya uangalizi wa uchaguzi ya TEMCO pamoja na ushauri mwingine ilisema kwamba;

".... Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kusimamia chaguzi za Jamhuri ya Muungano. Wajumbe wa Tume huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na wanatekeleza majukumu yao kama inavyoelekezwa katika sheria za uchaguzi. Baadhi ya wadau wa uchaguzi hawaridhishwi na sheria zinazotawala chaguzi Tanzania. Kuna hisia na mashaka kuwa sheria ina upungufu, mkubwa zaidi ikiwa:

i. Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina mamlaka ya kutosha ya kutekeleza majukumu yake bila upendeleo. Mashaka haya yanatokana na ukweli kuwa Mwenyekiti wa Tume, Makamu wake, Makamishna na Mkurugenzi wa Uchaguzi huteuliwa na Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa chama cha siasa na

wakati mwingine mgombea katika nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano;

ii. Tume haina wafanyakazi na maafisa wake mahsus i ukiacha wale walioko makao makuu Dar es Salaam. Inategemea kiasi kikubwa wafanyakazi wa Serikali ambao huwepo kwa ridhaa ya Rais. Utii wa wafanyakazi hawa uko kwa mwajiri wao na sio Tume”

98. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ibara ya (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaitaja Tanzania kuwa ni nchi ya kidemokrasia, na yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa; na kwa kuwa misingi ya demokrasia – na hasa demokrasia ya vyama vingi vya siasa ni pamoja na chaguzi zilizo huru na haki; na kwa kuwa chaguzi huru na za haki zinategemea sana umadhubuti na uhuru wa Tume za Uchaguzi zinazosimamia chaguzi hizo; na kwa kuwa historia inaonyesha kwamba pale ambapo haki haikutendeka katika chaguzi katika nchi mbalimbali duniani; nchi hizo zilikumbwa na machafuko ya kisiasa jambo lilirosababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe na hivyo kuleta madhara makubwa katika nchi hizo; na kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Tanzania inaonekana kushindwa kutenda haki katika chaguzi ilizosimamia kutoekana na Tume hiyo kukosa uhuru wa kimamlaka na kifedha³; na kwa kuwa matukio ya uhalifu wa kiuchaguzi (election fraud) hapa nchini yanazidi kuongezeka - ambapo imeshuhudiwa mgombea fulani anashinda uchaguzi lakini anatangazwa aliyeshindwa; au matokeo ya uchaguzi kutangazwa wakati bado kura zinahesabiwa; mambo ambayo yanayojenga hasira na uhasama baina ya wananchi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi; na kwa kuwa Ibara ya 74(12) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema kwamba: “*Hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lilitendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza*

³Tume ya Taifa ya Uchaguzi inateuliwa na Rais hivyo inawajibika kwake (haina mamlaka kamili) pia haina mfuko wa fedha – inategemea kupewa fedha na Serkali Kuu kutekeleza majukumu yake (financial dependence).

madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii; na kwa kuwa amani na utulivu wa nchi yetu vipo katika hatari ya kusambaratika kutokana uhalifu wa kiuchaguzi kuendelea kufanyika chini ya usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyopo sasa – rejea hali ya kisiasa Zanzibar baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2015 na madonda ya chaguzi za marudio za Udiwani na Ubunge Tanzania Bara – Taifa limegawanyika!!; na kwa kuwa chombo kinachotakiwa kusimamia mchakato mzima wa uchaguzi kinatakiwa kiwe huru na kinachoaminika na wananchi pamoja na vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki chaguzi; HIVYO BASI, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali ilelete Bungeni haraka iwezekanavyo, na kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2020; Muswada wa Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na marekebisho yake ambapo pamoja na mambo mengine itawezesha:

- i. Kuunda Tume Huru ya Uchaguzi (Tanzania Independent Electoral Commission – TIEC) itakayoondoa mamlaka ya Rais ya kumteua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe wengine au Wakurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na badala yake Wajumbe hao wa Tume wateuliwe kwa utaratibu mwingine maalum utakaowekwa kwa mujibu wa sheria hiyo.
- ii. kuanzisha Mfuko wa Fedha wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (Tanzania Independent Electoral Commission Fund), jambo litakalohakikisha uwepo wa fedha za kuendesha shughuli za uchaguzi nchini wakati wote bila kutegemea huruma ya Serikali Kuu kifedha na rasilimali watu.
- iii. kuondoa katazo la kuishtaki, au kupinga uamuzi wa Tume Mahakamani kuhusu uendeshaji wa uchaguzi

▪ **Maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

99. Mheshimiwa Spika, madai ya Tume Huru ya Uchaguzi yanakwenda sambamba na mahitaji ya lazima na ya haraka ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Hii ni kwa sababu uchaguzi ni takwimu na takwimu hizo zinatokana na

idadi ya wapiga kura walioandikishwa. Kasoro yoyote itakayotokea katika uandikishaji au utunzaji wa kumbukumbu za wapiga kura inakuwa na madhara makubwa katika matokeo ya uchaguzi mzima.

100. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba eneo hili la maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ndilo eneo lilitolalamiwi sana na vyama vyaisa; hususan vyai upinzani ambavyo kwa miaka mingi vimekuwa wahanga wakubwa wa udanganyifu na wizi wa kura unaofanywa na CCM chini ya uratibu wa Serikali ya chama hicho na vyombo vyake.

101. Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba zoezi la uboreshaji wa daftari la wapiga kura limeshaanza; lakini zoezi hilo linaendeshwa kimya kimya; hakuna uhamasishaji unaofanywa na vyama vyaisa ambavyo ndio wadau wakubwa wa uchaguzi jambo ambalo linaleta mashaka makubwa juu ya ufanisi wa zoezi hilo.

102. Mheshimiwa Spika, hakuna asiyefahamu jinsi zoezi la uandikishaji wa wapiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa 2015 liliyogubikwa na changamoto nyingi zikiwemo mashine za uandikishaji kushindwa kufanya kazi kutokana na matatizo ya kiufundi; wafanyakazi wa Tume kushindwa kutumia mashine kutokana na kutokuwa na mafunzo ya namna ya kuzitumia, mashine za uandikishaji kuwa chache, siku za uandikishaji kuwa chache – mambo ambayo yalisababisha idadi kubwa ya wapiga kura kushindwa kuandikishwa. Safari hii hakuna taarifa kwa umma juu ya changamoto zinazokabili zoezi la uboreshaji la sasa ambapo kuna wasiwasi kwamba pengine changamoto za sasa ni nyingi na kubwa kuliko za mwaka 2015 na kwa sababu hiyo kuna uwezekano wananchi wengi zaidi wenye sifa za kupiga kura wakaachwa kuandikishwa katika daftari la wapiga kura.

103. Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Serikali Mosi, kuruhusu vyama vyaisa kufanya uhamasishaji wa wananchi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura; Pili kutoa taarifa kwa umma juu ya mwenendo wa uandikishaji ikiwa ni pamoja

na kutoa idadi ya watu walioandikishwa katika kila mkao, na pia kutoa taarifa za changamoto zinazolikabili zoezi hilo mpaka sasa.

104. Mheshimiwa Spika, ilikuwa pia ni rai ya Kambi ya Upinzani kuitaka Serikali kueleza ni lini Watanzania ambao watakuwa wameandikishwa kwenye Daftari la Wapiga Kura watapata fursa ya kuhakiki Daftari la Wapiga Kura kwa mujibu wa sheria na zoezi hili litachukua muda gani. Aidha, kuna maandalizi gani kuwezesha wafungwa na mahabusu walioko magerezani kushiriki kujandidikisha na kupiga kura iliyo haki yao ya Kikatiba? Kwa muktadha huohuo, kuna maandalizi gani kuwezesha Watanzania walioko nje ya nchi na wenye sifa kujandidikisha na hatimaye kupiga kura?

105. Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa; yalikuwa ni madai ya siku nyingi ya vyama vyta upinzani kwamba uchaguzi huo usisimamiwe na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na badala yake usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Na sababu ya kutaka iwe hivyo, ni kutohana na kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina maslahi katika uchaguzi huo na kwa maana hiyo haitatenda haki kwa wadau wengine wa uchaguzi.

106. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI iko chini ya Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi. Mfumo mzima wa uchaguzi ndani ya CCM uko chini yake moja kwa moja. Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini – ambao ni waratibu na wasimamizi wa chaguzi hizo ni wateuliwa wa Rais na bila shaka ni wana-CCM kwa kuwa haitegemewi Rais kuteua timu inayompinga kufanya nayo kazi. Aidha, upo ushahidi wa wazi kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri ni makada wa CCM wakiwemo walioshindwa katika kura za maoni na kupewa zawadi ya Ukurugenzi; na wana maelekezo ya Rais kuwa wasiwatangaze wagombea wa upinzani hata kama wameshinda katika chaguzi. Rais alinukuliwa akisema “Mkurugenzi atakayemtangaza Mpinzani wakati amepewa nyenzo zote za utendaji atakuwa hana kazi.” Kwa sura hiyo; Ofisi yake haiwezi kuendesha kwa haki uchaguzi wa Serikali

za Mitaa ambao unajumuisha vyama vingi. Na hii sababu yake ni rahisi – yeye ni mwamuzi na ni mchezaji kwa wakati huohuo; hivyo hawezি kutenda haki katika mchezo.

107. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bado ina mtazamo kwamba kama mfumo uliopo sasa hautarekebishwa na kama Rais hatafuta kauli yake kwamba Mkurugenzi atakayemtangaza Mpinzani atafutwa kazi chaguzi zitapoteza maana yake na badala yake itakuwa ni fujo katika nchi inayoweza kupelekea machafuko ya kisiasa. Hivyo, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kushughulikia jambo hili mapema ili kuepuka uvunjifu wa amani unaoweza kutokeea.

H. MFUMO WA UCHUMI WA SOMO JAMII NI JAWABU LA KUPANGA MIPANGO YA MAENDELEO INAYOTEKELEZEKA

108. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilieleza katika hotuba yake ya bajeti mbadala kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwamba mapambano ya muda mrefu wa takriban miongo mitano ya Tanzania kujinasua katika lindi la umasikini na kushindwa kufikia lengo hilo; kulitokana na mfumo mbovu wa uchumi wetu. Tulieleza kwamba; Mosi, mfumo wetu wa uchumi umepitwa na wakati na hauendani na mahitaji ya dunia ya sasa; lakini pili ni uchumi uliohodhiwa na Serikali jambo ambalo limeua nguvu ya soko katika kuamua mustakabali wa uchumi. Tulishauri kwamba, Mfumo wa Uchumi wetu usipofanyiwa marekebisho makubwa; Tanzania itaendelea kuwa maskini milele yote.

109. Mheshimiwa Spika, huu ni mfumo wa uchumi ambao ni shirikishi na endelevu na unaomgusa kila Mtanzania kwa nafasi yake. Ni mfumo ambao unaheshimu nguvu ya soko katika kuamua mustakabali wa uchumi, ni mfumo unaoheshimu umiliki binafsi wa mali na pia ni mfumo unaoruhusu Serikali kuingilia kati pale kunapokuwa na hitilafu katika soko. Kwa kifupi ni mfumo unaochukua mambo mazuri ya mfumo wa uchumi wa kibepari na kuyaweka pamoja katika kujenga mfumo wa uchumi imara ambao unawapa wananchi fursa ya kushiriki kikamilifu katika kuujenga uchumi

wa Taifa lao lakini pia kuwapa fursa ya kunufaika na uchumi wao kikamilifu.

110. Mheshimiwa Spika, mfumo huu wa uchumi ni mfumo ulioainishwa katika Sera ya Uchumi ya CHADEMA iliyozinduliwa Septemba, 2018. Pamoja na jitihada za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuishauri Serikali kuutumia mfumo huu katika Bunge la Bajeti, 2019, ili kuondokana na matatizo ya kiuchumi ya miaka mingi; Serikali ilibenza mfumo huu na kusema kuwa inaufahamu zaidi kuliko CHADEMA na kwamba ni mfumo ambao hauwezi kutekelezeka Tanzania.

111. Mheshimiwa Spika, mwezi mmoja baada ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa ushauri huo kuhusu Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii, yaani Julai, 2019; taasisi za kidini zikiwemo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA); Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) walitoa taarifa ya utafiti wao kuhusu hali ya uchumi wa Taifa na kuja na mapendekezo ya kubadili mfumo wetu wa uchumi ili tuwe na mfumo wa uchumi ambao ni shirikishi na endelevu utakawanufaisha Watanzania wote bila kujali tofauti zao kiuchumi.

112. Mheshimiwa Spika, katika Taarifa hiyo, Taasisi hizo zilifanya uzinduzi wa Mfumo Mpya wa Uchumi kwa Tanzania unaojulikana kama Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii (Social Market Economy). Kimsingi taasisi hizi zilliona mantiki na kuunga mkono hoja ya CHADEMA ya kubadili mfumo wetu wa uchumi na kuanzisha mfumo mpya wa uchumi ili kuondokana na matatizo ya m dororo wa uchumi na umaskini yaliyodumu kwa zaidi ya miaka 50 toka nchi yetu ipate uhuru. Mtakumbuka kwamba CHADEMA kimekuwa chama cha kwanza cha siasa nchini Tanzania kupendekeza katika Sera zake zilizozinduliwa tarehe 25 Septemba, 2018 kuanzishwa kwa Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii.

113. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba azma ya chama ya kutekeleza pendekezo la kuanzishwa kwa mfumo wa uchumi wa Soko Jamii inafanikiwa; CHADEMA kuititia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika Bunge la Bajeti

liloketi toka mwezi Aprili hadi Juni, 2019; ilieleza kwa kirefu katika katika maoni yake kuhusu Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuhusu haja ya kuanzisha mfumo mpya wa uchumi ambao ni wa Soko Jamii. Katika maoni hayo, chama kilionesha namna ambayo mfumo uliopo wa uchumi usivyoendana na mahitaji ya dunia ya sasa ya utandawazi na jinsi mfumo huo ulivyoshindwa kutatuta changamoto za kiuchumi zinazolikabili Taifa.

114. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja ya kuanzisha Mfumo Mpya wa Uchumi wa Soko Jamii imeungwa mkono na Jumuiya ya Wasomi, watafiti na wataalamu waliobobea katika masuala ya kiuchumi; na kwa kuwa mfumo wetu wa uchumi umeshindwa pasi na shaka yoyote kutatua changamoto za kiuchumi zinazolikabili Taifa; napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya CHADEMA na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoa rai kwa Serikali kuitisha mjadala wa kitaifa kuhusu hali ya uchumi na kujadili faida za mfumo wa uchumi unaopendekezwa na hatimaye kuanza kutekeleza mfumo huo ili kujenga uchumi shirikishi na endelevu kwa manufaa ya wananchi wote.

I. HITIMISHO

115. Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza yafuatayo:-

- i. Serikali iheshimu na itekeleze matakwa ya ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Nchi yanayoitaka kuleta Muswada wa Sheria Bungeni kwa ajili ya kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo.
- ii. Serikali iijenguee utamaduni na nidhamu ya kutekeleza bajeti za maendeleo kwa ukamilifu kama zinavyodhinishwa na Bunge.
- iii. Serikali iache tabia ya kutumia fedha nje ya bajeti (reallocation of budget) iliyoidhinishwa na Bunge kutekeleza miradi ambayo haijaainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo – huko ni kuuvuruga Mpango.

- iv. Serikali iweke kipaumbele katika miradi au sekta zinazogusa maisha ya watu wengi na zenye kuchochea ukuaji wa sekta nyingine.
- v. Serikali ijenge na kuwezesha mazingira rafiki ya kisiasa (fair and friendly political situation) ili kudumisha amani ya nchi na hivyo kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufanisi.
- vi. Serikali ikubali kuupokea na kuufanyia kazi mfumo mpya wa uchumi wa Soko Jamii ambao unaipa nafasi sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa uchumi tofauti na ilivyo sasa ambapo uchumi unahodhiwa na kuendeshwa na Serikali.

116. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

David Ernest Silinde (Mb)

**KNY. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

5 Novemba, 2019

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa David Silinde kwa mawasilisho uliyoyafanya na kama nilivyooleza kabla hotuba yote Waheshimiwa Wabunge mnayo na hotuba zile zingine zote mnazo ya Mheshimiwa Waziri, ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na ya Msemaji wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni na zile *documents* zingine za mpango wenywewe na kadhalika pia mnazo katika vitendea kazi vyenu.

Waheshimiwa Wabunge, ni ushauri wangu kwamba uchangiaji tuanze jioni ya leo na wale wachangiaji wa leo tutawapa dakika kumi na tano, kumi na tano ili wajipange vizuri watuanzie zoezi hili. Kwa hiyo kwa sababu kila *documents* mnazo ni vizuri mkapitia michango yenu mtuwekee misingi ya namna ya kuanza zoezi hili la wiki nzima. Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

(Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuwataarifuni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amelazimika kusafiri kidogo kurudi jimboni nyumbani, kwa sababu amepata msiba wa kufiwa na kaka yake, ndugu yake kabisa, kaka mkubwa. Kwa hiyo tunaungana naye kwa niaba yenu katika kumpa pole katika msiba huu mkubwa na mzito ambao mwenzetu ameupata. Kwa maana ya shughuli za Serikali sasa yupo Mheshimwa Dkt. Mwinyi kuhakikisha mambo yanaendelea kama kawaida. Tunaiombea roho ya marehemu ikae mahali pema peponi. Amina

Pia ninalo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe, *Chapel* ya Bunge, wale wote ambao mnahudhuria Ibada katika *Chapel* ya Pius Msekwa mnaombwa kwenda pale leo tarehe 5 Novemba, 2019 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge wakati huu wa saa saba mchana.

Wachangiaji wetu jioni ya leo ni pamoja atatuanzishia Mwenyekiti wa Kamati ya Mheshimiwa Mashimba Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na wengine wote ambao mmeomba mtakuwepo katika orodha na kama nilivyokwishaelekeza mtakuwa na dakika kumi na tano, kumi na tano kwa siku ya leo kwa hiyo mijipange vizuri.

Basi, baada ya maelezo hayo kwa kuwa tutaanza jioni na Mheshimiwa Naibu Spika atakuwa hapa, basi naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

(Saa 6.58 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika alikuwa ameshataja majina ya Wabunge ambao tunganeza nao kuchangia kwenye mpango ambao umewasilishwa. Tutaanza na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk ajiandae.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasoi ili niweze kuchangia mapendekezo pamoja na muongozo wa Mpango wetu wa Mwaka wa 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ambayo tuanajadili kwenye kikao chako hiki ni mapendekezo ambayo yamepitia pia kwa wadau wengine na kupitia hatua mbalimbali hatimaye kuja kwenye Kamati ya bajeti lakini pia mwishoni yamekuja kwenye Bunge lako hili Tukufu ili pia Waheshimiwa Wabunge waweze kutoa mapendekezo yao ili kuboresha mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2020/2021. Kwa hiyo, hapa tunajielekeza kwenye kuboresha mapendekezo haya na kupendekeza mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wanadhani kwamba ni muhimu yakawemo ndani ya mpango wa maendeleo wa Mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha pili ni mwongozo; tunaoujadili ni mwongozo huo wa mapendekezo na mwongozo unatoa tu muelekeo kwa namna gani Wizara,

Taasisi na Mashirika ya umma, halmashauri zetu na watu wengine wa Serikali wanaongozwa katika kupanga, katika kubajeti, katika kutekeleza na kufuatilia na hatimaye kutoa taarifa kwa mipango watakayoitekeleza mwakani. Nilitaka nianze na huo ufanuzi ili kwamba tuweze kuelewana tunapokwenda pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, hapa hatujadili mpango wenyewe haujafika ni mapendekezo.

Mhesgimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze mambo machache ambayo naamini na ni mawazo yangu. Mengine tumeyazungumza kwenye Kamati ya bajeti lakini mengine ni mawazo ambayo ninadhani pia ni muhimu kuyazungumza mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni changamoto ya mzao yetu ya kilimo; nakumbuka mwaka jana tulikuwa na changamoto ya masoko ya zao la korosho mpaka Mheshimiwa Rais alilingilia kati, Korosho zikaanza kununuliwa, zikanunuliwa lakini zikakaa muda mrefu bila kuuzwa nje ya nchi mahali ambapo tunauza kwa wingi ikiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna changamoto ya zao la pamba mwaka huu; mwaka huu pia tumepata changamoto hiyo kwasababu soko la pamba kwenye soko la Kimataifa lilianguka kwa hiyo bei ikawa ya chini lakini bado tunaishukuru Serikali kwasababu iliweka bei ambayo ingekuwa na faida kwa wakulima sasa kukatokea kutoelewana hapo kati ya wakulima pamoja na wanunuzi wa zao hilo la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna changamoto hapa kubwa ya masoko ya mzao yetu. Nilikuwa naomba kwamba katika mapendekezo ya mpango huu, hebu Serikali ijielekeze katika kutatua changamoto hii. Tunapozungumza bado kuna wakulima wa pamba hawajalipwa pamba yao kwenye maeneo mengi ya maeneo wanayolima pamba. Sasa tatizo ni soko la zao hilo sasa ni muhimu sasa Serikali ikachukua hatua tangu mapema kuhakikisha kwamba masoko ya mzao yetu ya kilimo yanatengenezwa mapema

ili wakati wakulima wetu wanapovuna basi waweze kuuza mazao yao bila matatizo, bila shida, bila kurupushani na bila wao kuhangaika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana tufanye hivyo na tutaboresha masoko ya mazao yetu hata hapa ndani ikiwa tutakubaliana na usemi wa Serikali ya Awamu ya Tano kwamba tuwe na viwanda vinavyochakata mazao yetu badala ya kuyauza yakiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna soko la bidhaa; soko hili lipo, limesajiliwa na lina watumishi lakini hatujaona likitumika sawa sawa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwenye mapendekezo haya basi soko la bidhaa lionekane sasa linafanyakazi yake iliyopangwa kufanyika ya kuuza mazao yetu ya kilimo. Sasa inavyoonekana sasa hivi ni kama halijawa na uwezo mkubwa wa kufanya kazi hiyo sasa ni vizuri kwenye mapendekezo ya mpango huu, mapendekezo yangu ni kwamba lipewe uwezo wa kufanyakazi iliyopangiwa lifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nililotaka kuzungumzia ni mapato yetu hasa yale yanayokusanywa na *TRA*; tunaipongeza *TRA* kwa kuongeza mapato kutoka bilioni 800 Mwaka 2016 hadi trillioni 1.3 sasa trillioni 1.3 imeendelea hivyo kwa muda sasa wa miaka miwili tunakwenda mitatu haiongezeki zaidi ya hapo sasa ninachohisi ni kwamba inawezekana *TRA* wamefika mahali ambapo pengine hawawezi tena kwenda zaidi ya hapo lakini nakumbuka dhana ya uchumi wa viwanda. Kiwanda kikiwa kikubwa kikawa na malighafi nyingi, wafanyakazi wengi, mashine nyingi namna ya kukitawala inakuwa ngumu maana kunatokea kitu kinachoitwa *disconomies of scale*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana kwa *TRA* kitu kama hiki pia kimetokea sasa *TRA* ni kubwa. Sasa mapendekezo yangu ni kwamba, mapendekezo haya tunayojadili yatambue kwamba *TRA* ni kubwa na pengine inatakiwa sasa muundo wake utengenezwe upya kwa namna ya kuwa na Kanda badala ya kuwa na mikoa na wilaya kama ilivyo sasa hivi ili *management* ya *TRA* ya juu iweze kuwasiliana na watu wachache badala ya kuwasiliana

na watu mikoa 26 na wilaya sijui 100 na ngapi, huyo mkuu wa *TRA* inamuwia vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, muundo wake ubadilishwe na utakapobadilishwa utawezesha hawa watu wa kwenye Kanda kuwafikia kwa urahisi watu wa Mkoani, watu wa Wilayani na hivyo kuongeza mapato ya Serikali au mapato yanayotokana na kodi vinginevyo itakuwa bado ni ngumu kwasababu *TRA* imekuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu tulioupata mwezi wa tisa, mwezi wa juzi, *TRA* wamekusanya trillioni 1.740 sasa hiyo inawezekana ikawa ya kipindi tu, ikawa ni *event*, tusiporekebisha mambo kadhaa wa kadhaa lakini inawezekana kabisa makusanyo yetu kwa vyanzo tulivyonyavyo hatujakusanya kiwango cha kutosha lakini ikiwa tutarekebisha muundo wake kwa viwango au kwa kodi zilizopo sasa hivi inawezekana tutakusanya kiwango kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni deni la Serikali; deni la Serikali limekuwa likiongezeka na nakublaiana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri pia kwamba deni hili bado ni himilivu lakini Mwezi Agosti tumeambiwa denoi hili kuwa Trillioni 49, Mwezi Agosti mwaka huu lilikuwa trillioni 52 limeongezeka sasa ni himilivu kwasababu ya vigezo mbalimbali ambavyo Waheshimiwa Wabunge pia wanavifahamu humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilichokuwa naomba kwenye mpango huu tunaoujadili, ni kwamba thamani ya shilingi yetu iendelee kuwa imara pia. Mpango uhakikishe thamani ya shilingi yetu inaendelea kuwa imara vinginevyo ikitikisika kidogo tu deni hili linaweza likaongezeka bila hata kuongeza kukopa ikiwa shilingi yetu itakuwa dhaifu dhidi ya sarafu ya nchi zingine hasa zile tunazofanyanazo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba sana kwenye mpango huu ambao tunaupendekeza, Serikali ihakikishe thamani ya shilingi yetu inakuwa imara, inaimarika

dhidi ya Dola ili ya kwamba tusipate shida. Kuna usemi unaosema "wenzetu nchi zilizoendelea wakipata kikohozi sisi huku tunalazwa" maana yake ndiyo hiyo kwamba shilingi yao ikiimarika na ya kwetu ikawa dhaifu tunapata shida. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwmaba kwenye mpango huu tunaoujadili, Serikali ihakikishe shilingi yetu ni imara, imeimarika na kwmaba inakwenda vizuri dhidi ya sarafu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo machache ya kusema jioni ya leo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchnago wangu wa maoni kwenye mapendekezo ya Mpango na muongozo wa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake yote kwa jinsi ambavyo wameleta mapendekezo haya na hasa hasa jinsi ambavyo amewasilisha kwa ufasaha mapendekezo haya na niseme tu kwamba bahati nzuri sisi katika Nchi yetu tumebahatika sana kuwa na nguli wa mipango tangu wakati wa uhuru mpaka leo. Nchi nyingine zimekuwa zinakuja kujifunza uandaaji wa mipango katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka tangu enzi za wakina Dkt. Justina Rweyemamu, wakina Profesa Kigoma Malima na sasa Dkt. Mpango, mipango yote imekuwa ni

mizuri, kwa kweli ni mizuri sana hata ukiitaza, ukisoma mpangilio wake, malengo, shabaha imekuwa ni mipango ambayo kwa kweli inalenga kumkwamua Mtanzania kutoka kwenye umasikini na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mipango yetu kuanzia mwaka 2000 tulipoanza kutekeleza dira ya maendeleo ya Taifa, ule mpango wa kupunguza umasikini ambao ulilenga huduma za jamii, uje kwenye MKUKUTA wa kwanza, uje kwenye MKUKUTA wa pili ambao uliunganishwa na mpango wa kwanza wa miaka mitano kwa kweli mipango yote imekuwa ni mizuri sana na leo hii tunakaribia kuhitimisha Awamu ya II au mpango wa pili wa miaka mitano kuelekea kwenye mpango wa tatu wa miaka mitano ili tuendelee kusaidia uchumi wa Nchi hii ufile katika ngazi ya katи ya uchumi Kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuko katika mwaka wa nne wa utekelezaji na mpango ambao unapendekezwa leo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha unatupeleka kwenye maandalizi ya mpango wa mwisho wa miaka mitano. Kwa kweli hili ni jambo ambalo tunatakiwa tujipongeze kama Taifa, tunakwenda vizuri. Nchi nyingine huwa wanaishia katikati, wanakuwa na mpango wa miaka 15 (*long term*) wakifika baada ya miaka mitano wanaacha wanaingia katika kutatua mipango mingine lakini sisi tunakwneda *sequentially*. Baada ya miaka mitano tunaingia Awamu ya II tunaingia Awamu ya III. Hilo ni jambo ambalo tunatakiwa tujipongeze kama Taifa. Kwa kweli kama nilivyosema mwanzo mipango yetu ni mizuri sana na kazi zinazopangwa kwenye mipango ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo au maoteo ya makusanyo huwa ni mazuri sana yanalenga kuhakikisha wkamba mpango unatekelezwa, matarajio ya Watanzania ni mazuri tatizo ambalo ninaliona katika utekelezaji ni dogo sana. Kwa mfano, hadi sasa katika utekelezaji wetu tumekaribia kutekeleza malengo mengi kwenye mpango. Ukiangalia mipango mikubwa, ufufuaji wa Shirika la Ndege, ujenzi wa miundombinu, ukiangalia utekelezaji kwenye sekta

ya umeme, ujenzi wa reli, ujenzi wa minara ya mawasiliano na maeneo mengi sana, vituo vya afya, hospitali mpya, ujenzi wa madarasa, mabwalo na mabweni kwenye shule za msingi na sekondari na kwa kweli katika maeneo mengi tumefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji, jambo ambalo naipa heko serikali yetu ni jinsi ambavyo tumebadilika kutoka zamani ambako wenzetu walipokuwa wanatufanya tathmini. Kwa mfano, nirejee taarifa ya maendeleo ya Dunia (*World development report*) ya mwaka 2004 ambayo ilisema kwa sababu ilifanyika Tanzania hapa, ilisema fedha haziendi kwa watu masikini lakini ukiangalia utekelezaji wetu wa leo chini hasa ya Awamu ya Tano hii, fedha nyingi zimekuwa zinakwenda kwa watu masikini katika sekta ambazo zimezitaja. Walisema kwamba kuna matatizo ya nidhamu makazini, kulikuwa na *absenteeism* leo hii nidhamu kazini kwa kweli imeongezeka na mambo mengi ambayo waliyaona kipindi kile yamebadilika. Kwa hiyo, kwa kweli napenda sana kuipongeza sana Serikali yetu kwa kufanya kazi kubwa sana ambayo inalenga kumkwamua Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto bado zipo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezitaja changamoto, kwa mfano, changamoto kwenye ukusanyaji wa mapato kwamba bado kuna mianya, mapato yanapotea na ndiyo maana hatujawahi kufikia asilimia 100 ya makadirio ya makusanyo na sababu zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni pamoja na uwepo wa njia za panya yaani Bandari bubu, ukwepajji mwingine wa kodi, wahisani kutotimiza ahadi kwa kweli haya mimi nilikuwa naomba sana Serikali yetu iyavalie njuga kuhakikisha kwamba hizi changamoto zinaondoka. Tufanye kila mbinu kuhakikisha wkamba changamoto hizo zinaondoka ili tuendelee kufanya vizuri zaidi katika kumuhudumia Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine iko kwenye ufuutiliaji na tathimini, hapo nataka nisisitize kidogo; kuna tofauti kati ya kutembelea mradi na kufuutilia mradi hasa kwa wataalam. Kiongozi anaweza akatembelea mradi

kwa maana ya kuona kama ni ujenzi unaondelea lakini mtaalam anapotembelea mradi hapo ndiyo naona ni kioja. Mtaalam hatakiwi kutembelea mradi, mtaalam anatakiwa afuatilie utekelezaji wa mradi, kwa maana gani?

Mradi wowote ambao kwa mfano, unajengwa na Mkandarasi una mkataba sasa mtalaam anapokwenda kufuatilia mradi mkataba hajausoma huu, hana mkataba hapo ndiyo unapoona kioja. Lazima wataalam wetu wabadi like, kazima wanapokwenda kukagua miradi au kufuatilia miradi wawe na nyenzo za ukaguzi au nyenzo za ufuatiliaji ambao ni pamoja na mkataba, ambao ni pamoja na makadirio ya ujenzi au *BOQ*, ambayo ni pamoja na michoro ili ajionee je, huu mradi unaotekelizwa unafuata makubaliano ambayo yako kwenye mkabata na yaliyopo kwenye michoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo la pili ni tathmini; tathmini ambayo tumeizoea sana Serikalini na nchini kwa ujumla ni tathmini ile ya kila mwaka ambayo inafanyika kupitia bajeti kila Wizara inafanya tathmini yake na Mheshimiwa Waziri wa Fedha akija hapa huwa anahitimisha ile inaitwa *budget review* au mapitio au tathmini ya Mwaka ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wakati anasoma bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mipango hii lazima kuwe na tathmini ya nusu mwaka au *medium review*, tathmini ya nusu muhula au *midterm review*. Kama kuna mpango wa miaka mitano inapofika nusu lazima ifanyike tathmini ya nusu ya utekelezaji wa muda wa ule mpango halafu mwishoni mwa muhula yaani kama ni miaka mitano, mwishoni mwa miaka mitano ifanyike tathmini ya kina ambayo itasaidia sasa maandalizi ya mpango wa miaka mitano inayofuata. Kwa kweli hapa tumekuwa kidogo tunatatizo ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwasababu analifahamu ningependa aliye kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa tumekuwa tukipata vipaumbele vingi, lakini nikitazama kwa undani, tumekuwa tuna upungufu kwenye eneo la ardhi. Sekta ya

Ardhi kwa upande wangu ndiyo sekta mama ya uchumi. Hakuna mtu atafanya ujenzi wa aina yoyote bila kugusa Sekta ya Ardhi. Watu wa kilimo wanafanya shughuli zao kwenye ardhi, mifugo, uvuvi, maliasili na utalii ni kwenye ardhi; madini yako kwenye ardhi. Sasa Sekta ya Ardhi kama hatujaipa kipaumbele, kwa mfano kwenye eneo dogo tu la maeneo ya uwekezaji, hilo litakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuipe kipaumbele Sekta ya Ardhi na Mheshimiwa *Doctor*, Mwalimu wangu anajua vizuri sana. Naomba sana, tunapoendelea kupanga vipaumbele vyetu tuikumbuke Sekta ya Ardhi. Huyu Waziri wa Ardhi tumsaidie aweze kutimiza matarajio ya Watanzania. Haiwezekani tuendelee kupima Dodoma na Dar es Salaam peke yake, lazima tupime miji yote ikae vizuri, makazi yakae vizuri. Halafu kule vijijini kuna miji ambayo inaibuka kwenye vijiji, ina ujenzi holela. Lazima tumsaidie Waziri wa Ardhi aweze kuratibu miji ambayo inaibuka vijijini iwe na makazi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kila kipande cha ardhi Tanzania kikipimwa tutapata maendeleo ya kutosha kwa sababu ardhi itakuwa na thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani yangu ni hayo. Naunga mkono hoja, Ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Sudy Mwilima na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, ajiandane.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii niweze kuchangia Mpango ambaao ni wa awamu ya pili kati ya Awamu Tatu za Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa najaribu kupitia Mpango huu wa 2016/2017 - 2020/2021, nilikuwa najaribu kupita kwenye maeneo ambayo yamefanyiwa utekelezaji na kwa kiasi kikubwa naweza kusema tuipigie Serikali makofi kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tunakaa tuna-*negotiate* mambo mbalimbali kwenye kikao, kwa kweli nchi yetu kwa miradi mikubwa ambayo inafanyika imetubeba sana. Na mimi niwaambie Wabunge wa CCM kama kuna wakati mmefanya mambo mpaka yamefilisi upande wa kule kwenye hoja ni kipindi hiki. Mambo mazito kweli kweli! Siku moja nilikuwa namsikiliza kiongozi mmoja anasema, unajua uamuzi wa kununua ndege; ziko ndege ngapi? Kununua ndege saba...

MBUNGE FULANI: Nane.

MHE. MARWA R. CHACHA: Nane eeh!

MBUNGE FULANI: Eeh!

MHE. MARWA R. CHACHA: Siyo mchezo! Ni maamuzi magumu, lazima mtu awe ameamua kweli kweli. Mtu mwepesi mwepesi hawezi. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake. Nilikuwa nasikia asubuhi kwenye Ripoti ya Kambi ya Upinzani wanasesma Mpango haufuatwi, haujatungiwa sheria, ni maamuzi ya mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, nikawa najiuliza, nikawa napita kwenye Mpango humu nione uamuzi wa mtu mmoja ambao umetekelzwa ambao uko nje ya Mpango ni upi? Nikakuta Bandari imo kwenye Mpango, reli iko kwenye Mpango, ndege ziko kwenye Mpango. Sasa nitamwomba rafiki yangu Mheshimiwa Silinde atuoneshe kitu hata kimoja tu ambacho humu hakimo ambacho kimefanyiwa maamuzi yaliyo kinyume na Katiba na Sheria za Nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*chip in* kidogo baadhi ya maeneo ambayo ninadhani tuyarekebishe ambayo kimsingi kwenye utekelezaji wa Mpango nimeona yana shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo. Uksikia watu wanalia hawana hela

mfukoni, ujue kwamba kuna shida kwenye Sekta ya Kilimo. Kama kuna eneo ambalo kiukweli tunahitaji kupeleka nguvu kubwa, kuwekeza ni kwenye kilimo. Mfano, kule nihakotokea Jimboni kwangu Serengeti, wananchi wa Serengeti walikuwa wanalima tumbaku. Kulikuwa na Kampuni ya *Alliance One*, wakilima tumbaku, wakivuna wakiuba, shilingi bilioni 20 zinazungua ndani ya Wilaya. Unakuta watu mifukoni wana pesa. Tangu kampuni ilivyoonedoka, pesa hakuna. Kwa nini? Kampuni imeondoka. Kwa hiyo, jambo hili la kilimo lazima tulitazame kwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango huu tuna mikoa 17 inayolima pamba. Nimekuwa nikijiuliza, hivi ni lazima sisi Tanzania twende kuuza pamba ghafi nje? Kwamba mikoa 17 izalishe pamba, sisi tuwe watu wa *ku-export* pamba, hii itatuchukua mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka enzi za Mwalimu Nyerere kulikuwa na viwanda vingi sana vilivyokuwa vinachakata pamba, kwa mfano, *MWATEX*, *KILTEX*, *MUTEX* na vingine vingi. Sasa mimi nikadhani Serikali ukiuliza inasema mambo ya viwanda ni Sekta Binafsi inatakiwa ijenge, lakini kuna viwanda vingine lazima Serikali iingilie kati kuangalia namna ya kusaidia Sekta Binafsi kujenga viwanda. Maana ukijenga kiwanda cha *ku-process* pamba, leo utaokoa wananchi wa mikoa 17. Siyo jambo dogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali inaweza kutoa mabillioni ya pesa ikajenga miundombinu kwa mfano, ukununua ndege hata moja, ni *billions of money* lakini kumbe unaweza uka-*finance* sekta binafsi kwa kutumia Mfumo wa *PPP* ikasaidia kujenga kiwanda cha *ku-process* pamba ambacho kiwanda hicho kitaokoa wakulima wa mikoa 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mawaziri husika, jambo hili la kilimo cha pamba liangaliwe kwa upya, kwa undani. Kama ambavyo tumeingia *PPP* kwenye miradi mingine, tunaweza kuingia *PPP* kwenye kiwanda cha kuchakata pamba tukaleta

ajira kwa wananchi wetu ambao wengi wanategemea pamba. Hilo lilikuwa wazo langu kwenye kilimo cha pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye barabara. Unakumbuka kilianzishwa chombo kinaitwa *TARURA* kwa ajili ya kusimamia utengenezaji wa barabara mijini na vijjini na sababu ilikuwa ni kwamba wakati fedha zikienda kwenye Halmashauri zimekuwa hazitengenezi barabara zetu kwa kiwango kinachotakiwa. Iliamuliwa kwamba kingeundwa chombo hiki kikasimamia utengenezaji wa barabara za vijjini na mijini, barabara zingekuwa za kiwango, lakini hali imekuwa sivyo. Kwa nini hali imekuwa sivyo? Ni kwa sababu *TARURA* wanapata pesa kidogo, pesa wanayopata ni ile ile ambayo Halmashauri za Wilaya zilikuwa zikipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka kwa sasa *TARURA* hawako chini ya Halmashauri, wana Ofisi wamepanga mitaani, kwa hiyo, wanalipa *bill* za majengo. Wanatumia gharama kubwa kwa ajili ya *bill* za ku-rent majengo. Kwa hiyo, ni gharama kubwa kwanza kuendesha chombo hiki. La pili, pesa wanayopata ni ile ile. Kwa mfano, nchi nzima *TARURA* inahudumia kilometra zaidi ya 100,000, wanapewa shilingi bilioni 250, hazitoshii hata kidogo. Hizi shilingi bilioni 250 ni pamoja na barabara za lami kwenye Majimbo mbalimbali. Kwa hiyo, unaweza kuona ni hela kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri, *TARURA* na *TANROADS* kutegemea Mfuko wa Barabara, shilingi 100 ya mafuta peke yake haitoshi, lazima Serikali ije na *financing* nyingine ya kuisaidia *TARURA* kusimamia barabara. Kwa wale Wabunge wa Majimbo tunaotokea huko Majimboni, hali ni mbaya kwenye vijiji kiasi kwamba mazao ya kilimo kutoka vijiji fulani kwenda sokoni inashindikana. Magari yanashindwa kwenda kuchukua mazao kwenye vijiji hivyo. Kwa hiyo, naomba Wizara, mbali na Mfuko wa Barabara tutafute chanzo kingine cha ku-finance *TARURA* ama tuongeze shilingi 50/= kwa ajili ya *TARURA* peke yake ili tuweze kuhudumia barabara za vijjini na mijini ambazo ziko chini ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo kama hakuna chanzo kingine cha kuisaidia *TARURA* ni bora Serikali ikubali kuchukua maamuzi magumu kwamba popote kila Wilaya ilipo, *TARURA* waruhusiwe ama wakopeshwe fedha wawe na vifaa nya kutengeneza barabara ili fedha ambayo ni ruzuku wanayoipata ya Mfuko wa Barabara watengeneze wenewewe, vinginevyo barabara zetu zitaendelea kuwa mbaya sana. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu ili *TARURA* ikae vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Sekta ya Utalii. Sekta ya Utalii ni moja ya Sekta nzuri sana ambayo inachangia asilimia 24 ya mauzo ya huduma nje ya nchi. Ni moja ya Sekta ambayo inachangia kwenye *GDP* ya Taifa letu asilimia 17.2. Kwa hiyo, siyo sekta ya kubeza ni sekta ambayo inahitaji tuitazame kwa macho mangapi mangapi ili iweze ku-boom.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri kama wako hapa, kwa kuamua kujenga uwanja wa Serengeti uliopo Mugumu kutoka kwenye ule wa Seronera. Ni jambo zuri sana kwa sababu ndege zilikuwa zimejazana sana mle hifadhini na mnafahamu mpaka ikatokea ile ajali ni kwa sababu ndege zimekuwa nyangi. Nawapongeza sana watu wa *TANAPA* na Bodi ya *TANAPA* kwa kuridhia kwamba sasa wahamie kwenye uwanja ambao uko Mugumu. Nasi kama Halmashauri tuna hatimiliki tayari, tuna kibali cha *NEMna TAA* kwa ajili ya ujenzi wa uwanja ule wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, Mheshimiwa Mpango, kile kiwanja ni kiwanja kizuri sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba upande wa Magharibi wa Hifadhi ya Serengeti unakuwa kiutalii. Sasa ni vizuri Serikali itazame namna ya kuwasaidia *TANAPA*, namna ya kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kuboresha ule uwanja uwe katika kiwango ambacho kinatakiwa kwa sababu ndege zinaruka *almost* zaidi ya 200 kwa siku, siyo kitu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigosie barabara za kuunganisha mikoa na mikoa na hususan barabara ya kuunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha, barabara ya Makutano - Sanzate - Nata - Mugumu - Tabora B, Kilensi – Loliondo - Mtu wa Mbu. Hii ni barabara muhimu sana ya kiutalii na barabara ya kuanzia Sirari - Tarime - Mugumu ni barabara nzuri za kiuchumi kwa sababu unakuta watalii wengi wanaoshukia *Kenyatta International Airport* lazima waingie Sirari, Tarime. Sasa ni vizuri barabara hizi ziboreshwwe kwa kiwango cha lami maana ni barabara ambazo zina fursa ya kiuchumi ili ziweze ku-*boost* uchumi kwa wale watalii ambao wanatembelea Hifadhi ya Serengeti pamoja na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni maji. Maji bado *financing* yake pia hajakaa vizuri. Ni vizuri kwenye Mpango unaokuja, Mheshimiwa Mpango, mwangalia namna ya kupata *fund* nyingine ili kusaidia huduma ya maji vijijini. Maana huduma ya maji vijijini na yenewe ikitegemea Mfuko wa Maji shilingi 50/=, haitoshi. La sivyo, tuongeze ziwe shilingi 100 ili ziweze kusaidia. Kwa hiyo, nadhani kwenye hili ni vizuri mkaliangalia ili kuwepo na upatikanaji wa maji vijijini, kwani bado maji vijijini hali yake siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimpongeze Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri, naipongeza Serikai ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri. Naona kila sehemu Wenyevitii wa Vijiji wanapita bila kupingwa. Naona wenzetu wanalialia tu hawasimamishi sijui kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima. Hayupo, Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafuatiwa na Masoud Abdallah Salum na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ajiandae.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa naipongeza Serikai ya Chama cha Mapinduzi, inafanya kazi nzuri. Katika utawala wa Rais

Mheshimiwa Dkt. Magufuli wa miaka minne, lakini kazi na miradi iliyotekelizwa ni mingi sana, kwa hiyo, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la miradi. Kwa kweli Serikali inaleta miradi mizuri sana, lakini suala la utekelezaji ndiyo tatizo. Miradi ya maji kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu, tatizo la maji ni kubwa sana vijiji. Sasa Serikali inapopanga kutekeleza miradi ya maji vijiji, basi ile miradi ikamilike. Sasa mradi unachukua miaka mitano mpaka 10. Miradi ya *World Bank*, hatuna taarifa zake kwa sababu fedha zinatoka nje, lakini miradi ambayo inafadhiliwa na Serikali yetu hapa hapa, kuna miradi kama mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kijiji cha Bumila, Kijiji cha Iyoma, Kijiji cha Mima, Kijiji cha Mzanse, miradi imechukua miaka minne, huu wa tano sasa haikamiliki. Ndilo maana nilimWomba Mheshimiwa Waziri wa Maji aende awaeleze wananchi kwa nini ile miradi haikamiliki? maana mimi nimesema mpaka nimechoka na inaonekana kama mimi sifuatilii hii miradi. Serikali inafanya kazi nzuri sana, lakini naomba jamani mtekeleze hii miradi ili wananchi wawewe kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni barabara na madaraja. Kwanza naishukuru sana Serikali, nilipiga kelele sana kuona barabara ya Mpwapwa hadi Kongwa ijengwe kwa kiwango cha lami na Serikali katika bajeti ya mwaka 2019/2020 imenitengea fedha kama shilingi bilioni sita kuanza na kilometra tano. Sasa najiuliza, kutoka Kongwa *Junction* mpaka Mpwapwa ni kilometra 50, sasa hivi kila mwaka nkipata kilometra tano ina maana kukamilika kwa barabara ya Mpwapwa – Kongwa itachukua miaka 10. Naiomba sana Serikali watenge fedha za kutosha ili barabara hii iweze kufanyiwa matengenezo na ikamilike kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kuanzia Mbande kwenda Kongwa *Junction*. Barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha lami, lakini matengenzo yake yameanza mwaka 2012 mpaka sasa mwaka 2019, yaani

hata kilometra saba hawajafika na hii barabara inakwenda kwa Mheshimiwa Spika. Sasa nauliza, miaka tisa, hii miaka yote wanatengeneza, kuna tatizo gani? Wakandarasi hawalipwi au kuna tatizo gani? Kwa hiyo, naomba sana hawa wakandarasi, Serikali iwalipe haraka ili waweze kukamilisha hii miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Umeme Vijiji (REA). Naishukuru sana *REA* imefanya kazi nzuri sana. Katika Jimbo langu karibu vijiji 62 vimepata umeme. Vijiji ambavyo havijapata umeme ni kama vijiji vitano tu havijapata umeme. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Serikali, hivi vijiji ambavyo vimebakia basi Serikali ijitahidi kukamilisha miradi hii ili wananchi waweze kupata huduma ya umeme. Huduma ya umeme ni maendeleo, huduma ya umeme ni uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, naomba Serikali ikamilishe miradi ya umeme katika vijiji vile ambavyo vimebakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kilimo. Ni kweli taarifa ya Mheshimiwa Waziri inasema kwamba kuna baadhi ya Mikoa imepata chakula lakini kwa kweli Mkoa wetu wa Dodoma haiwezekani mtu akasimama akasema wananchi ni wavivu, hapana! Wananchi wa Mkoa wa Dodoma wanafanya kazi nzuri sana lakini bahati mbaya sana mvua zimekatika mwezi wa pili. Kwa hiyo, mimea yote ilikauka, hakuna kitu hata kidogo walichovuna. Kwa hiyo, Mkoa wa Dodoma una upungufu mkubwa sana wa chakula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iuangalie Mkoa wa Dodoma kwa jicho la huruma ili wananchi hawa ambao wameathirika sana na mvua ambayo haikunyesha na wana chakula kidogo sana. Kwa hiyo, Serikali ijiandae kwa ajili ya kusaidia wananchi ambao wana tatizo kubwa sana la njaa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie haya machache. Bada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Julius Kalanga ajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Mapendekezo haya ya Mpango. Kipekee kabisa namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai kwa sababu wote tulio hapa tumebarikiwa kuweza kuzungumzia maendeleo ya nchi hii na wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutamka rasmi kwa kweli kwamba Mpango huu ni mzuri na umeandaliwa kitaalam na kwenye Kamati tulipata fursa ya kuelimishwa. Sambamba na hilo, niseme mambo mengine yametekelzeza siku za nyuma ni bahati tu kwamba jambo likishatekelezeka haliwi tena motisha. Nasema hivyo kwa sababu hata guru mmoja wa *management* Maslow alisema: "*once a need is satisfied is no longer motivation*". Hapo alikuwa anazungumzia mahitaji maalum ya mwanadamu katika maisha, ikiwemo chakula, mavazi, malazi yaani nyumba na pia labda *esteem hierarchy of needs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Tumekuwa na kipindi kizuri japo kwa kupambana lakini tumefuta maradhi. Kwenye Mpango wa kwanza kabisa walikuwa wamedhamiria kuondoa ujinga, umaskini na maradhi. Ujinga umeondolewa kwa jumla na sasa hivi Watanzania wanaweza wakaongea kama watu wanaoelewa. Siyo hayo tu, maradhi yaliyokuweko wakati tumepata uhuru hayapo tena. Hata awamu hii tumeona hospitali zimeboreshwa, madawa yamekuwepo, tunaona ni jambo la kawaida ambavyo siyo kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo. Niseme tusibweteke bali tuzidi kupambana na hapo ndiyo nasema kwamba kuna haja ya kila mmoja wetu hapa ndani kuleta mapendekezo ili kuboresha Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunapanga? Tunapanga ili kutengeneza taswira ya siku za baadaye tunataka nini na iweje. Pia tunapanga kwa sababu rasilimali ni kidogo hatuwezi kwenda na vyote kwa mkupuo lazima tupange ili twende na vichache tupangue kila kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu nilitamani kuona jinsi gani mwananchi wa kawaida anapata fursa nzuri kufikia benki na ninaposema benki nina maana mabenki yaliyopo nchini. Mpaka sasa hivi tuna *commercial banks* zinazozidi 50 na zinakaribia 60 tuseme zaidi ya 57 lakini mabenki hayo pamoja na watu kupenda kuweka hela zao benki kwa usalama, kuweka katika amana ili waweze kuzifaidi siku za baadaye na ili ziweze kuongezewa, ukiweka kwenye amana unapata *interest rate* yaani unapata faida imekuwa ngumu kwa sababu gharama ambazo benki inatumia kuweka hela zile imezidi ile asilimia 3 ya amana inayolipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza mwananchi huyu wa kawaida ambaye hataki kulalia hela yake kama mto, hataki kuificha ikaja kuliwa na mende na panya au siafu, anafanyaje ili aweze kupata raha ya kuweka hela yake benki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo mwananchi huyu huyu anapopeleka hela yake benki kuna mwagine ambaye yuko tayari mwenye uelewa zaidi anakwenda kukopa. Hapa kwenye ukopaji wako wa aina mbili, wako wakopaji ambao ni wa biashara, wakopaji wakubwa wakubwa au hata kama hakopi lakini wafanyabiashara wakubwa kama aliyeka kushoto kwangu, lakini wako wakopaji wadogo kama mimi ambao tunakopa katika mishahara yetu na wafanyakazi wote wa nchi hii. Ukiija kuangalia riba zao zinalingana anayekopa kwenda kufanya biashara ni asimilia 16 au 17 na anayekopa kutoka kwenye mshahara ni asilimia 16 au 17. Sasa najiuliza uhalali uko wapi? Natamani kuona Mpango huu wakati unaandalishi mabenki hayo yanakaa chini na Serikali na kuona namna ya kuteremsha riba hii ya kukopa. Unakuta Benki Kuu iko vizuri,

discount rate sasa hivi imefika 7 ambapo ndiyo gharama ya *commercial banks* kuchukua hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka nadhani ni mwanzoni mwa mwaka huu au mwishoni mwa mwaka jana Serikali imeamua kuwa *Treasury Single Account*. Kwa hiyo, sasa hivi mabenki hayapati hela kiholela kutoka Serikali lakini hela hiyo pia haipatikana kwa gharama kubwa sana inapatikana kwa asilimia 7 tu, nilitaraji kuona anapokopa mtu wa kawaida ambaye ni mfanyakazi, Mbunge au mtu ambaye kulipa wakati wa *re-payment* hakuna gharama kubwa akopeshwe labda asilimia 3 juu ya ile ya Benki Kuu ya 7, kwa hiyo, iwe kwenye *single digit* kama asilimia 9. Katika Mpango huu ningetamani kuona hiso riba zinarekebishwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nikirudi kwenye watu wa kawaida kuwa na *account*, nakwenda sasa kwenye mkulima wa korosho kwa sababu mwaka huu tumeelimishwa sana kwenye korosho anayefungua *account* katika benki wakati wa mauzo ya korosho. Mauzo ya korosho au kahawa yako kwa msimu, msimu ukiisha kashachukua hela yake amekwenda kujenga, amekwenda kufanya nini mpaka msimu mwingine tena wakati analipwa na lazima alipwe kwenye benki, anakuta ile *account* imeshakuwa *dormant* anaanza kuhangainka. Mzee huyu ametoka kijiji ni ametumia gari, amelala kule ili aweze ku-*activate account*, ni jinsi gani Serikali itaelekeza au itaongea na mabenki haya hizi *account* za hawa wakulima ziweze kuwa wazi bila gharama wala usumbufuli leta barua kwa Mwenyekiti, leta kitambulisho hiki watu hawa *account* hiso ziwe wazi kila wanapokuja kuingiza hela yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupendekeza jambo lingine ambalo ni kuhusu kujenga taifa lenye afya. Taifa zuri lenye afya ni taifa la leo na kesho. Wote hapa tuna afya nzuri kwa sababu wazazi wetu walitulea vizuri kati ya siku moja mpaka miaka mitatu. Sasa hivi unakuta utapiamlo bado uko katika maeneo yetu, hata maeneo ambayo unaweza ukafikiria labda wana vyakula sana na ambayo unaweza

ukafikiria labda lishe ni bora ikiweko Kilimanjaro bado kuna utapiamlo, Mbeya bado kuna utapiamlo, hiyo ni Mikoa ambayo nina uhakika utapiamlo uko katika asilimia 29 mpaka 30. Sasa Mpango huu unatusaidiaje kuhakikisha kwamba tunafuta kabisa utapiamlo katika nchi hii kama tulivyodhamiria kufuta kabisa watu kutembea bila viatu, tumeweza tukafuta watu hao hao wakaweza kuwa na afya bora, tukawa tunatoa dawa za minyoo shuleni, tunakwenda tunatoa *vaccination* shuleni, nakadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiitumia Wizara ya Mifugo na Wizara ya Kilimo tunaweza tukafuta utapiamlo. Wananchi wakielimishwa kuwalisha watoto wao vizuri na sasa hivi Waziri wa Afya anasema kabisa mtoto wako asile chochote mpaka miezi sita na kila binti anayejifungua sasa anatamani kunyonyesha kwa sababu pia binti ukionekana hunyonyeshi tayari unaonekana una yale maradhi, kwa hiyo, siku hizi wananyonyesha. Baada ya muda wa kunyonyeshwa mtoto huyu aendelee kupata chakula kizuri hata ule uji unaopikwa mashuleni uwe mzuri, uwe na maziwa, yagawanywe shuleni watoto wale wadogo wanywe uji wa maziwa mazuri na mayai yagaiwe shuleni, yai moja moja kila mtoto, watoto wetu wale vyakula vizuri waondokane na utapiamlo. Mama mjamzito ale vizuri kwa sababu mtoto anaanza kupata virutubisho akiwa ndani ya mama na siyo nje. Mama akila vizuri anachokula kinaenda kwa mtoto na baada ya kujifungua hicho hicho ndiyo mtoto anaendelea kunyonya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo niombe kabisa Mpango huu uonyeshe jinsi gani mama atatuliwa ndoo ya maji ifikapo 2020/2021. Tumelipigia kelele huku Bungeni hata tumeomba iongweze shilingi 50 lakini bado kuna maeneo hayajawezekana. Kuna maeneo ambayo yamefika asilimia 90 nayo ni mjini lakini vijijini maji safi na salama hakuna kiasi hicho. Naomba tunapoelekea kumaliza Bunge hili turudi tukisema angalau tulizungumzia maji na sasa Tanzania nzima ina maji safi na salama na hakuna mwanamke anayejitwisha ndoo umbali mrefu, muda ule wa

kwenda kubeba maji anautumia kulea familia na kwa kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu mazingira. Natamani kuona ifikapo mwisho wa Mpango huu hakuna mwanamke anayepikia kuni, wala mkaa ila wote tunatumia *NLG (gas)* na tupewe mafundisho ya kutumia gesi ili zisije kuleta madhara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tuko hapa tunatamani kusaidika na sisi tukasaidie watu wetu, naomba sana chondechonde viingie kwenye Mpango. Ahsante kwa nafasi hii nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Joseph Roman Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa Charles Kitwanga aijandae.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe maoni kwenye hoja ilio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna mahali tumekosea kwa sababu miaka ya nyuma tulikuwa tunafanya semina Wabunge wote tunapitishwa kwenye Mpango kabla hatujaanza kuujadili. Vilevile tulikuwa tunapewa walau *ABCD* ya tathimini ya Mpango uliopita na yote hiyo ni ili kuijweka sawa tu ili mjadala uweze kunoga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, naomba nijadili kwa kuzungumzia mambo matatu. Jambo la kwanza ni kilimo. Miaka baada ya uhuru tulikuwa hatujaanza kuvuna madini katika nchi yetu na kwa sababu hiyo uchumi wa nchi yetu ulibebwa na kilimo. Mazao ya biashara wakati huo pamba, kahawa, korosho, katani, pareto na kadhalika ndiyo yaliyobeba uchumi wa nchi hii sasa mazao haya yanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sote tutakumbuka wakati wa Mwalimu katika maeneo ambayo mazao haya yalikuwa yanapatikana kwa wingi kulikuwa pia kuna viwanda vya *ku-process* mazao haya. Tulishuhudia *Mwatex*, *Mutex*, *Coffee Curing* kule Moshi na kadhalika sasa vyote hivi vimekufa na sjui nini kilitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri kwa sababu asilimia 65 ya Watanzania wamejilajiri katika kilimo, basi huu Mpango uje na kitu tofauti kuhusu kilimo. Sote ni mashahidi kwenye bajeti tunayomaliza fedha zilizotengwa kwa ajili ya kilimo karibu Wabunge wote tulikuwa tunapiga kelele kwamba ziongezwe katika kilimo, ufugaji, na katika uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha za kutosha zitengwe kwenye kilimo ili kuimarisha miundombinu ya kilimo. Ni muhimu sana tuone kuna mpango ambao uko wazi wa namna ambavyo nchi hii sasa tutakuwa na viwanda vya kutosha vya mbolea. Fedha za kutosha ziingizwe kwenye Mpango tuone ni namna gani sasa tunapata masoko ya ndani na hata ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hivi siyo kwamba nabeza kazi ambayo imeshaanza kufanywa, kuna kazi inafanyika, lakini nachosema liimarishwe ili wakulima wawe na hakika ya kupata kipato cha kutosha na kizuri kutokana na jasho lao. Wewe ni shahidi mzuri sana na Waheshimiwa Wabunge jinsi tulivyohangaika hapa na mahindi, wakulima Sumbawanga, Mbeya na maeneo mengine walivyopata shida ya kuuza mahindi yao. Sasa hivi gunia la mahindi kwa mfano Kaskazini huku imevuka laki moja na kitu, wakati huo huo mahindi gunia yaliuzwa shilingi 20,000, shilingi 25,000 au shilingi 30,000. Sasa tutengeneze utaratibu ambapo kutakuwa hata na *security* kwa mkulima huyu ili wakati mazao yakipatikana kwa wingi awe na hakika basi baadaye kunaweza kukawa na nafuu na yeye akapata kipato cha kutosha kutokana na nguvu zake alizotia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna soko nataka nilitolee mfano, kwa mfano soko la Kibaigwa hapa lilikuwa la Kimataifa watu walikuwa wanatoka Rwanda, Burundi na maeneo mengi ya nchi hii wanakuja kununua mahindi, alizeti na kadhalika lakini sa sahivi linalekeea kufa. Kwa hiyo, masoko ya aina ya Kibaigwa Serikali ingeona uwezekano wa kufanya utafiti masoko haya yawepo katika maeneo mbalimbali kusaidia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda nya kati kama ambavyo vilikuwepo hapo zamani. Nchi hii kuna maeneo ambayo kuna matunda mengi sana kwa mfano Muheza na Korogwe, machungwa ni mengi sana lakini wakulima wanaonewa kwa sababu yanakuja kwa wingi halafu hatuna hata viwanda vidogo vidogo nya kutengeneza *concentrate* za machungwa au kuhifadhi yale machungwa yaweze kutumika kipindi kingine ambacho siyo cha msimu. Hivi vitu hivi ndiyo vinakuza thamani ya yale mazao na wakulima wananaufaika kutohana na mazao yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuongeze fedha kwenye taasisi za kilimo ili ziweze kufanya utafiti wa kutosha kuhusu mbegu bora kwa ajili ya wakulima, tuweze kupata mbegu zinazoweza kuendana na hali ya hewa. Vyuo vingi sasa hivi vinapata shida ya kufanya utafiti kwa sababu fedha zinazoingizwa kwenye utafiti wa kilimo vilevile zinakuwa za mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia tuanze kufikiria kuongeza pesa za kutosha kwenye kilimo cha umwagiliaji. Nchi hii ina maji mengi sana, mvua ikinyesha sote ni mashuhuda kwa mfano barabara hii ya Dodoma maji yamekuwa yanatoka Kiteto na maeneo mengine yanafunga kabisa barabara lakini tungeweza yale maji kuyahifadhi na kuyatumia kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Rombo kwa mfano mvua zikinyesha na sasa hivi Rombo tunapata mvua nyingi sana za vuli, maji yanateremka kutoka Kilimanjaro yanavuka kwenye mito yetu ya asili kule

yanaenda Kenya na kule Kenya wameya-*tape* yale maji. Kuna eneo kule Kenya linaitwa Chumvini, wanalima mbogamboga, nyanya, vitunguu na kadhalika, wanakuja kutuuzia sisi ambao maji yanatoka kwetu. Kwa hiyo ilikuwa ni rahisi tungeweza kwenye makorongo ya ile mito ya misimu tukaiziba namna fulani na mawe yapo ya kutosha tukahifadhi yale maji, baadaye tukayatumia kwa ajili ya kilimo kuendelea kufikiria kuangalia anga mvua zitakuja lini na kadhalika, tutazidi kupata shida na kama nilivyosema nchi hii watu wetu walio wengi wamejajiri katika kilimo na hakika kabisa kwamba kilimo kikiboreshwa kwa namna kubwa sana tutakuwa tumesaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mazao ya biashara kuna mazao mchanganyiko kama mbaazi, kunde, mahindi na kadhalika, tuimarishe pia masoko kwa ajili ya haya mazao, kwa sababu haya mazao yana masoko ndani, yana masoko nje na wakulima wetu wengi wanalima mazao ya namna hii. Kwa hiyo kuhusu kilimo nafikiri nimeongea vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ufugaji, ngombe wetu wanabaki ni ngombe wale wa asili na hapa Bungeni tumekuwa tukizungumza namna ya kubadilisha wale ngombe waweze kuwa bora zaidi na wakulima waweze kufuga ngombe wachache lakini wenyе kipato cha kutosha. Sasa ni rai yangu kwamba Serikali iangalie namna sasa ya mawazo haya kutekelezwa. Zamani kulikuwa na vituo vya uhamilishaji katika baadhi ya vijiji, madume bora yalikuwa yanapatikana kwenye *centre* moja kwa ajili ya kubadilisha ile mbegu kwa ngombe na hata kwa mbuzi. Sasa baadhi ya hizi *centre* zimekufa na hatujui zimekufa namna gani. Kule kwetu *Rombo centre* kama hizi zilikuwa nyingi kabisa mimi nikiwa mdogo, nilikuwa naambiwa chukua ngombe peleka, napeleka, lakini sasa hivi vimekufa. Hivi ni vitu vya kawaida, lakini ni vitu muhimu sana kwa sababu ngombe hawa maziwa na mazao mengine ya maziwa yanasaidia sana katika kipato cha wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hawa ngombe wengi tunaopata Umasaini, Usukumani na kadhalika bado

hatujafanya nya kutosha. Mazao yanayotokana na ngozi, mazao yanayotokana na pembe na kadhalika bado ni shida, wenzetu Kenya hapa wana Kiwanda cha Nyama cha Thika, ngombe wanatoroshwa kupitia mpaka wa Loliondo, wanaenda wanachinjwa Thika na matokeo yake nyama inabaki huko, ngozi inabaki huko na kadhalika. Kama nchi hatujashindwa kujenga kiwanda cha kisasa cha kimataifa kinachohusiana na mazao ya mifugo, tunaweza kwa sababu kama mengine yamewezezana kwa nini hili lishindikane na likifanyika ina maana tunawasaidia wakulima na wenyewe wanapata faida kutokana na kazi wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uvuvi. Sasa hivi watu wamehamasika kufuga samaki na mimi nina diwani wangu mmoja ambaye amesoma hapo Sokoine anawafundisha watu namna ya kujenga mabwawa wanafuga samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hata Waziri Mheshimiwa Mpango ana bwawa lake kubwa sana la samaki, ndio mimi najua hatujafahamiana barabarani na huyu mzee, ana bwawa kubwa sana la samaki. Sasa uangaliwe uwezekano wa Watanzania kufundishwa namna ya kufuga samaki kwa sababu watapata kipato kibashara vilevile wataongeza afya zao, manaa yake tukizungumza samaki tunazungumza samaki wa baharini na kwenye maziwa yetu makubwa tu, lakini Watanzania wanawenza wakafuga samaki kama sehemu ya ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tuangalie uvuvi wa bahari kuu tumeiongela sana hili. Uvuvi wa bahari kuu unawenza ukatuletea kipato kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ambalo ningependa kuzungumza pia bajeti iongeze fedha za kutosha katika miradi ya maji. Huwezi kuamini sisi tuna ule mlima, chemichemi zilikuwa nydingi sana, lakini na vijiji karibu 41 havina hakika ya maji, yaani kilio cha maji ni kikubwa katika Jimbo langu la Rombo kuliko kitu kingine chochote. Nashukuru kuhusu umeme bado vitongoji kadhaa, lakini kuhusu maji

shida ni kubwa sana naomba Mheshimiwa Mpango atakapokuja bajeti yake katika miradi ya maji iimarishe kwa sababu kwa kweli maji ni uhai na kelele nyingi sana za Watanzania sasa hivi unaona hapa kila Mbunge akisimama anazungumza kuhusu maji katika eneo lake. Nadhani kama tukiweza kukazana kwenye maji kama tulivyokazana kwenye mambo mengine sasa watu wanaweza wakafikia mahali wakatulia na wakafanya mambo yao sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Julius Kalanga atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba ajiandae.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapendelekezo ya Mpango kwa jioni ya leo na nimshukuru sana Mungu kwa kutupa kibali tena cha kukusanyika mahali hapa. Pili nkipongeze sana Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kwa kuendelea kutekeleza shughuli zake kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendelekezo ambayo tumeyasoma na tunampongeza Mheshimiwa Waziri, mimi naomba leo jioni hii nijikite katika maeneo makubwa matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba uchumi wa nchi yetu unakua na miradi ya kimkakati inatekelezwa na kazi zinaonekana, lakini ni ukweli pia kwamba tunalo tatizo kubwa la ajira nchini. Mheshimiwa Waziri kama anakumbuka kabisa kwamba Serikali kama Serikali haiwezi kuajiri Watanzania wote yenyewe, lakini ajira tunayozungumza leo ni ajira ya sekta binafsi. Mheshimiwa Waziri pia anafahamu kwamba mabenki mengi yameweka masharti ya upatikanaji wa mikopo ili wananchi wengi waweze kujajiri katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika eneo hili, unajua Serikali inapeleka karibu bilioni 23 katika kutoa elimu bure katika maeneo yetu na katika historia ya nchi yetu karibu kila kata ina shule ya sekondari na katika shule hizi za sekondari kinachopatikana kule ni chakula, chumvi, nyanya, mahindi na maharage ambapo wananchi wetu ndio ambaao wanalima katika maeneo yale. Hata hivyo, ukiangalia pamoja na Serikali kipeleka pesa shughuli hizi zinafanywa na wafanyabiashara wakubwa. Mheshimiwa Mpango ni muhimu tukaiona kama tunapeleka fedha katika shule ambazo wananchi wamejenga wenyewe unaachaje kuwapa vikundi vyta akinamama na vijana ambaao wako kule vijiji wafanye shughuli hiyo unawapa wafanyabiashara wakubwa wanafanya hata biashara ya chumvi. Hao vijana wanaotoka katika vyuo vikuu ambaao hawana ajira watapataje ajira kama hata Serikali haiwezi kuwasimamia katika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo ambalo Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana tukalitazama kwamba haiwezekani tunatengeneza vikundi vyta ujasiriamali katika maeneo, tunatenga ile asilimia 10 ya halmashauri lakini hata mahali pa kufanya biashara na Serikali yake hakuna. Kwamba hata chumvi vijana wale hawawezi kipeleka, hata *stationary* vijana wale hawawezi kufanya. Kwa hiyo, nafikiri katika hili mpango huu wa fedha za elimu bure ambazo zinaenda katika shule zetu za kata, Serikali iweke utaratibu ambaao wale wananchi na vijana ambaao wamejajiri katika vijiji wafanye shughuli zile ambazo wao wanaweza waka-supply ikiwepo chumvi, sukari hata ikiwepo basi upelekaji wa maziwa, nyama na vitu vingine ambavyo vinapatikana katika jamii yetu. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia vijana wetu ambaao wanamaliza vyuo ili wapate shughuli za kufanya katika maeneo yao na wakakuza uchumi wao. Tusipofanya hivyo haitawezekana kuwasaidia vijana ambaao tunaona kuna tatizo kubwa la ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hili tatizo la maji nchini, nafikiri tatizo sio fedha na unajua kwamba Serikali inapeleka fedha nyingi sana katika miradi ya maji, lakini tangu uhuru

wa nchi hii pamoja na miradi mikubwa ya maji ambao imetengenezwa na Serikali haijawahi kupunguza tatizo kubwa la maji kwa kiwango hicho. Ni kwa nini? Ni kwa sababu miradi mingi ni hewa na haitekelezwi kwa kiwango kinachostahili kutekelezwa. Naiomba Serikali kabla ya kufanya mipango mingine ifanyie *auditing* ya miradi yote ya maji nchini kama ambavyo nimewahi kushauri ili tujue kwa nini tunapeleka fedha nyngi katika miradi ya maji, lakini tatizo la maji halipungui nchini. Hili ni tatizo kubwa sana, miradi ya kwanza inakwisha, lakini ikianza miradi mingine ile ya awali inakufa na haitoi maji. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ipate nafasi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo linafanyika ni kwamba anayefanya tathmini ni Wizara ya Maji ambaye ndio mtekelezaji wa miradi, halafu unampa akafanye tathmini mwenyewe, unamwagiza Waziri akafanye tathmini, wataalam wale wale waliokeleza miradi ndio wanafanya tathmini, hii haikubaliki. Ni muhimu katika hili tukafanya tathmini, kwa nini tatizo la maji nchini halipungui pamoja na kwamba Serikali inapeleka fedha nyngi katika maji, lazima tuone tatizo liko wapi katika utekelezaji wa miradi yetu. Aidha, ni miundombinu tunatengeneza vibaya au kuna uchakachuaji mwingi wa fedha katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kushauri katika eneo hili pia tujifunze Wizara ya Afya na TAMISEMI kwa kutumia *force account* ili fedha nyngi ziende kwenye shughuli za maji. Miradi mingi ya nchi yetu ya maji hakuna mradi unaoshuka chini ya bilioni moja, haina maana kama miradi ni ghali hivyo lakini wakandarasi wengi katika mfumo ule wa manunuzi, fedha nyngi zinaenda kwa wakandarasi na maji hayaendi kwa wananchi. Kwa hiyo naomba ikiwezekana tutumie *force account* katika kupanga mipango kwa mwaka unaokuja ili maji yaweze kupatikana katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la mwisho ni tatizo la masoko ya mazao ya kilimo na mifugo. Wenzangu wamezungumza, lakini hivi ni kweli kwamba wananchi hawazalishi, la hasha! Hivi ni kweli hatuna mifugo bora, la

hasha! Hivi ni kwamba wananchi hawazalishi pamba, la hasha! Tatizo kubwa ni upatikanaji wa soko la mazao hayo, kwa hiyo wananchi wetu wamekata tamaa katika kuzalisha. Naamini kama Serikali itaamua ikawekeza nguvu kubwa katika upatikanaji wa masoko katika mazao yanayotokana na wananchi wetu naamini kila mtu atazalisha kwa kiwango kinachotakiwa. Leo unakuta mtu anazalisha pamba, watu wanasema hiyo mikoa 17, lakini pamba inaoza nje, yule mwananchi mwakani ni lazima atabadiilisha zao ataanza kuzalisha zao lingine, lakini kama tungekuwa na soko la uhakika la pamba kila mwanachi angezalisha kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kwa sasa iweke nguvu kubwa katika maeneo ya kupatikana masoko ya uhakika ili wananchi wetu waweze kuzalisha kwa tija na kiwango kinachotakiwa. Ndio maana tunasema hata katika mifugo watu wengi wanahangaika kuhamisha mifugo na kusafirisha nje kwa kuvunja sharia, lakini kama tungekuwa na viwanda vya kutosha nchini vya mazao yanayotokana na mifugo kama viwanda vya maziwa, viwanda vya ngozi, hakika leo tusingekuwa tunapata watu wanaosafirisha ngozi kupeleka nje. Hivyo, kwa sababu masoko hayapatikani nchini na viwanda havipo ndio maana uzalishaji unakuwa mchache na watu wanatorosha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuacha nchi yetu na wafugaji wetu na wakulima wakajihangaikia soko wenyeve wakati Serikali yao ipo. Ni lazima kama ambavyo tumewekeza katika miradi mingine mikubwa tuwekeze katika upatikanaji wa soko kwa ajili ya bidhaa na mazao ya kilimo kwa wananchi wetu tukifanya hivyo wananchi wetu watazalisha. Kwa hiyo naomba katika mpango unaokuja Serikali iweke mkakati na itueleze bayana kwamba ni kwa namna gani unamhakikishia mwananchi kwamba akizalisha, akilima pamba atapata soko la pamba, akilima kahawa atapata soko la kahawa. Tusipofanya hivyo kila mwaka tutakuwa na tatizo la uzalishaji kwa sababu mtu anaona kwamba zao hili halina soko, anaacha kuzalisha. Kwa hiyo Mheshimiwa Mpango hili ni eneo ambalo ni lazima

tuhangaike, tusipofanya hivyo tutakuwa hatuwasaidii wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndege tunazonunua, tunaipongeza Serikali kwa kununua ndege, kama hatutakuwa na shughuli zinazowasababisha wananchi wetu kutumia ndege hizo, hizo ndege hazitazalisha, lakini kama tutaendelea kuwa na shughuli ambazo wananchi wana-move kutoka sehemu moja kwenda nyngine lazima lile Shirika la Ndege litakuwa na ndege zetu zitaonekana za maana. Ndio maana nilikuwa nawaambia watu huwezi kufanya utalii bila ndege kwa sababu mtu akishuka Dar es Salaam ni rahisi kusafiri kwenda Arusha kwa ndege na yule anayefanya biashara lazima aende huko. Kwa hiyo lazima tuone kwamba faida za zile ndege ni kuwasaidia pia Watanzania kutoka sehemu moja kwenda nyngine kufanya biashara na moja ya biashara wanazofanya ni pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hakuna mzunguko wa fedha za shughuli anazofanya, shirika hili litakuwa haliwanufaishi Watanzania. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mpango katika mpango unaokuja tuhakikishe basi kwamba masoko ya mazao ya wakulima yanapatikana ili ndege hizi tunazozinunua wananchi wasafiri wakauze mazao nje, wasafiri Dar es Salaam waende Mwanza na kwingine kwa sababu kuna biashara inayozunguka. Kama hakuna upatikanaji wa soko la uhakika hizi ndege hazitawasaidia watu wa chini na hakika ina maana kwamba haitakuwa na faida kwa mtu mmoja mmoja. Kwa sababu tumeshajenga miundombinu rahisi sasa ya upatikanaji wa ndege, barabara zinajengwa, ni lazima sasa tuwajengee wananchi wetu uchumi kwamba katika barabara hizo waweze kusafirisha bidhaa zao na pia wapate masoko. Kwa hiyo Mheshimiwa Mpango naomba katika eneo hilo tujitahidi sana ili na eneo hilo lipate suluhu la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho, ni namna ambavyo biashara zetu zinakwama nchini. Naomba nitoe *challenge* kwenye Bunge na kwa Serikali, kwa nini tusifanye tathmini kwa miaka mine, hii ya biashara nchini, ni

wapi tumekwama na tufanye nini ili basi tuweze kuendelea mbele na biashara zetu. Tunaangalia hapa upatikanaji wa mikopo binafsi imepungua kuliko mategemeo ya Serikali na kwa nini tunaona hata mabenki mengi mikopo imepungua. Lazima kama Serikali itusaidie Watanzania tufanye nini ili biashara zetu ziendelee kunawiri tusiendelee kukwama kama ambavyo tunaona. Kwa sababu tunaonekana kila mwaka hatufanyi vizuri, lakini tathmini yetu inatuelekeza nini kinatukwamisha katika biashara, mzunguko wa fedha unaonekana sio mkubwa sana, watu wanalamika lakini ukweli biashara zinafanyika. Kwa nini tusifanye tathmini kuangalia ni nini ambacho kimekuwa kikwazo hasa katika biashara. Kama barabara zipo, kama miundombinu rafiki ipo, kama *blue print* ipo, ni kwa nini bado biashara zetu hazijatengemaa vizuri. Nafikiri katika mipango inayokuja ni muhimu sana Serikali ikafanya tathmini katika eneo hili kwa namna ambavyo inaweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naipongeza sana Serikali, lazima tutembee kifua mbele kama Watanzania, miradi hii mikubwa inayofanyika ikiwepo ndege, barabara, ni kielelezo tosha kwamba nchi yetu inaenda kwenye mwelekeo mzuri sana. Wale unaowaona wanaopinga hilo ni kwa sababu tu wana chuki zao binafsi, lakini kazi tunailona, Mheshimiwa Mpango kazi yake ni kubwa, anamsaidia Rais na sisi Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wenyе nia njema na Taifa hili tupo nyuma yake kumsaidia Rais na kumsaidia ye ye maana uchumi huu anaoujenga si uchumi wake, ni uchumi wa Taifa letu hili na akila adui wa mipango ya Serikali ambayo ni ya kujenga uchumi, lazima wote tuwanyooshee vidole na kusema hapana haiwezekani katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachowaomba hawa ambaa wanatuongoza wazibe masikio, wasonge mbele, nchi yetu inaelekea kwenye mwelekeo, Rais anafanya kazi nzuri, nchi yetu ina maadili mazuri sana, miradi ipo na kazi inaonekana na kila mahali duniani Rais wetu anapongezwa kwa kazi nzuri. Tunachowaomba wasirudi nyuma, wasonge

mbele kumsaidia Rais ili kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makof)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kitwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Salim Hassan ajiandae.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika ajenda hii iliyoko mbele yetu. Tuanze kwanza kwa kutazama uchumi wetu na jinsi tulivyojipanga. Sisi sote tunatambua kwamba tuna *vision 2025* na hii *vision tukakubaliana kwamba tutai-cascade in five years plans*. *Plan* ya pili tullonayo leo hii ni *plan* ya kuipeleka nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda. Sasa tunafikaje pale kwenye uchumi wa viwanda Mheshimiwa Mpango pamoja na timu yake wameweka vizuri katika hotuba yao na katika maelezo ambayo tumeyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunaitafsiri vipi na kuielewa na kuhakikisha kwamba *ina-add value* na kumwezesha kila Mtanzania aweze kusema kwamba yuko kwenye uchumi wa viwanda na anaishi maisha bora kuliko alivyokuwa zamani. Tuangalle kwanza nchi yetu imeajiri au watu wetu wanashughulika na kitu gani kwanza, asilimia kubwa. Tukiangalia tunakuta kwamba wananchi wengi wanashughulika na kilimo. Sasa viwanda vyetu vingi vielekezwe wapi na tutambue kwamba kuna viwanda angalau *nya three categories*; kuna viwanda vikubwa, mahitaji yake ni tofauti; kuna viwanda nya kat, mahitaji yake ni tofauti; na kuna viwanda vidogo ambavyo vitawezaka kuajiri au kuwafanya wananchi wa kawaida washiriki wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyote hivi vinahitaji mazingira yanayoelewaka. Nirudie tena nilishawahi kusema katika eneo letu la kwanza kabisa ambalo tuli-*invest heavily* lilikuwa ni eneo la madini, mwekezaji anapokuja kwenye

madini anachukua madini anahama nayo, tukawapa *incentives* za kutosha wakaendelea wakawekeza kwenye madini. Sasa hivi tuko kwenye viwanda, viwanda hivi vinatakiwa vipewe *incentives*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kitu kimoja tu. Mtu ye yote atakayekuja hapa atakuta ardhi, atakuta wananchi ambao watashiriki, atakuja na *expertisen*a *capital*. Baada ya kujanavyo hivyo vitu, atajenga kiwanda. Sijawahi kuona hata mtu mmoja amejenga kiwanda akakibeba. Tuseme kwa mfano ametoka London, akakibeba akaendanacho London. Tuwepe *incentives* hawa watu wajenge viwanda, hawatavibeba kutoka hapa kwendanavyo London. Madini tuliwapa *incentives*, wakabeba wakaendanayo leo tuna mashimo baadhi ya sehemu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitze sasa hili la kilimo. Kwanza naipongeza Serikali, inaweka miundombinu kwa ajili ya kupata umeme. Je, huu umeme mkubwa tunaoujenga kama hatuuwezeshi kuwa na viwanda vya ku-*consume* huu umeme, si tutaanza kuu-*export* huu umeme badala ya ku-*add value* ndani na kusababisha watu wakapata ajira; watakapata ajira watalipa *Pay As You Earn* na zile pesa zitazunguka mifukoni mwa wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokuwa na kilimo, nichukulie mfano mzuri tu wa pamba; enzi ya Mwalimu pamba ilikuwa inanunuliwa na Vyama vya Ushirika na Vyama vya Ushirika vilikuwa *heavily subsidized*. Tulikuwa na viwanda (*generies*) vya katni tulikuwa na viwanda vikubwa vya nguo. Vyote hivi vilikuwa kwa nini? Hebu angalieni leo China; wengi tunavaa nguo kutoka China, wengi tunavaa nguo kutoka India. *Policy* yao kuhusu viwanda vya nguo ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwa na kiwanda cha nguo bila Serikali kuwa *involved in one way or another*. Kwanza kumbuka kwamba unahitaji *a minimum* ya kama dola milioni 50 ili uweze kununua *raw materials* ambayo ni pamba uweze ku-*run* mwaka mzima. Pamba ile utaihifadhi

kwa mwaka mzima, kwa sababu, utakapokuwa unanunua pamba, ni msimu na sana sana ni miezi mitatu, baada ya miezi mitatu msimu umefungwa. Je, hiyo pamba utakayostahili kuwanayo kwa mwaka mzima, si lazima uwe na *capital* ya kutosha? Sasa kama una hela zako nydingi, na huwezi kuwa na *cash money*, itabidi ukakope. Kama unataka kukopa, hiyo *interest rate* ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufikirie, leo hii kama kila Mtanzania anaevaa nguo kutoka China, asivae nguo kwa ku-save dola 10 tu, Watanzania wote, tuko milioni ngapi? Tuko milioni 55, lakini dola 10 tu kila mtu a-save anunue nguo ya hapa ili hiyo dola 10 izunguke kwenye uchumi wetu, tutakuwa tumezungusha hela kiasi gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela hizo zitakapokuwa zimezunguka, si zitanunua vitu vingine ambavyo vimelipiwa ushuru? Ushuru huo utaupata kutokana na hiyo dola 10 kuwa imezunguka kwenye uchumi wako ukaweza kuwezesha uchumi wako kukua. Kwa nini hawa watu wenye viwanda vyta nguo wasipewe *tax holiday* au *incentive* kubwa hata ya ku-save dola 10 tu kwa kila nguo? Hilo ni jambo la kutazama. Tutazame: Je, watu wangapi watakuwa wameajiriwa kwenye viwanda vyta nguo? Angalia *MWATEX*, *MUTEX*, *KILTEX* na kila mahali ambapo kulikuwa kuna viwanda kama hivi, vilikuwa vinaajiri watu wangapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka *MWATEX* wakati ule kilikuwa kinaajiri zaidi ya watu 1,000. Wacha hapo, wako wale wa kutengeneza zile nyuzi. Viwanda vile vyta kati vyta kuchambua pamba; kulikuwepo sijui Bukumbi, Buchosa, sijui wapi, kulikuwa na *generykaribu* 20; katika hiyo ilikuwa inaitwa *Victoria Federation* kwanza halafu ikawa *Nyanza*, ikaja *SHIRECU* na sehemu zote zile. Zote hizo leo hazipo. Maana yake wale wafanyakazi hawapo na kwa sababu hiyo sasa hakuna *Pay As You Earn* na kwa sababu wale wafanyakazi hawapo, hawana hela ambayo itawawezesha kusaidia kiwanda cha chumvi Uvinza kwa sababu wangeweza kununua chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie ile *trickledown* na jinsi ambavyo tunaweza tuka-affect. Kwa hivyo, mipango yetu iangalie wapi tu-invest, wapi tutoe msamaha ili tuwezeshe viwanda vyetu na watu wetu waweze kupata faida kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu, najua rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango una akili sana na Naibu wako, hebu panueni zaidi tuione hivyo na muishawishi Serikali yote kwa pamoja, tuweze kuangalia ni kwa namna gani sasa tutatoka tulipo tuweze kweli kuwa nchi ya viwanda? Hatuwezi kuwa tunaimba tu bila kuangalia watu wengi ambaao wanaguswa na eneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie labda tena eneo la *service au transport*. Tunajenga *SGR; very good plan* na *very long looking* kama ambavyo Wajerumani walikuwa wanajenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza na kote walikuwa wanakwenda kuchukua *raw materials*. Sasa uchumi umebadilika, tunahitaji kujenga reli hii ili ituletee faida. Hatuwezi kujenga reli kwa ajili ya abiria wa kibinadamu tu, tujenge hii reli tukiwa na *thinking kwamba*, reli itakapofika Mwanza iweze kutusaidia kubeba mizigo yetu tuweze *ku-export* au tuweze kupeleka *raw materials* kwenye viwanda vidogovidogo ambavyo vimeajiri watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna daraja zuri sana, natumaini litaanza kujengwa hivi karibuni pale Kigongo - Busisi. *Very good decision again*. Watu sasa hivi kwa sababu ya usafiri kutoka Kigongo kwenda Busisi, wakati mwingine malori yanajipanga kuanzia saa sita mchana linakuja linavuka saa sita usiku. Hayo ni masaa 12, lakini kama tutakuwa na lile daraja, litatumia dakika nne tu kutoka Kigongo kwenda Busisi na kuendelea na safari zake. Tutakuwa tume-save time na tutakuwa tumemwezesha huyo mtu kufanya *business haraka* zaidi. Sasa tu--add value kwa sababu vilevile pale Fela kutakuwa na *dry port*. Hatuwezi tu tukawa tunaleta mizigo inayotoka nje tukaiweka pale Fela halafu wananchi kutoka DRC, Burundi, Rwanda na Uganda wanachukua mizigo kutoka bandarini na kupitisha pale kwenye daraja. Lazima

tuwe na mpango mkakati wa kujenga maeneo ya biashara kubwa, *business centres*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana pale kuwe na *business centre* kubwa, vifaa badala ya watu kwenda kununua Guanzhou watu walete au tuwashawishi wale wanye maviwanda kule Guanzhou walete pale Mwanza au eneo lolote karibu hapo. Sasa nguo au vifaa vyote vinavyoletwa pale vipewe *tax free*. Vikiwa *tax free*, Mtanzania unapokwenda kununua pale unalipia ushuru, unachukua vile vifaa vyako unaweza kuvitumia. Mtu anayetoka Rwanda, Kongo, Burundi nakadhalika akinunua pale, anapeleka Rwanda bila *tax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho mimi nakiona tuna shida kubwa ya uwoga na vilevile tuna shida kubwa ya kuona kama tutaibiwa. Tupige *brain*, tuweke *control*, tuweke *system* ambazo zitatuzezesha leo hii vifaa vinapokuwa hapa, unakuwa unaviona kwamba, huyu ameleta mizigo ya dola 1,000,000. Katika mizigo ya dola 1,000,000 labda 500,000 ameziuza *locally*, 500,000 amezi-*re-export* baada ya kuwa ame-*import*, lakini kwa sababu tuna wasiwasi inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu, tulikuwa na wasiwasi kweli kutumia hata hii. Tulyapenda sana makaratasi, lakini leo hii *you could see* hapa kwenye meza zetu. Meza zetu ni safi, hazina matatizo *and you will save a lot of money*, tume-*dare*. Rais wetu ni *very daring, let all of us be daring*. Tu-*dare* kufanya, tukifanya makosa, tumwambie hapa nimekosea, nipe nafasi. Kama anaona hawezikukupa nafasi, akutumbue, halafu tuendelee mbele, mwingine atakuja. Naye kama ni *daring*, mwishoni ataona hawa wamefanya hivi kwa nia njema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie *tourism*. *Tourism again* nimeionta hata humu kwamba tunanunua ndege tunaimarisha *Air Tanzania*, *very good, brilliant* na matokeo yake tunayaona na *trickledown again* nimeshaizugumza. Ndege zetu sasa zinaruka kwenda Mumbai na Watanzania

wanaleta mizigo, zinakuja na watalii, watalii wanakwenda kwenye mbuga. Watu kwenda kwenye mbuga hawaendi na ndege, wanaenda na Landrover ambazo zinaendeshwa na Watanzania. Wakifika Mlima Kilimanjaro kwa rafiki yangu Mheshimiwa Selasini, wale wanaozunguka ule mlima wanakuwa wapagazi, wame-*gain* wanapanda kwenda Mlima Kilimanjaro. Hiyo ndio *trickledownya* uchumi na ndege zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusiishie hapo. Wenzetu wa ATC wana mpango wa mpaka 2021, *let us look beyond that*. Tumeleta *Dreamliner 8* mbili, *let us think of having Dreamliner 9* mbili nydingine za *market* ya kwenda Israel na Ufaransa. Watu wengi wanaokuja hapa; sasa hivi ukiangalia, nilikuwa naangalia kwenye *TV* naona jinsi Waisrael wanavyokuja wengi na wanalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nina rafiki zangu wawili watatu kule, walikuwa naniambia, hivi nchi yenu inashindwaje kuwa na *flight* angalau mara tatu kwa wi ki kuja Israel ili zitupunguzie gharama? Kwa sababu tunapokuja Tanzania, ndege tunazokujanazo tuna-*charter* mandege makubwa, *it becomes very expensive* kwa sababu anaenda mara moja, akirudisha, basi anaendelea kule, anaanza kutafuta *market* nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tutakuwa na *three times per week* labda kutoka Tel Aviv na pale Israel kuja hapa, tutapata watalii wengi zaidi. Kwa hiyo, *we should not be afraid, let us dare again to bring Dreamliner 9* mwaka 2023 mwaka 2024. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa biashara ya ndege, ndege hainunuliwi hivi hivi. *You buy a slot: Unapo-buy a slot* wanaweka kwenye kiwanda jinsi ndege zinazyokwenda kama inafikia *time* yako ndiyo ndege inatoka. Kwenye kiwanda kama umeweka, wana-*plan* vizuri kwamba, itakapofika wakati wa kuweka *engine, engine* itakuwa imetolewa *Rollsroyce* imefika kwenye kiwanda inafungwa pale. Pale itakapofika, wewe ndio unahangaikahangaika,

inafika wakati wa kuwekewa *engine*, *engine* hazipo, huwa hawasubiri. Inapita, *engine* itakwenda ifungwe huku pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu ndugu zangu hapa wakati fulani wakati tunaleta ile *Dreamliner 8* ya kwanza kwa sababu tuliinunua haraka haraka *time* ya kuiwekea *engine* ilikuwa imeshapita, *slot* yake ikawa imepita, *engine* zikafungwa nje watu wakaanza kusema aah, mmenunua ndege ambazo zina *engine* siyo za *Rollsroyce*, kumbe ile tumenunua *slot* ilikuwa ni *too short*, muda ukawa umepita wa kufunga zile *engine* zikafungwa badaye. Hivi, hamkuona aibu siku zinafika hapa na zina *Rollsroyce*? Hao ninaowasema wanajijua. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie umeme. Umeme tulionao sasa hivi *we are looking at 2,150 Megawatt, very shortly*, lakini kwa nchi kama ya kwetu kama kweli tutafuata mipango tuka-*plan* kama ninavyoshauri, huo hautatosha. Lazima tuwe na *mixture*. Maji yakikauka kama inatokea, siombei hilo, lazima tuwe na *alternative*. *We should be thinking again* kwenye mipango yetu ya viwanda hii, tuwe na umeme mwingine mkubwa wa *level* ya *at least three thousand, five thousand Megawatt* za makaa ya mawe. Leo hii tukianza kutengeneza, kufua vyuma hapa, umeme unaohitajika siyo huu mnaozungumzia. Kiwanda kimoja kinaweza kikahitaji *200 Megawatt* na ndivyo hivyo viwanda vikubwa tunavyovizungumzia. Hapa mliokaa mbele, kaeni kwa pamoja, chakateni, tusitoe nafasi kwa watu ambao hawana *environment* nzuri kama sisi kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja, kuna kiwanda hapo nchi jirani sitaki kuitaja, nyuma yake kimeandikwa *his excellence something her*, halafu mwisho kuna e; wamejenga kiwanda na kilikuwa kijengwe hapa. Kinachonuma zaidi, sasa hivi wanatengeneza magari ya kutumia umeme nchi hiyo na hao watu *I brought them here*. *The bureaucracy we have in our system is so bad*, mwishowe wakaenda Rwanda. Volkswagen sasa hivi zinatengenezwa

Rwanda, ilikuwa kiwanda kijengwe hapa. Hebu tupunguze hiyo *bureaucracy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kwa kumalizia, anayejenga kiwanda hapa, hatakinyanya kwendanacho. Hebu punguzeni hizo *bureaucracy*. Kama ataleta figisufigisu na kutaka kutuobia, hatakibeba, mwondoeni, wekeni watalaam wengine, Watanzania watakuwa wamejifunza, wataendeleza hicho kiwanda. *It should not take six months to discuss issue ya kiwanda.* Anaambiwa nenda hapa, nenda hapa, nenda hapa. Hivi kwa nini wenzetu wana-discuss mara moja mara mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I have so many bad experiences* ya kuleta wataalam au viwanda hapa halafu mambo yanakuwa hivyo hivyo, tubadilike. *We should be business minded* halafu wote tutumie *coconut*; wote humu ndani. Nilikuwa namsikiliza Waziri mmoja kwenye Baraza la Obasanjo, Mnaigeria, anazungumzia jinsi ambavyo tunasitasita na jinsi ambavyo hatuwezi kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukeni, dakika moja ikipita, ukitaka kuirudisha nenda kaburini. Utaikuta kaburini umeshakufa, kwa sababu ikishapita unasogea kaburini, ikishapita dakika nyingine unasogea na wote jinsi tunavyosherehekea mwaka mpya, yaani sherehe za kuzaliwa, kumbuka unasogea kaburini. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Wahesnimiwa Wabunge, tutamalizia na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia mpango ulioko mbele yetu. Nianze tu kwa kuipongeza Serikali na sisi wenywewe kama Wabunge kwa sababu hii mipango

yote imekuwa ikipita mikononi mwetu hapa ndani ya Bunge na wote tumeitendea haki katika kuichangia

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko Kamati ya Bajeti, tumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na ofisi nzima kwa ushirikiano mzuri waliotupa na maelekezo na ndani ya mjadala ule yalikuwa ni mengi tumeyaongea, lakini kwa kweli naishukuru Wizara inafanya kazi nzuri na wako *very responsive* katika masuala yetu katika vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu ya kusema. Tukiangalia viashiria vya uchumi, kwa kweli ni hakuna namna zaidi tu ya kuwapongeza kwa sababu dalili za viashiria vya uchumi vyote viko vizuri na tunaenda vizuri. Ukuaji wa uchumi kulingana na malengo yetu ni kwamba ifikapo mwaka 2021 tunataka uchumi wetu ufile asilimia 10. Sasa hivyo ni mwaka 2018/2019 tumefika 7%, tuna-*gap* ya 3% pale ambayo nahisi kwamba tunaenda vizuri, *progress* iko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye mfumuko wa bei, bado tuko chini, sasa tumefikia asilimia 3.2 ambayo kwa kweli tunaona tunaenda vizuri. Hata hivyo, hapa ni lazima tuangalie, pamoja na kwamba tunaminya ule mfumuko wa chakula usiwe mkubwa ambapo unachangia kwa asilimia zaidi ya asilimia 28 sasa ni vizuri tuone, kwa sababu hapa inaonyesha kwamba kwa wawekezaji inawapa *mileage* nzuri kwa sababu *they can plan*. Vilevile kwa wazalishaji inaonyesha kwamba bei haibadiliki kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri wataalam waioanishe na riba tunazopipata kwenye mikopo. Kama *inflation* ya 3.2 siyo kubwa, vile vile na riba za kupata mikopo ili uweze ku-*invest* għarama zako na kupata faida, ni vizuri sasa pale wachumi muweze kutuchanganulia ili tuweze kuipata vizuri. Inaonekana kwamba huenda faida ya kuzalisha inakuwa ni ndogo kwa sababu mfumuko nao umebana sana, kama *interest rate* ya kwenye mabenki hujaibana vizuri. Kwa hiyo, hapo napo wataalam wetu wa mipango mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Sekta ya Kilimo, *target* yetu ni mwaka 2021 tunataka ukuaji uwe wa 7.6%. Sasa hivi tumefika 5.3%, tunakwenda, lakini Mheshimiwa Waziri wa Mipango tuangalie kwa kina ukuaji huu wa kilimo ambao unaajiri watu wengi hebu mkae mfanye *retreat* mwone ni wapi tunakosea? Kwa nini huu ukuaji usipande? Kwa sababu lengo letu tunataka tufike 7.6. Tutakapofika 7.6 kidogo mwananchi ataanza kuona pato kwenye mfuko wake. La sivyo, kama hatuwezi kwenda kwa namna hiyo na ku-*invest* na kutoa fedha kwenye vipaumbele vya Wizara hii, ukiangalia *trend* ya utoaji wa fedha kwenye za maendeleo kwenye kilimo saa nyingine hatufanyi vizuri, kwa hiyo lazima twende sasa tuweze kuwekeza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi za mazao ambazo zinashughulika na kilimo cha wananchi wetu ni vizuri na ninashauri kwamba kwa kuwa sasa Serikali imeweka macho na Waziri Mkuu yuko huko kwa ajili mambo ya ushirika, tuongeze nguvu, tusipunguze nguvu ili wakulima wetu wawze kufaidi matunda yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija sasa kwenye mpango wenye kwenye ukiangalia mpango wetu kila kitu ambacho kinafanywa na Serikali ya CCM nchi hii, kiko kwenye mpango; lakini utakuta watu wanabeza au kuona kwamba hiki kitu ni kipywa, hakikuwepo kwenye mpango. Mheshimiwa Waziri nakuomba, elimu ya mpango wowote tunaoutoa inaonekana haufiki kwa watu. Kitu kikija wanaona kwamba Serikali imekurupuka, hakikuweko kwenye mpango. Sasa ni vizuri bajeti ya kutoa elimu kwa ajili ya kuelimisha wananchi kwenye mpango, aidha Wizara yako, Kitengo chako kile cha Mpango ukipe bajeti kiwe kinaeleza mipango ya Serikali kwa kila sekta kwa miaka inayokuja ili wote tuweze kwenda pamoja. Inaonekana bado kuna *information gap* kati ya wananchi na mpango wenye.

Mimi bado naijuliza kitu kimoja, naipongeza Serikali, mnatoa fedha nyingi na zinaenda kwenye miradi, lakini utakuta mwenge wa uhuru ukipita kwa dakika tano kwenye mradi wanagundua kosa. Mwenge ukipita kwa dakika tano

kwenye eneo lako, wanagundua kosa. Wizara walikuwa wapi? Wataalam walikuwa wapi? Mkuu wa Wilaya alikuwa wapi? Mkuu wa Mkoa alikuwa wapi? Waziri mhusika wa sekta alikuwa wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vitu tunaweza tukaendelea kusema kwamba tuna fedha nyingi lakini kumbe miradi yote tunayoipelekea fedha inakuwa haina tija. Kwa hiyo, naomba kwa kweli tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tilitunga Sheria ya Uhujumu Uchumi, sasa itoke kwa wafanyabiashara, iende sasa kwa wataalam. Wahujumu uchumi wawe ni wataalam ambao hawasimamii miradi vizuri. Fedha hizi zinakusanya kwa wananchi kwa nguvu kubwa na tunatoa kodi kubwa, hii sheria sasa iingie maofisini, Waziri ajikute naye ameingia kwenye uhujumu uchumi, kwa sababu hakusimamia fedha alizozipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nirudi kwenye miradi hii ya kawaida. Mheshimiwa Waziri ulikopa fedha Euro milioni nane za maji katika mikoa ya Kigoma. Ubelgiji walitoa hizo fedha lakini miradi ile nayo haiendi. Sasa tukuulize na utuambie: Je, zile fedha zimeshatoka au imekuwaje? Maana yake miradi halendi na hakuna kazi yoyote inayofanyika. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli uangalie hiyo miradi ya maji ambayo mmekopa fedha Euro milioni nane ili tuweze kwenda vizuri na miradi kote ilikopangwa iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya *PPP* haitoshi Tanzania. Tunacho kitengo kizuri sana pale Wizara ya Fedha ambacho kinachushughulika na miradi ya *PPP*. Miradi ile tunaisoma kila wakati, hakuna kitu kinachofanyika. Tangu nimeingia Kamati ya Bajeti miradi ile inaletwa kwetu, tunaisoma, inachakatwa inafanyiwa nini, hakuna kinachoenda. Lazima *PPP* ifanye kazi iweze kuachia fedha za Serikali ili nazo zifanye kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mpango huu wa mwaka 2015 – 2021 tulisema unakuwa *financed* na shilingi triliioni 107. Tukasema watu binafsi watachangia shilingi triliioni 48. Tumeingia kwenye Kamati, Wizara haina *data* inayoonyesha *private people* wamechangia kiasi gani na hiyo miradi iko wapi? Sasa kama huwezi ku-track miradi iliyochangiwa na wawekezaji binafsi, lakini uliiweka kwenye mpango, hilo ni eneo ambalo lazima huo udhaifu tuweze kuuondoa. Tunataka kuona shilingi triliioni 48 za *private sector* imechangia wapi? Sehemu gani? Mradi gani? Kiwanda gani? Au *project* gani? Kwa hiyo, hiyo naomba kwa kweli tuweze kulii-improve vizuri ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umeme, barabara na afya, tunaomba *speed* ya ukopaji, kwa sababu wakati mwingine fedha ni za watu, kwa hiyo, tuongeze kasi ya kutafuta fedha hii miradi iweze kuendelea. Vijiji tunavyotajiwa ni vijiji ambavyo tunapeleka umeme, vinatugombanisha na wananchi kwamba umeme uko sehemu ya *center*, lakini kwenye vijiji ndani haujaingia. Kwa hiyo, ni vizuri tutafute fedha. Pamoja kwamba tumekopa mpaka tumefikia shilingi triliioni 53, tusiogope kwa sababu deni letu bado linahimilika, tuendelee kufanya hii miradi iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango sijaona mahali ambapo mafunzo kwa vijana yamesitizwa sana. Vyuo vya *VETA* mna mpango wa kuvijenga, lakini kwenye mpango hakuna mahali ambapo pamesitizwa sana. Naomba hapo kwenye Mpango tutakapourekebisha tuweze kuona mafunzo kwa vijana na ajira baadaye inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema mengi, mengi tumeyaandika kwenye ripoti yetu ya Kamati, nafikiri inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Ahsanteni sana kwa michango yenu ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango ambao unatupa dira ya namna Serikali inavyojipanga kwa ajili ya bajeti na pia Mpango wake wa Maendeleo.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya tarehe 6 Novemba, 2019 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.52 jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 6 Novemba, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*